

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 1 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 132

Kuimarisha Ulinzi na Usalama Jiji Dar es Salaam

MHE. CHARLES N. KEENJA : Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne imechukua hatua madhubuti za kuimarisha Ulinzi na Usalama kwenye Jiji la Dar es Salaam kwa kuligawa Jiji kwenye Mikoa na Wilaya za Ki-ulinzi ; na kwa kuwa, hatua hiyo haikwenda sanjari na ile ya kuigawa Mikoa ya Kiutawala:-

- (a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kuligawa eneo la Jiji la Dar es Salaam kwenye Mkoa/Wilaya zinazokwenda sanjari na zile za Ulinzi na Usalama ?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba Viongozi kwenye eneo lenye hadhi zinazotofautiana kunaleta matatizo ya ushirikiano na mawasiliano hatimaye kukwamisha utendaji kazi ?
- (c) Kwa kuwa, zaidi ya 10% ya wananchi wa Tanzania wanaishi Dar es Salaam. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuweka utaratibu mzuri zaidi wa Uongozi kwenye Jiji hilo ?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika hatua za kuimarisha Ulinzi na Usalama kwenye Jiji la Dar es Salaam Serikali iliamua kuligawa eneo katika ngazi ya Mikoa ambapo Wilaya zote tatu za Kinondoni, Temeke na Ilala ni Mikoa ya Kiulinzi na ngazi ya Mkoa kupewa hadhi ya Kanda Maalum ya Ulinzi na Usalama. Hatua za kuligawa eneo la Mkoa wa Dar Es Salaam katika hadhi sawa na zile za Kiutawala bado halijaamuliwa. Hivi sasa Serikali imeunda Kamati Kupitia Muundo wa Uongozi wa Halmashauri ya Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam na kutoa mapendekezo Serikalini.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na kutofautiana kwa hadhi kwa Viongozi kwenye eneo moja, hakujaathiri kabisa utendaji, Ushirikiano na Mawasiliano kwa kuwa Mgawanyiko huo unaendana na mtiririko mzima wa Uongozi katika Idara hizi muhimu za Ulinzi ambazo zinaongozwa na Kanuni na Sheria zake. Hivyo, mgawanyo huu ni katika hatua ya kutekeleza majukumu tu.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu utaratibu mzuri wa uongozi katika Jiji la Dar es Salaam utafikiriwa kutokana na matokeo ya Kamati iliyondwa na Serikali kupitia Muundo wa Jiji la Dar es Salaam ambayo kwa sasa inaendelea na kazi hiyo.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na hasa kuundwa kwa Kamati hiyo. Lakini kutokana na jibu lake kwa sehemu ya B ya swali langu ningependa kujua ni wapi kwingine ambako kuna mpango kama huu ambao Afisa mwenye hadhi kubwa anaripoti kwa Afisa mwenye hadhi ya chini zaidi na Afisa mwenye hadhi ya chini anaweza kumpa maagizo Afisa mwenye hadhi ya juu maana kama hakuna mgongano basi uko njiani waja.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba tuna Kata kubwa sana Kimara, Mbezi Louise, Goba na Kibamba. Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka wa kugawa Kata hizi kabla ya uchaguzi wa mwakani?

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Charles Keenja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa nakubaliana na yeye anachosema hapa ni kwamba unaye *RPC*, *RPC* ambaye anafanya kazi kwa kupokea maelekezo kutoka kwa DC na yeye kwa maana hiyo anaona kwamba huu ni mgongano.

Kwa kawaida Ma-*RPC* wako chini ya Mkuu wa Mkoa lakini kwa sababu ya matatizo ambayo yameonekana yapo katika Mkoa wa Dar es Salaam ilionekana kwamba ni vizuri Mkoa wa Dar es Salaam ukapewa umuhimu wake kwa maana ya kugawanya eneo hilo katika utaratibu wa kiulinzi huu ambao anauzungumzia hapa. Kwa maneno mengine ni kwamba wanapokutana Kamati ya Ulinzi na Usalama pale Temeke au pale Kinondoni au pale Ilala wanakutana pale *DC* ndiye anakuwa Mwenyekiti wa ile Kamati na mle ndani kwa maana ya mfumo huu unaozungumzwa hapa maana yake *RPC* anakuwapo hapo ndani na ndiyo mgongano ambao uanonekana kama unakuwapo pale.

Kwa maneno mengine ni kwamba *RPC* anafika mahali anajiona kwamba hawezi kupokea maelekezo kutoka kwa *DC*.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyojibu hapa, hatupata tatizo lolote katika kufanya kazi hiyo na kama nilivyoieleza hapa Kamati imeundwa ili iangalie vizuri kwamba ni kwa namna gani tunaweza tukaboresha utaratibu huu.

Sasa ameuliza hapa ni eneo gani lingine ambalo limewahi kufanya hivyo, sinalo mimi eneo ninalolifahamu lakini najua kwa mantiki yake ndiyo hiyo.

Amezungumzia habari ya Kata hapa kwamba yeye haoni kuna umuhimu wa kuzigawanya kata zile. Suala la kata hatuna tatizo nalo kabisa sisi tunasema kwamba Kata zitasaidia kwa ajili ya kuimarisha mfumo huu na kama tulivyojibu hapa tunaomb maombi yale yaletwe yote ili tuweze kuyashughulikia yote kwa pamoja na hivyo hivyo tumefanya hivyo kwa upande wa ulinzi kwamba kuna Kata zake na Wilaya zake. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Dar es Salaam ni Jiji ambalo linakua sana inaonekana hata halmashauri za Jiji ambazo zipo pengine zinashindwa hata kufanya kazi sawasawa kulifanya Jiji la Dar es Salaam likaonekana ni Jiji zuri machoni pa watu wengi.

Je, sasa Serikali haioni kwamba wakati pengine umefika kuliundia Jiji la Dar es Salaam Wizara maalum kama nchi nyingine zinavyofanya ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi kwa kuwa na Bajeti ambayo Waziri Maalum atalisimamia?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godfrey Zambani, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu ambao Mheshimiwa Zambani anauzungumzia ni utaratibu ambao mimi nimewasikia wenzetu wa Nairobi wanauzungumzia na wala si kitu cha ajabu sana kwa maana ya kwamba wao wanaona ili wafanye mji ule uweze kufanya kazi kwa ufanisi lile Jiji la Nairobi wameligeuza wakalifanya sasa linakuwa na Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, hivi nilivyozungumza hapa Wizara na Serikali kwa ujumla tumekubaliana kwamba tuunde Kamati ambayo itaangalia mfumo mzima wa kiutawala wapo watu ambao wameboba pale Mzee Mmari ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa TAMISEMI, wako watu kama Mzee Nsakaisi watu ambao wana utaalamu mkubwa.

Mimi nina hakika kwamba tutachukua wazo hili na tutalipeleka kwao kwamba yapo mawazo ya kufikiria kwamba Dar es Salaam iwe ni Wizara ili kuweza kuleta ufanisi zaidi na kama itakubalika basi kwa maana hili ni suala la Sheria ya Serikali basi litakuwa limefanyiwa kazi kwa msingi huo.

Na. 133

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliamua kwa makusudi matumizi ya njia tatu (3) kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam na kwa kuwa, lengo hilo zuri sasa limegeuka kuwa chanzo kipya cha vifo kwa wananchi wetu:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuboresha utaratibu huo ili kupunguza au kuondoa kabisa vifo kwa waenda kwa miguu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuanzisha utaratibu wa njia tatu katika Jiji la Dar es Salaam ulilenga kupunguza msongamano wa magari hususan nyakati za asubuhi na jioni. Utaratibu huu umeweza kusaidia kupunguza msongamano wa magari na wananchi kuweza kuwahi shughuli zao saa za asubuhi na kuwahi kurudi majumbani wao muda wa jioni. Takwimu za ajali zilizotokea katika barabara za Morogoro na Ali Khasan Mwinyi kuanzia tarehe 21 Mei, 2007 hadi Mei, 2008

zinaonyesha kupungua kwa kiasi kikubwa. Kupungua kwa ajali hizo kumetokana na juhusi za Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara juu ya utaratibu huo wa njia tatu.

(ii) Kuweka alama za barabarani (*Road Signs*) kwa watumiaji wa barabara.

(iii) Kuongeza idadi ya Askari wa Usalama Barabarani hasa katika maeneo ambayo njia tatu huanza kutumika na kumalizikia na kwenye vivuko rasmi vya waenda kwa miguu?

(iv) Kuzifanyia matengenezo barabara ndogo ndogo kwa nia ya kupunguza msongamano katika barabara Kuu za Jijini. Barabara zinazohusika na mpango huu ni:-

- Kigogo – Mburahati – Ubongo Maziwa;
- Twiga – Jangwani – Kigogo – Tabata Dampo;
- Vingunguti – Segerea;
- Africana – Njia panda ya Kawe; na
- *Jet Club – Davis Corner – Mtongani.*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri ikaeleweka kwamba mpango wa njia tatu siyo suluhisho la kudumu la tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mikakati ya baadaye ya kudumu ni pamoja na:-

- (i) Kujenga barabara za pete (*ring roads*);
- (ii) Kujenga miji modogo yenye huduma zinazotakiwa nje ya Jiji (*Satellite Towns*);
- (iii) Kupanua vituo vya daladala; na
- (iv) Kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii kuwaomba watumiaji wote wa barabara kufuata na kuzingatia maelekezo ya matumizi ya njia tatu ili kupunguza msongamano na ajali ambazo pia husababisha vifo kwa watumiaji wa barabara.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, anakiri daladala ndiyo chanzo kikubwa kwa ajali za njia tatu. Je, Serikali inachukua hatua gani zaidi kuhusu wanaosababisha ajali hizo?

La pili, kwa kuwa Bima mpaka hivi sasa hawatambui hizi njia tatu na ajal haina miadi. Je wanaopata matatizo hayo waende wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, kama ifuatavyo:-

Ni kweli, nalitambua hilo na ndiyo maana nimelitaja na kutoa tahadhari kwamba madereva wa daladala waangalie sana katika hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kusema kwamba kwa mujibu wa tarakimu tulizokuwa nazo kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba hizi ajali zimepungua na kwa mujibu wa takwimu tulizokuwa nazo wakati tuliporuhusu uendeshaji wa njia tatu kwa shabaha ya kupunguza msongamano wa asubuhi na jioni katika Jiji la Dar es Salaam tulipoanza mwezi Mei mwaka 2007 ajali kwa ujumla zilikuwa 24 na hivi tunazungumza mwezi Mei wa Mwaka huu ajali ilikuwa ni moja kwa maana hii inaonyesha kwa mujibu wa tarakimu tulizokuwa nazo kwamba ajali kwa kweli zimekuwa zinapungua.

Kutokana na watu kuendelea kufahamu utaratibu wa matumizi wa njia tatu lakini bado Serikali na *Traffic Officers* wetu wanachukua hatua kufuatana na mujibu wa Sheria zetu kuwabana hawa madereva wa daladala ambao kwa muda wanakwenda na kukiuka. Kwa hiyo adhabu zipo na kwa kweli wanadhibitiwa.

Kuhusu la pili la Bima si kweli kwa sababu hii ni Sheria kama Sheria nyingine na inatumika na itatumika kwa muda na imetangazwa kwa mujibu wa Sheria ambazo tunazo nchini kwa hiyo si kweli kusema kwamba mashirika ya Bima hayatambui utaratibu huu.

MHE. IDD MOHAMED AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado kuna barabara ambazo hazijaruhusiwa kuwa na njia tatu yaani Barabara ya Kawawa lakini bado madereva wanatumia kwa njia tatu. Je, Serikali inasema katika hili kwa sababu nako ajali pia zinatokea.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshiwa Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge Azzan, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa mazoea ambayo tumeyaona kwa kipindi hiki ni kweli kwamba madereva wa daladala nakiri kwamba wamekuwa wakiukaji na wavunjaji wa Sheria za barabarani na kitu ambacho nimefanya tumeongeza Maaskari barabarani kwa shabaha ya kuwadhiti wale madereva ambao wanakwenda kinyume na taratibu ambazo zimewekwa au Sheria ambazo zimewekwa barabarani na hii aliyoitia Mheshimiwa Azzan Mbunge mimi ninaichukua na nitawaambia watu wetu wajaribu kuitazama na kuifanyia kazi. Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowatangazia jana tumewapokea wenzetu kutoka Kenya na ninasimama sasa kuwatambulisha kwa sababu hawatakaa muda wote wamekuja kututembelea na kwa hiyo wataondoka kabla ya saa nne kwenda katika ziara ya kulitembelea jengo letu.

Kwa heshima kubwa na furaha napenda nimtambulisha kwenu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Kenya Keneth Marende, karibu sana tunafurahi sana kuwa na wewe kama unavyosikia Wabunge wote wamefurahi. (*Makofi*)

Pamoja naye wapo Wabunge wafuatao nitawatamka na kila mmoja asimame ili Waheshimiwa wabunge waweze kumtambua.

Yupo Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Huduma za Bunge Kenya Mheshimiwa Walter Nyambati, karibu sana. (*Makofi*)

Mwingine ni Mwenyekiti wenzetu hawa Tume yao wameiweka halafu wamegawana majukumu. Kwa hiyo, katika Tume hiyohiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Watumishi wa Bunge la Kenya Mheshimiwa Peter Mwachhi. Halafu yupo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mheshimiwa Zakayo Chemioti. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi ya Tume Mheshimiwa Jamly Kamau. Karibu sana. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Ugavi na Manunuzi yaani *Procurement Committee* Mheshimiwa Olago Aluochi. Karibu sana. (*Makofi*)

Mjumbe Mheshimiwa Julius Murgu, karibu sana. (*Makofi*)

Pamoja nao sasa wapo Wataalamu mbalimbali kwa haraka haraka nitasoma tu majina yao, nao ni:-

Ndugu J. Mwangi, Ndugu W. Makate, Mama E. Kamau, Ndugu Sialai, Ndugu G. T. Mwita na Bi. Ofelia Nyambu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nawaomba pia wasimame Maafisa kutoka Ubalizi wa Kenya kule Dar es Salaam Ndugu Patric Nzusi na Ndugu Fredy Zesunda, na mwenyeji wao kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Ndugu Pinda Idara ya Itifaki. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na maombi ya wengi wenu nimeamua kusitisha shughuli za Bunge baada ya matangazo ili saa tano kami tuende ukumbi wa Msekwa, Mheshimiwa Marende Spika wa Bunge la Kenya amekubali kuingea nasi kama mlivyoomba kuhusu mabadiliko ya Maendeleo ya Katiba na Utawala katika Kenya katika Kipindi hiki. Haya yana maana sana kwetu kwa sababu mambo mengi ambayo yanatokea kwa jirani zetu sisi inabidi na sisi tuweze kuyazingatia.

Nilipata maombi mengi jana nikaona ni vizuri basi saa tano hadi saa saba tutafanya shughuli hiyo halafu tukarejea tena saa kumi na moja kama kawaida.

Kwa hiyo, saa tano Msekwa Hall kwa ajili ya kumsikiliza Spika wa Kenya na wakati tukiwa hapo kutakuwa na *interactive session* yaani mtakuwa mnaweza kuchangia na kuuliza maswali na kadhalika na kwa kipindi hicho waandishi wa habari wanakaribishwa pia. Ahsante sana.

Bado tupo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali linaulizwa na Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi. Kwa niaba yake Mheshimiwa Shoka Khamis Juma.

Na. 134

Sheria ya Traffic

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI) aliuliza:-

Kwa kuwa, Waziri Mkuu Mstaafu aliagiza kuwa wakati wa msongamano wa magari barabarani (kati ya saa 12 asubuhi mpaka saa 3 asubuhi) na (saa 10 jioni mpaka usiku) wenye magari watumie barabara tatu ili kupunguza msongamano:-

(a) Je, Serikali inaelewa kuwa, jambo lolote linalowekwa kwa mujibu wa Sheria haliwezi kubadilishwa na mtu bila Sheria husika kubadilishwa?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba endapo gari inayopita upande wa kulia ikipata ajali Mashirika ya Bima yana haki yana haki Kisheria kukataa kulipa madai ya ajali hiyo kwa mujibu wa Sheria ya *Traffic*?

(c) Kama hali hiyo ikitokea je, mwathirika anaweza kupeleka madai yake Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo iliagiza magari hayo yapite kulia

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdulhabibi Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaelewa kuwa jambo lolote linalowekwa kwa mujibu wa Sheria haliwezi kubadilishwa bila ya Sheria husika kubadilishwa.

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Sheria ya usalama barabarani (*The Traffic Act Cap 168 R.E 2002*) inampa Mamlaka Waziri anayehusika na mambo ya Usalama Barabarani kufanya yafuatayo:-

(i) Kufunga upande mmoja wa barabara nakutumia upande mmoja tu wa barabara kwa muda utakaona unafaa.

(ii) Kubadili matumizi ya pande za barabara au sehemu yake na kuamuru zote zielekee upande mmoja kwa muda atakaona inafaa.

(iii) Kufunga barabara yote au sehemu ya barabara kwa magari yote kwa muda atakaona unafaa.

(iv) Kutenga sehemu ya barabara kwa ajili ya kuegesha magari.

(v) Kutenga sehemu ya barabara kwa ajili ya Kituo cha basi, gari ndogo za abiria (*taxi cab*), ukanda wa kupakia na kupakua mizigo.

(vi) Kuweka alama za kuongozea mwendo wa magari barabarani.

Hivyo uamuzi wa Serikali kuamua kutumia njia tatu ili kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ulifanywa kwa mujibu wa Sheria ya usalama barabarani.

(a) Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Bima yanatakiwa kuwalipa fidia wahanga au ndugu wa wahanga wa ajali za barabarani kwa mujibu wa Sheria za Bima.

Kwa mujibu wa makubaliano kati ya mwenye gari na shirika la bima. Hata kama wakati ajali hiyo inatokea mtumiaji wa barabara alikukwa anapita upande wa kulia wa

barabara kwa idhini ya Serikali na katika muda wa kipindi kilichoidhinishwa kutumika kwa barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, mwathirika wa ajali anatakiwa kupeleka madai yake ya fidia kwenye Shirika la Bima ambalo lina mkataba wa Mmiliki wa gari lililopata au kusababisha ajali na si Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wako wananchi waliokwisha kupata ajali kwa utaratibu huo wa njia tatu na Bima ilishindwa kuwalipa. Je, Waziri anasema nini kwa watu hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiwelu kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba ni kinyume na Sheria ya nchi kwamba mashirika ya Bima yakatae kuwalipa kwa sababu ya ubadilishaji wa barabara au matumizi ya barabara unatendeka kwa mujibu wa Sheria na Mamlaka ambayo Waziri amepewa. Kwa maana hiyo, kama Mashirika yanachukua uamuzi wa kutofanya hivyo basi huo ni ujanja lakini wanawajibika kuwalipa. Mheshimiwa Spika, ahsante.

Na. 135

Bei ya Zao la Pareto

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE aliuliza:-

Kwa kuwa, bei ya zao la pareto kwa wakulima hutegemea kiwango cha sumu iliyomo kwenye pareto yaani daraja la kwanza Shs. 1,500/= daraja la pili Shs. 1,200/= na daraja la tatu 900/=-

(b)Je, Serikali inawashirikishaje wakulima wa pareto katika kujua kiwango cha sumu iliyomo ndani ya maua ya pareto inapopimwa kiwandani ili kuwajengea imani kwamba wanalipwa kulingana na ubora uliomo ndani ya pareto yao?

(c) Je, katika msimu wa 2006/2007 ni tani ngapi zilinunuliwa katika kila daraja kati ya yale matatu na ni wakulima wangapi waliolipwa katika kila daraja?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA) alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilithi Mahenge, Mbunge wa Makete, lenye sehemu A na B kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, bei ya zao la pareto kwa wakulima hutegemea kiwango cha sumu iliyomo kwenye pareto iliyoletwa na wakulima na kupimwa kiwandani. Kwa hiyo, pareto huuzwa kwa madaraja kadri ya sumu iliyomo. Ili kulinda maslahi ya mkulima katika upimaji wa sumu ya pareto kiwandani Bodi ya Pareto imeajiri Mkemia ambaye anasimamia na kushuhudia upimaji wa sumu ya pareto ya wakulima kwenye maabara ya kiwanda cha pareto.

Baada ya upimaji taarifa za majibu zinaandaliwa na kurudishwa kwa wakulima husika kwa kadri ya namba ya usajili wa kikundi cha wakulima na kwa kuzingatia takwimu za uingizaji wa pareto kiwandani.

(b) Katika msimu wa 2006/2007 jumla ya kilo 1,597,520 za pareto zilinunuliwa kwa madaraja kama ifuatavyo:-

(i) Daraja la Kwanza shilingi 900 kwa kilo. Kilo 800,560 zilinunuliwa kutoka kwa wakulima 2,650;

(ii) Daraja la Pili Shilingi 700/= kwa kilo. Kilo 355,660 zilinunuliwa kutoka wa wakulima 650;

(iii) Daraja la Tatu Shilingi 500/= kwa kilo. Kilo 245,650 zilinunuliwa kutoka wa wakulima 620; na

(iv) Daraja la Nne Shilingi 360/= kwa kilo. Kilo 195,650 zilinunuliwa kutoka kwa wakulima 435.

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini kama inavyoonyesha katika Jibu lake la Msingi kiwango cha pareto kinachopatikana ni kidogo sana yaani tani moja na nusu. Je, serikali ina mkakati gani wa kuwajengea uwezo wananchi hawa au wakulima hawa wa kuweza kupata mbegu bora kuweza kuwajengea mabaloni yaani *pyrethrum dries* na kuweza kuwa na vyama vya Ushirika yaani *Pyrethrum Cooperatives Societies*? Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo wananchi hawa kuweza kuwa na barabara zinazoweza kupitika hawa wakati wa masika ili kuweza kusafirisha pareto inayopatikana?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, kama ifuatavyo na nitapenda niyajibu yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kujenga uwezo wa wakulima hasa kwenye ushirika nafurahi kwamba Mheshimiwa Mbunge analiona hili kwa sababu sisi wenyewe katika Serikali tumeamua kufufua ushirika.

Kitakachofanyika sasa ni wakulima wenyewe kuandaliwa katika vyombo hivi vya ushirika na kuanzisha ushirika kwa kweli hautaanzia Serikalini, utanzia palepale kwa wakulima wenyewe.

Tunachosema ni kwamba, tutawasaidia kama Serikali ili kuhakikisha kwamba ushirika wa wakulima wa pareto unaanzishwa ambao ndio utakaokuwa mkombozi tu sio tu kwa ajili ya kuzalisha pareto nyingi, lakini pia kulinda maslahi ya wakulima wa pareto ambayo hata nami nayaona yanayumbayumba kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara na huduma nyingine za kuongeza uzalishaji wa zao la pareto, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba bado ipo nafasi katika program zetu za *DADPs*, wakulima hawa wanaweza kusaidiwa, wakaweka taratibu za kuomba misaada Serikalini kupitia katika miradi au mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya husika. Kwa hiyo, nafasi hii ipo na naamini kwamba tukiwashauri kwa pamoja namna hiyo basi mipango hii italetwa Serikalini na tutawasaidia kuongeza uwezo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, tayari kuna utaratibu ambao tumefanya kupitia katika Chuo chetu cha Kilimo cha Uyole kuwasaidia wakulima kupata huduma bora za ugani ili maua ya pareto wanayotoa yaweze kuwa yanafikia ubora huo. Hiyo program inaendelea hivi sasa kushirikiana na chuo cha Uyole.

Na. 136

Vituo vya Wazee Wasiojiweza

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Kwa kuwa vituo vya Wazee wasiojiweza hapa nchini ambavyo vilianzishwa kuwasaidia wazee na wale wenye magonjwa ya ukoma hasa kwenye maeneo ya Manispaa ya Tabora (Ipuli, Nzega na Iduguta) viko kwenye hali mbaya na majengo mabovu na kwa kuwa idadi ya watu kwenye vituo hivyo huongezeka mara kwa mara kutokana na kuzaana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kuongeza majengo kwenye vituo hivyo ili kuondoa adha wanayopata?

(b) Je, ni idadi gani ya watoto waliozaliwa baada ya kuanzishwa kwa vituo hivyo ambao wanaishi kwenye mazingira magumu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kuimarisha vituo vilivyopo na kuongeza vituo vingine vipya Mikoani?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, makazi ya Ipuli yalianzishwa mnamo mwaka 1969 na Halmashauri ya Mji wa Tabora yakiwa na wakazi 350 katika eneo la Malabi. Idara ya Ustawi wa Jamii ilianza kuyahudumia makazi haya 1974. Mwaka 1975 makazi haya yalihamishwa Ipuli ambako ndiko yaliko hadi sasa. Makazi haya yana jumla ya majengo kumi na tano. Serikali itaendelea kukarabati majengo hayo na kuboresha huduma katika makazi haya na makazi mengine yaliyopo.

Hata hivyo, kwa kuwa sera ya Serikali ni kuwatunza wazee na wasiojiweza katika familia na jamii zao huko waliko, Serikali bado haijaona haja ya kuendelea kuongeza majengo mapya katika makazi haya. Makazi ya Iduguta – Nzega yenye kaya 26 yanaendeshwa na Taasisi isiyo ya Kiserikali (Shirika la Dini), hivyo, Serikali inaajibika kwa ushauri wa kitaalam tu.

(b)Mheshimiwa Spika, makazi ya Ipuli, yana wakazi wapatao 121. Kati ya hao watu wazima ni 90 na watoto 3. Aidha, makazi ya Iduguta yana jumla ya kaya 26, wakazi 87 kati yao watoto ni 47.

(c)Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mfupi wa kuimarisha makazi ni kuendelea kufanya ukarabati wa makazi na kuboresha huduma kulingana na uwezo wa Serikali. Aidha, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) hapo juu. Sera ya Serikali ni kuwatunza wazee na wasiojiweza katika familia na jamii zao huko waliko. Kwa msingi huo Serikali inaandaa mpango wa kuzijengea uwezo jamii na familia ili kuwahudumia wazee pale walipo badala ya kuwaweka katika makazi. Kuwapeleka wazee wasiojiweza itakuwa ni hatua ya mwisho kabisa.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya kutia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa hivi karibuni Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara kwenye eneo hilo na kujionea hali halisi ilivyo lakini pamoja na hayo makambi haya yalikuwa na nia nzuri ya kuwasaidia wale ambao wana ukoma, wana maradhi makuu na kwa kuwa Baba

wa Taifa alifanya kazi nzuri sana kuwakusanya na hawa watu hawajui mahali pa kwenda na wala hawana ndugu.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutelekeza makambi hayo kunachangia sana ongezeko la ombaomba mitaani? Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuwakusanya hao? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Baba wa Taifa aliwakusanya na kuwaweka wale wenye ukoma katika makambi ili kuweza kulelewa. Kwa sasa hivi tunavyoona ni kwamba, wale wagonjwa wa ukoma walio katika makambi idadi yao inapungua sana kutokana na huduma bora zinazotolewa na Wizara, wanaonekana kuongezeka katika yale makambi na kuongeza mzigo mkubwa ni wale ndugu ambao wanakwenda kukaa nao na hivyo kuwa tegemezi kwa wale wenye ukoma.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nia yetu ni njema ya kuhakikisha kwamba watu wenye ukoma wanalelewa vizuri.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutaweza kuwasaidia waliopo katika makambi lakini bado tunatoa ushauri kwamba wale ambao hawana ukoma na wanakaa na wazee wenye ukoma katika makambi wajitegemee, lakini kinachotokea ni kwamba, wale ambao ni tegemezi na wale wenye ukoma wote wanategemea ule msaada tunaowapa wenye ukoma badala ya kwenda kufanya kazi na kujitegemea, hivyo wanasababisha msaada tunaowapa kuwa ni mdogo kwa sababu tegemezi wanakuwa ni wengi. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa njia inayotumika sasa ya kupeleka huduma kwa walemavu hawa hupewa mkoa, halafu wanapeleka kwa walemavu moja kwa moja. Je, Serikali haioni kwamba njia hii haina tija ni bora sasa fedha hizi zipelekwe kwenye Halmashauri za Wilaya moja kwa moja?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba jinsi utaratibu ulivyowekwa wa kupeleka fedha katika makambi hauna tija na kwa kuzingatia hilo Wizara inafanya utaratibu sasa hivi wa kuhakikisha kwamba kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa mpaka Wilaya kunakuwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii na Afisa huyo ambaye atakuwa kule Wilayani atakuwa chini ya TAMISEMI kwa maana hiyo fedha itakwenda moja kwa moja katika Wilaya na itahudumia zile kambi zilizo katika Wilaya husika.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ugonjwa wa ukoma unaambukiza je, ni kiasi gani watoto wanaozaliwa na kuishi katika nyumba za wagonjwa wa ukoma wako salama?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa ukoma ni kweli unaambukiza na huwa unaambukiza kutokana na kukutana

baina ya ngozi kwa ngozi kwa muda mrefu lakini inapotokea mama anapokuwa na mtoto anakuwa yuko katika matibabu basi inakuwa si rahisi kumwambukiza mtoto na kama itatokea mtoto ana dalili za kuambukiza basi inabidi awe anaonana na wataalam na kuona kama amembukizwa au vinginevyo lakini ugonjwa huu mara anapokuwa anaanza kutumia dawa unakuwa hauambukizi tena.

Na. 137

Kuangamiza Mazalio ya Mbu

MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA) aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye miaka ya sitini moja ya njia zilizokuwa zikitumika ili kupambana na mbu ilikuwa ni kuwaua mbu kwenye mazalia yake:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa mpango ule sasa unafaa kuanzishwa tena ili kupambana na mbu?

(b)Kwa kuwa zamani dawa ya *DDT* ilitumika katika kuangamiza mazalio ya mbu lakini sasa hivi dawa hiyo haitumiki tena, je, Serikali inatoa kauli gani juu ya matumizi ya dawa ya *DDT* kwenye mpango huo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba dawa ya *DDT* haijawahi kutumika kuangamiza mazalia ya mbu hapa nchini. Dawa hii iliwahi kutumika kuua mbu wapevu wanaoingia majumbani kabla ya kusitishwa katika miaka ya 1970.

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeanzisha Mpango wa Uwiano wa Kudhibiti mbu waenezo malaria kwa kutumia njia mbalimbali ambazo ni:-

- Kutumia vyandarua vilivyowekwa dawa ya viuatilifu;
- Kupulizia dawa majumbani;
- Kuboresha mazingira na kuondoa mazalia kwa kuishirikisha jamii; na
- Kupuliza dawa za kuua viluwiluwi kwenye madimbwi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kutoka nchi nyingine katika kutokomeza malaria kwa kutumia *DDT*, Serikali inakusudia kuanza kutumia dawa hiyo pamoja na viuatilifu vingine ili kutokomeza malaria nchini, matumizi ya *DDT* nchini yatazingatia mambo yafuatayo:-

(i) *DDT* itatumiwa kwa uangalifu kulingana na mpango wa usimamiaji na utekelezaji na pia kulingana na Mazungumzo ya Stockholm na Tamko la Shirika la Afya duniani kuhusu matumizi sahihi ya *DDT*. Baraza la Mazingira (*NEMC*) litakuwa na wajibu wa usimamiaji wa maizngira wakati wa unyunyiziaji wa *DDT*.

(ii) Baraza la Taifa la Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira itatoa mwongozo na kusimamia tathmini ya athari za Kimazingira (*Strategic/Environmental Impact Assessment*) kabla ya kuanza kutumia dawa ya *DDT*. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

(iii) Jamii itapewa mafunzo na kuhamasishwa kuhusu utumiaji wa *DDT* kwa kunyunyizia ndani ya nyumba.

(iv) Kwa kuanzia *DDT* itanyunyuziwa katika Wilaya zile zinazotarajiwa kupata milipuko.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kuna nchi ambazo zinatumia *DDT* katika mapambano na malaria na pia kuna nchi ambazo hazitumii dawa hii katika mapambano yake na malaria na kwa kuwa sasa Tanzania inataka kutumia dawa hii katika mapambano na malaria. Je, Tanzania yenyewe imefanya tathmini yoyote kubaini faida au hasara ya matumizi ya dawa hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa mpango huu wa mapambano ya malaria umeleta mafanikio kule Zanzibar. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutanua maeneo ya kupuliza dawa majumbani ya *in-door-spraying* ili gonjwa hili la malaria liweze kutokomezwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna nchi ambazo zimetumia *DDT* kwa mfano nchi nyingine za Afrika Kusini, Zimbabwe, Swaziland na Botswana zimetumia *DDT* kwa muda wa miaka ishirini sasa na zenyewe zimepata mafanikio makubwa lakini vilevile hata jirani zetu Uganda wanatumia *DDT*. Utafiti uliofanywa kuhusu faida na hasara ni kwamba, *DDT* inalenga *long term effect* yaani *side effect* yake inachukua muda mrefu lakini ukiitumia inaua mbu isipokuwa hasara zake ni kwamba inapoingia katika ardhi inaharibu ule uoto wa asili, kwa hiyo inaharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa pili ni kwamba tunaweza kupima kuona kwamba tutumie *DDT* au tuache maana wagonjwa wanaokufa kwa malaria ni

wengi sana ambapo watoto na watu wanakufa kwa muda mfupi ukilinganisha na ile *effect* ambayo inapatikana kutokana na athari za *DDT*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Mheshimiwa Salim alitaka kujua ni kweli Zanzibar wamefanya vizuri sana kwa kutumia *In-door-spraying*. Kwa hiyo, wameweza kupunguza kwa asilimia kubwa sana na kudhibiti ugonjwa huu wa malaria na sisi tunajifunza kutoka kwao lakini tatizo lililopo ni kwamba Zanzibar tunatumia *icon* ambayo tunaitumia huku Bara.

Tatizo ni kwamba nchi ni kubwa na *icon* ina gharama kubwa sana kwa hiyo hatuwezi kutumia kama wanavyotumia kule Zanzibar. Ndiyo maana sisi tunaanza ku-*opt* kwa *DDT* ambayo ni rahisi kama ikitumiwa vizuri na kwa uangalifu tunaweza kupunguza kwa asilimia kubwa sana malaria kwa upande wa huku Bara.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa huko nyuma hasa kwenye miaka ya 80 na 90 utaratibu wa kuua mazalia ya mbu kwa kutumia dawa pia ulitumika katika Jiji la Dar es Salaam na Tanga na kwa kuwa katika majibu yake anasema Baraza la Mazingira ndiyo chombo cha kusimamia. Kwa vile mipango ya nyuma ilishindikana kwa sababu ya kukosa watu waadilifu na hasa katika suala gumu na ambalo linaweza kuwa na madhara pande zote mbili. Je, ni chombo gani kitakachosimamia utekelezaji wa mradi huu ambao kwa kweli ni wa manufaa kwa nchi nzima?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, jukumu la kufanya *spraying* au la kuua mazalia ya mbu kwa kutumia dawa ambayo tulikuwa tunatumia zamani tulikuwa tunatumia *pyrethrum spraying* ilikuwa tunafanya Wizara ya Afya, lakini kama mnavyofahamu kwamba suala hili lazima tushirikiane na wenzetu wa mazingira ili kuona kwamba ile shughuli inafanyika kwa utaalim kwa maana hiyo Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ina maana tutafanya kazi pamoja kuweza kuhakikisha kwamba wataalam wa afya watafanya ile kazi ya kufanya *spraying* lakini wakati huo huo wataalam wa mazingira kupitia *NEMC* watakuwa wanatuangalia na kushirikiana na sisi kuona kwamba tunafanya hii kazi ikiwa ni salama kwa wananchi na wakati huo huo isilete madhara ya kuharibu mazingira kama nilivyosema hapo mwanzo.

Na. 138

Kitendo cha Kumweka Mtu Kizuizini

MHE. RIZIKI OMAR JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Mkataba wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa ni kosa kwa mtu yeyote kuadhibiwa kabla hajatiwa hatiani:-

Je, Serikali haioni kuwa kumweka mtu kizuizini kwa kipindi kirefu kabla ya kuhukumiwa na kutiwa hatiani ni kumvunjia haki yake ya kibinadamu?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge neno kizuizini katika swali hili limetumika kuelezea mtu anayewekwa rumande akisubiri kusikilizwa kwa kesi dhidi yake pale anapotuhumiwa na kushtakiwa kwa kosa la jinai. Kwa kuzingatia tafsiri hi napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, nchi yetu inafuata misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu. Ili kukidhi hilo Katiba yetu imeainisha haki za msingi za binadamu ili ziweze kuzingatiwa na vyombo vya dola katika utekelezaji wa majukumu yake. Sheria zote zinazohusu kanuni na taratibu za kushughulikia makosa ya jinai zinazingatia misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa sheria zetu, mtu anapotuhumiwa kutenda kosa la jinai na taarifa kutolewa kwa vyombo vya dola, anaweza kukamatwa na kupelekwa polisi kwa uchunguzi wa tuhuma dhidi yake. Katika hatua hii, baada ya kupima uzito wa tuhuma wanaweza kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Ikiwa tuhuma zilizotolewa zinahusu makosa madogo mtuhumiwa anaweza kuachiwa kwa dhamana ya Polisi ili ahudurie Mahakamani katika muda na mahali kama ilivyoandikwa katika hati ya dhamana.

(b) Ikiwa mtuhumiwa atalazimika kubaki chini ya Polisi kutokana na makosa ambayo dhamana hairuhusiwi kisheria, Polisi watamfikisha Mahakamani ndani ya kipindi cha masaa ishirini na nne au mapema iwezekanavyo wakati wakiendelea na uchunguzi wa tuhuma husika. Aidha, Polisi wanayo mamlaka kisheria baada ya kuchunguza tuhuma na kujiridhisha kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kuhusu tuhuma kumwachia mtuhumiwa huru.

Mheshimiwa Spika, pale ushahidi uliokusanywa unapotosheleza na kuonekana kwamba kuna haja ya Mahakama kusikiliza shauri la jinai na kulitolea uamuzi, shauri husika hufunguliwa Mahakamani ambapo mashahidi wa pande zote huitwa kutoa ushahidi na hatimaye Mahakama hutoa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua zote hizi mtuhumiwa anaweza kuwekwa rumande kutegemeana na kosa analotuhumia nalo. Lengo la kumweka mtuhumiwa rumande ni kulinda usalama wake, kulinda usalama wa jamii dhidi ya vitendo vya kijinai na pia kutoa nafasi kwa vyombo vya upelelezi kufanya uchunguzi wa kosa pasipo kuingiliwa na mtuhumiwa au kuzuia mtuhumiwa asiingilie shughuli za upelelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kwa baadhi ya makosa ya jinai sheria inatoa nafasi kwa mtuhumiwa kupata dhamana. Dhamana hiyo imezuiliwa kwa baadhi ya makosa makubwa ya jinai na kwa kuzingatia mazingira ya makosa anayotuhumiwa kuyatenda.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, nchi yetu bado inazingatia suala zima la utawala wa sheria na haki za binadamu katika utekelezaji wa majukumu yake.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kwa mujibu wa sheria na mamlaka waliyonayo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wana nafasi ya kumweka mtu ndani kwa muda wa masaa 48 kabla ya kufikishwa Mahakamani na wakati mwingine mtu yule huweza kuachiwa palepale kituoni Polisi kwamba hana hatia. Je, hapo mwananchi yule anakuwa hajavunjiwa haki yake ya kibinadamu na adai fidia gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tuko katika mfumo wa Vyama Vingi na mara nyingi Wakuu wa Mikoa huwa wanateuliwa na Rais anayetokana na Chama kinachoongoza Serikali. Je, hakuna haja ya kufanya marekebisho ya sheria ili iendane na mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa? (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sheria inampa uwezo Mkuu wa Mkoa kuweza kumweka mtu ndani kwa masaa 48 na baadaye ndiyo kumpeleka Mahakamani lakini ukweli ni kwamba lazima kuwe na kitu kilichomfanya Mkuu wa Mkoa achukue hatua hiyo. Endapo baadaye ushahidi utathibitisha kwamba hakuna kitendo kilichotendeka lakini wakati akitenda tendo lile kulikuwa na ushahidi wa kutosha kumfanya Mkuu huyo achukue hatua hiyo ya kumweka ndani kwa masaa arobaini na nane, hakuna fidia yoyote anayoweza kupata mtu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kuhusu mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Wazo alilotoa Mheshimiwa Mbunge ni zuri tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Katiba amesema mtu huwekwa rumande ili kutoa nafasi ya upelelezi kukamilika na kwa kuwa makosa ya mauaji hayana dhamana.

Je, upelelezi hauna kikomo kwa sababu watu wanakaa zaidi ya miaka mitano gerezani wakati kesi zao hazijasikilizwa? (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika makosa ya mauaji dhamana hairuhusiwi. Lakini kama nilivyosema sheria zetu na taratibu na kanuni zinazingatia Katiba ya nchi na hasa haki za binadamu.

Kwa hiyo, vyombo vinavyohusika vinapaswa vihakikishe kwamba vinakamilisha upelelezi wao mapema iwezekanavyo ili yule mtu ambaye yuko ndani aweze kutendewa haki.

Na. 139

Wananchi Kubambikizwa Kesi

MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA)
aliuliza:-

Kwa kuwa vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti kwamba, kuna wananchi wanaobambikizwa kesi:-

(a)Je, ni Mkoa gani unaongoza kwa kesi hizo?

(b)Je, kwa kipindi cha miaka mitano mpaka sasa ni wananchi wangapi walibambikizwa kesi za aina tofauti tofauti?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina takwimu za matukio yanayoripotiwa na vyombo vya habari kuhusiana na wananchi wanaodai kubambikizwa kesi. Hii inatokana na ukweli kuwa Wizara ikipokea malalamiko hayo huyafanyia kazi mara moja.

Hata hivyo, malalamiko mengi baada ya kuyafanyia uchunguzi hubainika kuwa hayana ukweli na yale machache yenye ukweli taratibu za kisheria huchukuliwa mara moja.

(b) Hatuna takwimu zinazoonyesha idadi ya wananchi waliobambikizwa kesi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na aina ya kesi walizobambikizwa.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kama anazo taarifa zilizothibitishwa kuwa ni za kweli juu ya ubambikizaji wa kesi tutamshukuru akiwasiliana nasi ili Wizara yangu iweze kuziangalia na kuona jinsi ya kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sijaridhika na majibu ya Serikali na inasikitisha kwamba Serikali imekiri kuwa haina takwimu za taarifa za kesi.

Aidha ni vizuri Serikali iwe na utaratibu wa takwimu za kesi ijulikane yapi na malalamiko na zipi ni za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, sasa nina maswali mawili ya nyongeza mawili.

Je, Serikali inafahamu kuwa wafuasi wengi wa Vyama vya Upinzani na wale hasa wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi hubambikiziwa kesi mbalimbali zikiwemo za jinai na hasa kwa kile kipindi cha uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali hutoa fidia gani kwa wale waliobambikiziwa kesi na hutoa adhabu gani kwa wale ambao wamebambikizia wenzao kesi? *(Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA): Mheshimiwa Spika, hatuna taarifa yoyote kwamba, kuna wafuasi wowote wa Vyama vya Upinzani ambao wamebambikiziwa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwa sababu hatuna taarifa hiyo hatuwezi kusema ni fidia gani ambayo watu wa namna hiyo wanaweza kupata. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea muda umetubana kidogo.

**Matengenezo ya Barabara
ya Galula – Magamba - Namkukwe**

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA aliuliza:-

Kwa kuwa kumbukumbu za taarifa za Wizara ya Miundombinu zinaonyesha hatua za mwisho kabisa za upembuzi yakinifu kuhusu barabara ya kuanzia Njiapanda ya Galula – Magamba – Muheza hadi Namkukwe imeshakamilika:-

Je, Serikali inawapa matumaini gani wananchi wa Jimbo la Songwe kwa kutamka ni wakati gani hatua ya ujenzi wa barabara hiyo utanza?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Galula – Magamba – Namkukwe yenye urefu wa kilometa 57 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mbeya. Barabara hii ilifanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2004/2005 na baadaye ikafanyiwa usanifu wa kina mwaka 2006/2007. Matokeo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina yalionyesha kuwa barabara hii inakidhi vigezo vyote vya kiuchumi na kijamii kujengwa kwa kiwango cha changarawe. Makisio ya gharama za ujenzi kwa mwaka 2007 zilikuwa Sh. 9bn/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha zinazohitajika kujenga barabara yote ni nyingi, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitumia kiasi cha Sh. 147m/= kwa matengenezo ya barabara hii. Katika mwaka ujao wa fedha wa 2008/2009, Serikali inategemea kutumia jumla ya Sh. 152m/= kwa matengenezo ya barabara hii.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yanaleta matumaini. Ni kweli kabisa barabara hiyo imeshaanza kutengenezwa na naipongeza Serikali kwa kutekeleza azma yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sehemu ambako barabara hiyo imeanzia kuna sehemu tatu ambazo ni korofi na bahati nzuri Naibu Waziri alipita katika sehemu hizo na katika Bunge hili. Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba sehemu hizo zitashughulikiwa kwa kufunikwa kwa lami na sehemu hizo bahati nzuri ndiko ambako zile changarawe zinakotokea, magari ndiko yanakopita.

Je, Waziri anaweza kuwathibitishia wananchi wa Jimbo la Songwe kwamba sehemu hizo zitashughulikiwa kabla ya mwisho wa mwaka huu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikiri tu kwamba mimi binafsi niliwahi kupita katika barabara hiyo, na nilibahatika kufanya kazi katika Mkoa wa Mbeya kwa kipindi cha miaka sita. Kwa hiyo, ninakuelewa sana katika maeneo hayo.

Sasa kuhusiana na swali kwamba katika maeneo hayo korofi yanaweza yakashughulikiwa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kama nilivyoeleza kutokana na ufinyu wa Bajeti ndiyo maana tunatenga fedha kidogo kidogo mpaka tuhakikishe kwamba barabara hiyo inapata ukamilifu wa kupitika kwa uhakika.

Kwa hiyo, niendeleo tu kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendeleo kushirikiana naye kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana na eneo hilo litakuwa linaangaliwa hatua kwa hatua.

Na. 141

Mitambo ya Mawasiliano ya Simu - Njombe

MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)
aliuliza:-

Kwa kuwa, mitambo ya mawasiliano ya simu ni muhimu sana katika Jimbo la Njombe Magharibi, kwa ajili ya kukuza uchumi hasa mawasiliano ya masoko:-

(a) Je, ni lini mitambo hiyo itafungwa katika Jimbo la Njombe Magharibi?

(b) Je, ni mitambo mingapi imejengwa katika Tarafa za Wanging'ombe, Mdandu na Imalinyi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *CELTEL* imejenga mnara katika eneo la Wanging'ombe na Ilembula na kufikisha huduma ya mawasiliano katika Majimbo hayo na maeneo jirani. Kampuni hiyo inafanya tafiti za masoko katika Tarafa za

Imalinyi na Mdandu ili kupeleka huduma na kuondoa matatizo ya mawasiliano katika Tarafa hizo ifikapo Februari, 2009. Katika Tarafa ya Wanging'ombe kuna mitambo (minara) miwili, (Wangingombe na Ilembula) na Kampuni hiyo inaendelea kufanya utafiti za masoko kwenye Tarafa nyingine ili kujenga minara.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya simu ya *VODACOM* imeunganisha baadhi ya maeneo ya Jimbo la Njombe Magharibi na ina mpango wa kuongeza wigo wa mtandao wake katika maeneo mengine ya Jimbo hilo. Aidha, Kampuni hiyo tayari ina mitambo mitatu (3) ya mawasiliano katika Tarafa ya Wanging'ombe, na ina mpango wa kujenga mtambo wa mawasiliano katika Tarafa ya Mdandu ambao utatoa huduma ya mawasiliano pia katika Kata ya Imalinyi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Kampuni ya *ZANTEL* imefikisha mawasiliano katika maeneo ya Wanging'ombe, Ilembula na Imalinyi yaliyoko Njombe. Aidha, Kampuni hiyo itafanya utafiti katika maeneo mengine Wilaya Njombe ili kufikisha huduma za mawasiliano ifikapo mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TIGO* tayari imeanza mkakati wa kuweka mitambo ya mawasiliano katika maeneo ya Njombe Magharibi hususan katika eneo la Wanging'ombe ambalo utafiti wa awali umefanyika na kubaini kuwa linafaa. (*Makofi*)

SPIKA: Nani hajauliza sana maswali Mheshimiwa Devota Likokola. (*Makofi*)

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, Makampuni hayo yanajenga minara katika maeneo mbalimbali; na kwa kuwa Makampuni hayo katika minara yake yanaweka walinzi; na kwa kuwa thamani ya minara ile ni kubwa na vibanda ambavyo walinzi wanakaa kulinda minara ile inatia huruma.

Je, Serikali inaweza ikayaamuru Makampuni hayo yajenge vibanda vizuri kwa ajili ya walinzi wale ili kujenga hadhi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba tutawaomba wenzetu waone umuhimu wa kuboresha sehemu wanazo kaa walinzi wale. Lakini ieleweke kwamba walinzi pale kazi yao ni kulinda siyo kulala. Isipokuwa tutawambia wenzetu waboreshe maeneo yale ili walinzi wakae mahali pazuri. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita, matangazo machache.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Kanuni gani?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Kwa kutumia kanuni ya 68(7) wakati anazungumza na kujibu swali hapa Bungeni, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametamka kwamba Serikali haina taarifa yoyote ya kesi za kubambikiza.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ni shahidi Wabunge wote tumegawiwa taarifa ya Jaji Kisanga, ametembea katika magereza yote nchini, taarifa ya Jaji Kisanga imeeleza wazi kwamba kuna kesi nyingi za kubambikiza.

Je, Serikali inataka kutuambia katika Bunge hili kwamba haina taarifa ya Jaji Kisanga ambayo imelipiwa kodi na Watanzania wote? Serikali haina taarifa ya watu ambao wamebambikiziwa kesi hizo ndiyo maana haikufuatilia utekelezaji wa maelekezo na mapendekezo ya Jaji Kisanga? (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza, suala hili halihitaji Mwongozo wa Spika kwa sababu kinachohojiwa hapa na ambacho kwa bahati mbaya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa amekinakili kwa kukosea pia ni masuala ya kuwekwa kizuizini au kuwekwa ndani na kubambikiziwa kesi kwa misingi ya kisiasa. Linaweza likaleta mjadala mpana.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Dr. Slaa kama bado anataka kulifuatilia atumie Kanuni ambayo nitamruhusu aweze kutoa kauli wakati wa Kuahirisha Bunge (*adjournment*). Ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa tunaendelea, wageni walioko Bungeni pamoja na wale Waheshimiwa niliokwishawatangaza sasa wapo wafuatao:- Wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud ni Bwana Shekan Hilary, Bibi Mosa Nasor na Bibi Tuma Shelukani wametoka Muscat. Wale pale karibuni sana.

Yupo pia bi Ubwa Masoud anasema ni mlezi wake, karibu sana. Haya mambo ya Kizanzibar sijui mlezi wake vipi. Yupo Bwana Ali Said na Musa Anthony pia wale pale, karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Yupo mgeni wa Mheshimiwa William Shellukindo Bwana Sostenesi Koloa ambaye ni Katibu wake kule Jimboni yule pale, karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa

Emmanuel Luhahula ni Mzee Yona Nuhu mstaafu na ni asiyeona, karibu sana angalau anasikia nini kinaendelea hapa.

Pia, Mwalimu Wayala ndiyo amemsindikiza Mzee Yona. Ahsante sana Mwalimu Wayala kwa kujitolea. *(Makofi)*

Wapo katika *gallery* washiriki 50 wa mafunzo ya kidini kutoka Shirika la Donbosco hapa Dodoma. Naomba wasimame ili Waheshimiwa Wabunge wawatambue Donbosco. Ahsante sana na karibuni sana.

Wapo washiriki 80 kutoka Asasi za kiraia wanaendelea na maonyesho katika Viwanja vya Bunge wale wa AZAKI. Naomba wasimame tafadhali, wale pale. Karibuni sana. Tunafurahia ushirikiano mzuri mlionao na Bunge hili na pia shughuli mnazozifanya ambazo zinasaidia kwenye ujasiriamali na pia haki za raia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 33 kutoka Chuo cha Biashara Dar es Salaam *(CBE)*. Naomba wasimame, wale pale, karibuni sana. Safari ndefu ya kutoka Dar es Salaam hadi hapa Dodoma Bungeni tunafurahi sana mnakuja kujionea wenyewe demokrasia ya nchi yetu inavyofanya kazi. Karibuni sana na muendeleo kuwa nasi kama mlivyoomba na kesho na kesho nadhani mtakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo kwa ajili ya mafunzo kuhusu Bunge na linavyofanya kazi, yatakayotolewa na Maafisa katika Idara yetu ya Habari na Elimu ya Umma ya Bunge.

Sasa matangazo ya Kikao. Mheshimiwa William Shellukindo Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane leo tarehe 1 Julai, 2008 saa saba mchana Ukumbi Namba 227 katika jengo la utawala. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Kamati ya Nishati na Madini saa saba mchana Ukumbi Namba 227 jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo langu kwamba nitasitisha Shughuli za Bunge asubuhi hii halikuwa na maana kwamba shughuli inayoendelea ya wachangiaji katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwamba wachangiaji sasa wamefutwa, hapana, tutaendelea nao jioni.

Wachangiaji hao wa jioni ni pamoja na Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Magalle John Shibuda na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. Watapata nafasi ya robo saa kila mmoja kuanzia pale saa 11.00.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na zile hatua nyingine ili kuhitimisha majadala wa Bajeti hiyo jioni ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo na sina lingine ila sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(Saa 4.21 Asubuhi Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma na wakati huo huo Mheshimiwa John Magale Shibuda, ajiandae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hotuba hii ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitoe pongezi kwa Mawaziri wawili, kwa kazi nzuri wanayofanya na naomba uniruhusu niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri ambayo anatumia sisi Watanzania na hasa baada ya kupokea kijiti kutoka kwa Mzee wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, moja ya maneno aliyoyatumia kwa ruksa yako, naomba uniruhusu ninukuu, yanasema:-

“Ndugu zangu, mkiona natembea kifua mbele, mkiniona nasimama kwa kijiamini, ni kwamba nimesimama juu ya mabega ya miamba iliyotutangulia, Mwalimu Julias Kambarage Nyerere, Mzee Ali Hassan Mwinyi na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa”.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu aliwataja viongozi hawa wakuu kwa sababu ndiyo msingi wa maendeleo na matunda ambayo sisi Watanzania leo tunayo lakini pia ni msingi wa amani tuliyonayo leo.

Mheshimiwa Spika, uniruhusu, niwatakie kila la kheri, Mzee wetu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi lakini pia nimitakie kheri Mzee wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote yanayosemwa, lakini ni vizuri kwa kweli na lazima tuwe na fadhila kwa viongozi wetu hawa wakuu. Niiombe Ofisi hii, kwa sababu ndiyo inayowatunza, kwa kweli iendelee kuwatunza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Mkapa, alituachia uchumi ambao umesimama imara. Tulikuwa hatuaminiki na hatukopesheki, leo tunakopesheka vizuri na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu huko anakokwenda, anatembea kifua mbele kwa sababu ya msingi mzuri uliowekwa na hawa waasisi wetu hasa Mzee Benjamin William Mkapa. Namtakia kila la kheri huko aliko na tunaomba msaada wake wa mawazo ili na sisi tuwe kama yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania hasa sisi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunao utaratibu ambao naona unaendelea. Alipong'atuka Baba wa Taifa, watu walisema huyu Mzee hakutusaidia sisi Watanzania. Alipomaliza muda wake, Mzee Mwinyi, watu wakasema huyu Mzee Mwinyi hakutusaidia. Hivyo hivyo Mkapa, baada ya muda wake Watanzania tukasema. Lakini inawezekana kwa sababu ya utaratibu huu tunaokwenda nao, hata Rais Kikwete atakapomaliza kwa sababu ya staili hiyo hiyo, watasema mzee huyu hakutusaidia. Niwaombe sana Watanzania, tabia ambayo inajengeka sasa ya kukosa uaminifu lakini ya kukosa imani kwa viongozi wetu, tusifike huko.

Mheshimiwa Spika, lakini ndugu zangu, sisi Wakristo huwa tunasali, kama si kusali tuna wimbo, nafikiri ndugu yangu hapo, Mheshimiwa Dr. Slaa, anaweza kunisaidia. Kuna wimbo unasema hivi, sitauimba ila nitausema tu.

SPIKA: Huruhusiwi kuimba.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika na mimi nimesema sitaimba.

Unasema hivi:-

“Kama Mungu angehesabu makosa yetu sisi binadamu, kama Mungu akihesabu makosa yetu, hakuna mtu ambaye angesimama mbele yake kwa sababu sote sisi tuna upungufu”.

Hata ndugu zangu, upande wa kule, wana upungufu. Ni vizuri tukasahihishana. Mheshimiwa Spika, naomba sana, Bunge lako Tukufu, lina heshima yake kubwa mno, Watanzania na wananchi wengine huko nje wanasikia maneno yetu tunapozungumza humu Bungeni, kwa mfano juzi na jana endapo tutaendelea kwa tabia

na utaratibu huu, alisema siku moja Mzee Malecela ipo siku tutabeba viti humu tutatupiana. Hatutaki chini ya uongozi wako, tufike huko. Ni vizuri zaidi tukafuata Kanuni zetu zinazotuongoza humu ndani lakini tuheshimu Kiti kwa sababu imejitokeza tabia ambayo si nzuri hata kidogo ya kubishana kati ya Mbunge na Kiti, huu si utaratibu wa Bunge letu. Tabia hii inatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, hili ulione kwa sababu wewe tunakuamini sana kama kiongozi wetu, hili ulikemee. Kama ipo hoja ya msingi, basi iletwe kwa utaratibu lakini tukianza kubishana Kiti na Mbunge, haionyeshi tabia nzuri kwa wale wanaotusikiliza. Nakuomba sana hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Wizara husika. Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara hii, naomba ninukuu maneno aliyosema ilikuwa tarehe 7/3/2006. Alisema hivi:-

“Civil service, ndiyo injini ya chombo kinachoitwa Serikali. Utendaji wake ukiwa mzuri, gari hilo litatembea vizuri. Utendaji wake kama sio mzuri gari letu litakuwa halitembei vizuri. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba, gari letu hili linatembea vizuri. Taaluma za watumishi wetu ili kuboresha uwezo wa utendaji kazi, nidhamu yao, maslahi yao, haya ni mambo ambayo hatuna budi kuyafanya”.

Hapa Mheshimiwa Rais alikuwa na maana ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo ambalo sisi tunalo na Waziri Mkuu alipokuwa anahitimisha hotuba yake, aliwaomba Watendaji Wakuu sasa wawe na maamuzi ya kusaidia nchi na wawe na uharaka wa kuamua kuliko kukuaa na maelekezo wanayafungia kwenye kabati. Lakini bado ile tabia ya njoo kesho, njoo kesho, ipo maofisini. Naomba, ili twende kwa *speed* ambayo wewe unaenda nayo, basi utaratibu huo ufuatwe. Nchi yetu, ni nchi ya wakulima na wafanyakazi. Lakini bado iko haja ya kuangalia na kuboresha maslahi ya wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwazungumzie Waganga na Walimu. Najua Walimu wana chombo chao lakini Waganga, hawana chombo cha kuwasemea. Hapa naomba kuweka ombi tu, katika Wilaya ya Kwimba, wapo Walimu wa zamani wanadai malimbikizo yao pamoja na kwa jirani yangu, Jimbo la Mvomero, wanadai malimbikizo yao. Lakini wapo walimu wapya ambao wamesharipoti Wilaya ya Kwimba, kwa ajili ya kufundisha shule zetu za msingi, bado hawajalipwa pesa zao za kujikimu. Naomba sana, kwa sababu hii ni haki yao, walipwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia upande wa Mahakimu, mfano yupo Hakimu mmoja kwenye Kituo cha Nyambiti, anatembea kutoka Nyambiti kwenda Ngula, hana gari wala pikipiki, anatumia baiskeli karibu km 20 na ni mwanamke, akitoka Ngula anarudi Nyambiti km 20, anatoka Nyambiti anakwenda Nyamikoma km 22, hivi haki itatendeka namna gani? Naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa Mahakimu wa

Mahakama za Mwanzo, usafiri ili waweze kutenda kazi zao vizuri. Hili naliomba sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Ikulu. Ikulu ni sura ya nchi, panatakiwa pawe safi. Namwomba sana Mama yangu, Mheshimiwa Sophia Simba, ile sura ya Ikulu, usafi umepungua. Ukipita pale barabarani, utakuta ule ukuta umeshaanza kuchakaa, sura ya Ikulu haionyeshi vizuri. Lakini mle ndani, kulikuwa na wanyama na *Zoo* leo sijui iko wapi?

Mheshimiwa Spika, wageni wanapokuja kutoka nje, kwa sababu wanyama tunao, kwa mfano tausi na wanyama wengine kwa nini wasianze kuwaangalia wakiwa kwenye *Zoo* yetu ya Ikulu? Walikuwepo, wamepelekwa wapi? Naomba sana hili lakini zile bustani nazo ziimarishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU. Nawapongeza kwa upande wangu, wanafanya kazi nzuri hasa kwenye Wilaya yangu ya Kwimba wanafanya kazi nzuri. Naomba mishahara yao iboreshwe na wapewe usafiri wa kutosha kwa sababu wana gari mmoja na hawawezi kutoka Mbudu kwenda Mwamashimba, kwenda Kadashi, Malidisu kwa hiyo gari moja. Ikiwezekana na kwa sababu hali ya mafuta sasa hivi ni ngumu, naomba wapewe angalau pikipiki. Kwa kutokufanya hivyo, tutakuwa hatuwatendei haki kwa sababu inawezekana wakarubuniwa na kuchukua rushwa. Kwa hiyo, tukifanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Mipango. Nashukuru Tume hii ipo chini ya Mheshimiwa Rais kwa sababu, Tume hii kama itaanza kufanya kazi mapema, najua uwezo wa Balozi Mtalemwa, naomba wachaguliwe wale wenye kujua na wenye taaluma zao kwa sababu hiki ndicho kichwa cha treni, hii ndiyo *think tank* ya nchi. Kama itachaguliwa kwa kufuata taaluma, nina uhakika watafanya kazi yao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, tarehe 2/6/2008 - 6/6/2008, ulifanyika mkutano mkubwa Arusha. Mkutano huo ulikuwa kwa ajili ya kutangaza utalii wetu lakini pamoja na mambo ya miundombinu. Lakini kuna mtu mmoja anaitwa Andrew Young, alimsifia sana Baba wa Taifa pamoja na Karl Master, walimsifia sana. Sasa hii *Leon Sullivan Foundation* inawezekana lakini tuulizane, hivi *Mwalimu Julius Nyerere Foundation*, iko wapi? Kama kule kuna Andrew Young na sisi huku kuna wakina Joseph Butiku, Salim Ahmed Salim, nina hakika, hii *foundation* ya Mwalimu Nyerere na yenyewe ikisimamiwa vizuri, iwekwe kwenye Kitengo cha Serikali, itafanya kazi yake vizuri ya kumtangaza muasisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nikushukuru sana lakini niombe yale ambayo nimeyasema hasa ya upande wa watumishi wa Jimbo langu la Sumve na Wilaya ya Kwimba, yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii, ili nami nichangie angalau kidogo katika Wizara hii ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru na nimpongeze, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa kuongoza Wizara hii na kwa juhudi yake kubwa anayoifanya ili kuweza kutimiza malengo ya Wizara hii.

Vilevile naomba nimwambie Mheshimiwa Hawa Ghasia, Ndugu yangu, ana kazi ngumu sana lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, *Inshallah*, atamsaidia.

Mheshimiwa Spika, kazi moja ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ni kuimarisha utawala bora na katika kuimarisha utawala bora, kuna nyanja nyingi sana na utawala bora unakwenda katika kila sekta ili kuleta maendeleo ya nchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, siku zote duniani, ni siku tatu. Kuna jana, ambayo huwa imepita na mara nyingine huwa haina umuhimu sana kwetu inabakia kuwa ni historia, kuna kesho ambayo huna hakika ya kuifika na kuna leo ambayo tunapaswa tuitumie vizuri sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa uongozi wake katika Wizara hii, aitumie sana hii leo ili kuhakikisha utawala bora unapatikana katika Tanzania hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana, sisi viongozi, ndio tunapaswa kuonyesha mfano wa jambo lolote ambalo tunalitangaza. Siku zote huwa tunatangaza sana utawala bora katika nchi yetu na katika baadhi ya mambo, tunajitahidi lakini mengi sana hubaki vitabuni. Ili tuweze kwenda vizuri, sisi viongozi ambao tumo ndani ya Bunge lako Tukufu, basi utawala bora unapaswa uanzie hapa.

Mheshimiwa Spika, katika nyanja ya utawala bora, kwanza kuna suala la ukweli na uwazi, hapo ndipo utawala bora utapopatikana. Kama viongozi hatukuwa wakweli na hatutaki kuwa wazi, basi utawala bora haupo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, siku zote, Serikali inayokuwepo madarakani, Chama cha Upinzani, huwa ndiyo kioo chake kwa sababu mcheza ngoma siku zote, hajui kama anacheza vizuri au la lakini mtazamaji ndiye anayeamua kwamba mchezaji anacheza vizuri au anacheza vibaya. Mtazamaji anapokuangalia, akakwambia unacheza vibaya, rekebisha *step* zako, unapaswa ujiangalie na urekebishe *step* zako ili uweze kwenda na mdundo wa ngoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumo humu kwa ajili ya kuwawakilisha Watanzania, tumo humu kwa ajili ya kuwasemea yale yanayowakera, tumo humu ndani kwa ajili ya kuwasemea yale mambo ambayo wanahisi hayatowaletea maendeleo na tuyarekebishe ili tuweze kupata maendeleo. Kwa nini tunapofika mahali tukazungumza kuhusu mambo yaliyoko nje na ndani ya jamii, yanayotendeka na ambayo hayaleti utawala bora, tukakamatana kwenye Kanuni haraka haraka, kwa kusema futa usemi, uongo na mambo kama hayo? Tunapaswa tugeuke nyuma, tuangalie je, haya yanayozungumzwa na

wenzetu, ni ya kweli au uongo? Kama ni ya uongo, turudi tuchukue hatua! Lakini kama ni ya kweli, basi tujisahihishe kwa maslahi ya wananchi wote kwa ujumla. Tanzania ni nchi yetu, ni ya Watanzania, tunapaswa kuiongoza vizuri, sisi ndiyo masuli, kwa hiyo, hii leo lazima tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, hivi nani ambaye hajui kwamba Zanzibar kuna matatizo? Hii ni Jamhuri ya Muungano, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, sisi Wazanzibar, Baraza la Wawakilishi ndipo pa kupeleka kilio chetu kwanza kwa sababu yule ndiye mama lakini tukishindwa kama mama hakuchukua hatua tunapaswa kuja kwenye Bunge lako la Jamhuri ya Muungano kulia kwa baba, atuangelie tuna tatizo gani. Ni nani ambaye haelewi kwamba chaguzi zote zinazofanyika Zanzibar, si huru na si haki na mauaji hutokea jamani yanayosababishwa na hawa hawa Askari tunaowasema? Serikali hii huchukua hatua za kuwapa uhamisho kwa ajili ya kuwaficha baada ya kufanya vile vitendo, je, huo ndio utawala bora?

Mheshimiwa Spika, tunalia hapa kwa sababu hili ndilo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar ni sehemu ya Muungano na mpasuko wa Zanzibar unapaswa ushughulikiwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tuweze kwenda vizuri, tuweze kupeleka nchi yetu pazuri, tukiacha hali kama ilivyo sasa, tutazidi kupeleka pabaya zaidi. Tunapozungumza humu msitulaumu, msituelewe vibaya, nia ni kujenga!

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwenye suala la huu huu utawala bora. Kukiwa na utawala bora, maisha ya Watanzania yatakuwa bora kwa sababu yataboreka katika kila sekta. Wafanyakazi wa Taifa letu hili la Tanzania ni watu duni, maskini, wanyonge ambao hawamiliki hata mlo wa siku. Mishahara aliyosema Mheshimiwa Waziri utapandishwa mpaka Sh.100,000/-, tunawachezea Watanzania na tunawadanganya. Tunapaswa viongozi tutembeo twende tukaone maisha ya wananchi wetu huko vijijini, tuone wanaishije jamani!

Mheshimiwa Spika, mwenye watoto wawili, hawezi kumudu maisha yake hata kwa mlo wa siku kwa fedha hii. Tuachie mbali mfanyakazi, huyo mtu wa chini ambaye hana hata hiyo kazi ya Serikali, lakini tukimboresha huyu mfanyakazi basi huyu mlalahoi naye ataboreka kutokana na shughuli zake ndogo ndogo anazozifanya. Kwa sababu mimi kama naweza kumudu maisha yangu, naweza kwenda mahali kununua kitu changu kwa bei ile ambayo nimeiweka basi na yeye maisha yake yanasogea. Lakini kama mimi mwenyewe mfanyakazi wa Serikali, siwezi kwenda kununua nakwenda kumkopa, ukishamkopa umemuumiza, hurudi tena, unamkimbia.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba wananchi wote wanaoishi Tanzania, wafanyakazi wa Serikali na wasiokuwa wafanyakazi wa Serikali, sote ni wezi. Tunaishi kwa rushwa, tunaishi kwa uongo, tunaishi kwa udanganyifu kwa sababu maisha tuliyonayo, mishahara haikidhi haja kutokana na gharama kubwa za bidhaa na jinsi maisha yalivyopanda.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie tena vizuri sana mfanyakazi, tutawezaje kumwezesha ili maisha yake yaweze kuboreka na yule Mtanzania aliyeko kijijini naye aweze kuboreshewa maisha yake kutokana na mahitaji yake mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii tunayokwenda nayo...

SPIKA: Mheshimiwa Riziki, ndiyo hayo hayo huwa mnayaomba sasa. Nilidhani kuna Mheshimiwa Mbunge, atasimama hapa kwa sababu ukisema sote nchi nzima, unautangazia umma wa Watanzania hakuna mwaminifu hata mmoja, Watendaji, Wabunge, ni kweli? Haiwezi kuwa hivyo!

Waheshimiwa Wabunge, nadhani ni vizuri mnapochangia ili tusiingie katika malumbano, ulenge kitu ambacho Mtanzania mwenye akili yake ya kawaida, ataona huyu anasema kweli lakini ukisema kila mtu, unaanzia Rais mpaka Mtendaji wa Kijiji, kwa kweli, inakuwa ni tofauti.

Mheshimiwa Mbunge, nakuomba uondoe hayo maneno kwa sababu kwa usemi huo, hata Spika umemtukana. (*Makofi*)

MHE. RIZIKI OMAR. JUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunielekeza, naomba niseme lengo langu halikuwa hilo na nafuta usemi huo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amefuta. Endelea Mheshimiwa Riziki.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Nije kwenye suala la wastaafu. Wastaafu wanapofikia wakati wa kustaafu hali zao ni mbaya sana na ni mbaya kiasi cha kwamba hawawezi kuendelea na maisha kutokana na ugumu wa maisha unavyowaelelea. Maisha ya Mtanzania ambaye amestaafu, ukimkuta, wewe mwenyewe, utamwonea huruma. Kwanza, viinua mgongo vyao vinachelewa kupatikana, anaanza kusunoneka kuanzia siku ile anayostaafu mpaka anapopata kiinua mgongo chake bado hairidhishi kabisa. Kuna wastaafu ambao wanalipwa Sh.15,000/- ambazo haziwezi kukidhi mahitaji ya maisha. Hilo limesemwa na wengi na mimi nasaidia kulichangia.

Mheshimiwa Spika, nielekeze nguvu kidogo kwenye suala la haki za binadamu. Utawala bora ni pamoja na kuheshimu haki za binadamu. Mheshimiwa Waziri, leo alisema haki za binadamu katika nchi yetu zinalindwa, ni kweli lakini kuna baadhi ya mambo namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa karibu sana na hii Tume ambayo ipo ya Haki za Binadamu basi ifuatilie kwa karibu sana uvunjwa wa haki za binadamu unaotokea katika baadhi ya maeneo. Sisemi kama nchi yetu hailindi haki za binadamu lakini kuna baadhi ya maeneo tunakiuka na tunapokiuka basi yale matatizo yafuatiliwe haraka iwezekanavyo ili isitafsiriwe kwamba Tanzania ina matatizo. Kwa sababu kila mmoja akitimiza wajibu wake ipasavyo na kila mmoja akashughulikia sekta waliopo kwa

uadilifu kama Menejimenti ya utumishi inavyosema, basi tutafikia huko, tutaijenga Tanzania yetu kwa pamoja na tutakwenda vizuri na nchi itafika mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, aiangalie sana leo kwa faida ya Watanzania na faida yake mwenyewe kesho tutaulizwa na *Subuhanah Watallah*, ahsante. (*Makofi*)

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa, hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii, ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, dada yangu wa hiari ambaye huwa hatutaniani sana lakini napenda Mwenyezi Mungu azidi kumwongezea sifa kama za hiari ya utamu wa mua na hasa kifundo chake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, kwa kazi nzito aliyonayo ya kubeba mema na mabaya. Hata sisi Wabunge tunapohoji masuala ya matumizi ya fedha, huwa tunapata uadui na chuki. Kwa hiyo nampongeza kwa moyo wake wa subira. Mwenyezi Mungu ujasiri amzidishie ili aweze kukabiliana na mitihani mbalimbali katika majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajielekeza kutoa mchango wangu katika hoja iliyombele yetu, napenda kuipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kufuta Mkataba mtambuka wa kutoka Richmond hadi Dowans. Napoingeza sana kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge imara, huzaa Serikali imara. Kwa hiyo, napenda kulipongeza Bunge lako, kwa kazi nzuri lililofanya la kuzaa Serikali imara ambayo imechukua majukumu hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa imani ya Chama cha Mapinduzi, ni kazi nzuri inayofanywa na Bunge nje ya Chama, ndani ya umma. Kwa hiyo, napongeza sana kazi nzuri ya Bunge, tuzidishie CCM katika kazi nzuri ya kuimarisha umoja na mshikamano kwa maslahi ya ustaarabu na maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kupambambanua kwamba, ufisadi wa uhalifu kwa viburi vya madaraka, ni adui mkubwa sana katika ustawi na maendeleo ya uongozi wa nchi yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala la Menejimenti ya Utumishi wa Umma, liko katika hazina ya matendo pamoja na kauli zinazotolewa na viongozi mbalimbali. Naomba tujiulize suala moja, hivi ni kwa nini pana msururu mkubwa sana pale Ikulu wa watu wanaotaka kumwona Mheshimiwa Rais? Kwa nini pana msururu kwa Waziri Mkuu wakitaka kumwona Waziri Mkuu? Kwa nini pana msururu Wabunge turejeapo

Majimboni, wananchi wanataka kutuona? Kwa nini kuna msururu wa kutaka kumwona Jaji Mkuu? Hiyo ni kutokana na sababu ya udhaifu ndani ya maeneo machache ya watu wachache wanaosababisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma kulaumiwa na Utawala Bora usionekane.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kubainisha ya kwamba adui mkubwa anayetafuna sura ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ni kauli zinazotolewa na Watumishi pamoja na viongozi mbalimbali. Mathalani uhalifu wa viburi wa madaraka wa ngazi mbalimbali za viongozi, huwa wanatafuna sana sura ya kozi zinazotolewa na Menejimenti ya Utumishi mfano Ngurudoto na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Waziri anayehusika, ahakikishe kwamba sura ya Utawala Bora, inazaliwa na sura ya Menejimenti nzuri ya Utumishi, ndiyo kichocheo kwa ustawi na maendeleo ya uchumi na ndiyo haki ya uhuru, ni maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, fikra zilizopauka, huzaa maamuzi chakavu. Kwa hiyo, naomba Waziri anayesimamia masuala ya Menejiment ya Utumishi, ahakikishe kwamba anajitahidi kuwa na uvumbuzi na ugunduzi wa kuondoa yale yote ambayo tuliyarithi katika zama za ukoloni, kwa sababu kila zama kuna mambo yake na twende na kasi ya Ari Mpya na *Standard* ya Bunge letu.

SPIKA: Hebu rudia ile ya fikra, nzuri sana ile, ni fikra zipi? (*Kicheko*)

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nitaomba ulinde muda wangu, fikra zilizopauka, huzaa fikra chakavu na fikra chakavu huzaa mawazo mgando na mawazo mgando hayaendani na Ari Mpya na Kasi Mpya ya Bunge lako. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia juu ya mchwa unaoitwa ufisadi wa uhalifu wa kutumia viburi vya madaraka ya viongozi mbalimbali. Naomba kutanabaisha ya kwamba, kauli na matendo ya Mawaziri, Wakuu wa Mkoa, Ma-DC, DED na viongozi wote, ni vyombo vya kusaidia maendeleo ya wananchi. Hivyo, ninaomba viongozi waangalie kauli wanazotoa wakitambua kwamba Bunge na Serikali ni wamoja katika fungamano la maslahi ya ustawi na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza masikitiko yangu makubwa, yaliyotokea mnamo tarehe 25 Juni, pale ambapo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dokta Mathayo, alipofika Shinyanga akiwa na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Mjengwa, walipotoa kauli ambazo zilikuwa katika vyombo vya habari ambazo zilisema kwamba Mbunge adaiwa kuzuia ziara ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha hayo, pia nina mkanda ambao unanukuu za maneno ambayo naomba kusoma hapo kwa ruhusa yako. Yanasema:-

"Mheshimiwa Naibu Waziri wa Chakula na Ushirika, Mathayo David, amedai kuwa, Mbunge wa Maswa, Mheshimiwa John Shibuda, kamzuia kufanya ziara katika Jimbo hilo Mkoani hapa. Akitoa madai hayo jana katika kikao cha pamoja cha Viongozi

na Watendaji na Waandishi wa Habari Mkoani hapa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, alisema amesikitishwa na kitendo cha Mbunge huyo kumzuia kutembelea Jimboni mwake kwa madai kwamba yeye hayupo Jimboni jambo ambalo alidai kuwa ni kuwanyima haki wapiga kura wa Maswa, sijui aliwanyima kura gani huyu Mheshimiwa?

Alisema yeye akiwa kiongozi wa Serikali, anapokwenda katika Jimbo la Mbunge yeyote, huwa hana nia ya kumharibia bali ni kupeleka salamu za Mbunge katika eneo husika iwapo kama yeye Mbunge hayupo na kufanya kazi iliyompeleka na si vinginevyo. Hakuna Waziri anayekwenda Jimboni kwa Mbunge kwa lengo la kumharibia huwa tunapeleka salamu za Mbunge, ni lazima muwaeleze ukweli wananchi wa Jimbo la Maswa kuwa Mbunge amemkataza Waziri kutembelea miradi iliyopo Jimboni mwake, alisema Naibu Waziri huyo. Alisema hakuna lugha nyepesi wala kubembeleza kuwaeleza wananchi wa Maswa juu ya Mbunge kumkataza Waziri aliyekuwa amepangiwa Wilayani humo kwani Serikali ni msumeno, unakata kote kote.

Awali Kaimu wa Mkoa Kanali Edmund Mjengwa, alisema amepokea taarifa kuwa Mbunge wa Maswa amekataa Naibu Waziri kwenda Jimboni mwake na kusema hilo ni tatizo la Maswa na siyo la Mkoa.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri, Ndugu Songe alisema kwamba amepokea simu ya kuzuia ziara ya Mheshimiwa Waziri”

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa wamezusha uwongo katika magazeti haya na habari hizi zilitangazwa pia katika radio. Ninaomba kusema kwamba, nilipokea taarifa ya ugeni wa Mheshimiwa Waziri wa Chakula na Kilimo, siku ya tarehe 24, saa 11.45, nikiambiwa tarehe 25, saa tano, niwe Maswa, hata kama ningetumia ungo, nisingeweza kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wasira, nilipomwuliza kuhusu ziara hiyo alisema kwamba yeye haendi bali amemwomba Naibu Waziri wake aende. Nilizungumza na Profesa Mwandosya iwapo anaelewa ya kwamba ziara hii ni ya kwenda kuzindua bwawa la maji ambalo mimi naliomba bilioni 1.2 ili tuweze kukamilisha mradi huu. Nasikitika Mheshimiwa Waziri wa sekta alikuwa hajui kama kuna kauli ya kutoka Wizarani au kwa Rais ya kwamba bwawa hilo likazinduliwe, Waziri wa sekta alikuwa hajui. Nilimtuma Injiniwa kwa Katibu Mkuu akasema hajui, nikamwuliza Injiniwa wa mradi na yeye akasema analazimishwa.

Mheshimiwa Spika, je, hii ndiyo Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa Viongozi, yaani Mawaziri dhidi ya Wabunge? Je, hii ndiyo Menejimenti ya Utawala Bora kutoka kwa Viongozi wa Serikali dhidi ya Wabunge? Je, kama ningemtendea Dokta Mathayo haya katika Jimbo lake, angejisikia vipi? Je, matendo kama haya ya udhalimu, kama yangetokea katika Jimbo la Mtwara Vijijini, Mheshimiwa Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, asingeharakisha kuandaa Kanuni ya kuwadhiti watu wanaoingia katika Majimbo na kutoa kauli kwa utashi wa ufasadi wa viburi vya madaraka?

Mheshimiwa Spika, naomba sana habari hii ichukuliwe uzito, Naibu Waziri huyu, katumia kauli ambazo kwa kweli haziendani na maadili fungamano kwa umoja wa mihimili mitatu Bunge, Serikali pamoja na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ikiwa mtu akidharau Mahakama (*Contempt of Court*), hupewa adhabu, je, mtu akimdharau Mkuu wa Wilaya huadhibiwaje? Kwa nini sisi Wabunge ambao tunafanya kazi za Bunge pasiwe na sheria ya kuadabisha watu wanaowadharau Wabunge wenzao? Hili Bunge ndiyo linalopitisha Sheria, ninaomba Wabunge tulindwe, kuna Idara ya Sheria, naomba ipitie haki na *immunity* za Wabunge, utagundua kwamba hatuna pahala pa kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, naomba sana vyombo vya habari vilivyotoa habari hizi, kwa kweli vimeleta mfarakano kati ya wananchi wa Jimbo la Maswa na Mbunge wao, mdai chake hulaumiwa. Ninapodai haki yangu stahiki kama Mbunge wa Jimbo la Maswa dhidi ya udhalimu na dhahama aliyokamilisha Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba Spika uchukue hatua ya kunilinda na kunitetea mimi Mbunge wako. Kila muungwana atavuka aibu zake kwa matendo yake. Kwa hiyo, ninaomba tusingiliane katika Majimbo kwa tabia za uzushi.

Mheshimiwa Spika, natambua Mwanasiasa, hawezi kukosa adui, naomba tuzingatie maadili na Idara ya Menejimenti ya Watumishi pamoja na Utawala Bora, mtunge Kanuni ambazo zitapambanua masuala ya kuheshimiana kwa sababu Mbunge hata katika ziara za viongozi huwa anaonekana mtu dhalimu lakini wakati wa vikao vya Bunge kila mmoja humnyenyekea Mbunge ili mambo yake yapite.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika, tutanabaishe udhalimu na uungwana wa matendo na kauli. Naomba kusema kwamba iwapo ziara hiyo ingeenda kule Maswa maana yake pesa nilizokuwa nimeomba tusingeweza kupata machujio, tusingeweza kupata maji safi Maswa, kwa hiyo wananchi wa Maswa wangeendelea kuwa na uhaba wa maji.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kusema kwamba Bajeti ya Taifa iendelee kunifikiria kunipatia bilioni 1.2, kwa taarifa nataka kuwasaidia Maswa na vilevile kwa elimu kwa Wakandarasi wa fitna ambao ndiyo Menejimenti ya Uzushi na ndiyo hasa miradi ya porojo ya kuibua kashfa dhidi ya Wabunge. Napenda kuwaambia kwamba kura za wananchi wa Maswa siyo matunda mwitu ambayo kila mmoja anaweza kuyavamia, kura za wananchi wa Maswa zina wenyewe na ndiyo wakazi wa Maswa.

Mheshimiwa Spika, wenye fitna nawaarifu ya kwamba dua la kuku haliwezi kumhasi mwewe, Maswa ni njema, karibuni wote na ninasema mwaka 2010, Maswa haitakuwa dangulo la Wanasiasa. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishieni CCM, ni imara na Mbunge, ni imara. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wanandoa wanapoaswa huwa wanaambiwa kwamba peaneni matumaini ili mjengane. Sasa namwomba Mheshimiwa Hawa Ghasia na ninamwomba Mheshimiwa Sophia Simba, waendeleo kutuhamasisha, tupeane matumaini ili tujengane

katika kudumisha umoja na mshikamano kati ya viongozi wa Serikali na Bunge. Ili tuendeleze umoja huo, basi pana haja ya kupeana mahaba ya utu na ubinadamu dhidi ya uhasama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Leo Waheshimiwa wengi hamfuati Kanuni za Bunge, wewe unawaomba mahaba Mawaziri hawa? Basi kwa kuwa umeshaketi nakusamehe. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru.

MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU: Mheshimiwa Spika,

SPIKA: Naomba utulivu ili tumsikie mwenzetu

MHE. KINGUNGE NGOMBALE MWIRU: Mheshimiwa Spika, ninapenda nikushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini kukushukuru vilevile kwa kutuongoza vizuri hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, amewasilisha vizuri sana hoja yake na kwa ufasaha mkubwa. *(Makofi)*

Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Ninapenda niwapongeze pia Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu wa Ikulu, Katibu Mkuu wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na viongozi wengine wote, watendaji katika Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wanatufanyia kazi nzuri sana na ndiyo maana Rais wetu anamudu kufanya kazi za nchi yetu kwa wepesi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie nafasi hii nianze kwa kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kuiongoza nchi yetu na kuijengea nchi yetu heshima kubwa nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kikwete ameimarisha amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Mtakumbuka hali iliyojitokeza mara baada ya kuapishwa kwake lakini hatua za haraka zilichukuliwa za kuhakikisha kwamba nchi inadhibiti ujambazi, inakabili hali ya ukame, inakabili hali ya mafuriko na wananchi wote wakapata faraja, wakatulia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kifupi, ametusaidia sana. Ameendeleza kazi aliyoirithi, mfano ni elimu ya sekondari, mambo ambayo yamefanyika katika Tanzania katika kipindi hiki kifupi, ni mambo ya kuigwa. Mimi naita ni mapinduzi, sisi

tulikuwa tunashika mkia katika suala la elimu, kuanzia elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upande wa shule za msingi, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa aliweka msingi mzuri, kwa kupitia *MMEM* iliwezekana kufika mahala ambapo zaidi ya asilimia 90 ya watoto wetu wenye umri wa kwenda shule za msingi walikuwa wanahudhuria shule. Mheshimiwa Rais Kikwete, akashika hapo na sasa shule za msingi zinakaribia asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba tumepiga hatua kubwa sana upande wa elimu ya sekondari. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, tuliweka lengo kwamba ifikapo mwaka 2010, watoto wanaomaliza darasa la saba, angalau asilimia 50 waweze kuingia *form one*. Lengo hilo tumelifikia kabla ya mwaka jana na sasa zaidi ya asilimia 70 ya watoto wetu wanaomaliza darasa la saba, wanaingia sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hakufanya kazi nzuri hapa ndani tu, pia amefanya kazi nje ya nchi, ametujengea jina zuri la Tanzania katika Afrika, amepata heshima na ametupa heshima na sasa yeye ni Mwenyekiti wa AU. Kutokana na kazi yake, ameweza kuitisha mikutano mikubwa hapa Tanzania. Kutokana na kazi yake, wawekezaji wanaongezeka Tanzania, kutokana na kazi yake Utalii unaongezeka sana Tanzania na kutokana na kazi yake heshima ya Tanzania inazidi kung'ara. Ninapenda kumpongeza sana na kumwomba aendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunayo matatizo. Baadhi ya Watanzania tena kwa kawaida, ni wachache sana, hawaoni kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne. Nilipokuwa huko nje nilisoma misahafu, nilisoma *comparative religion* na wanasema, Nabii Issa yaani Yesu Kristo alisema:-

“Kuna watu wana macho lakini hawaoni, wana masikio lakini hawasikii, wana pua lakini hawanusi”.

Sasa nasema, wapo wachache na kwa sababu hawaoni, kwamba wanajengewa heshima, kwamba nchi inakwenda mbele, kazi yao ni kulalamika na kukashfu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tufanye kazi ya kuwaelimisha tu, wala tusibabaike, tuwaelimishe watakuja kuona, hasa wataona vizuri mwaka 2010, kwa sababu wananchi wana macho na wanaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nia yangu ni kuzungumzia jambo moja tu baada ya hilo nalo ni suala la Tume ya Mipango. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais na Ofisi yake, kuamua kwamba tuwe na Tume ya Mipango. Uamuzi huu ni wa busara sana. Siku za nyuma, tulikuwa na mipango. Mara baada ya kupata uhuru, tulianzisha utaratibu wa mipango ya miaka mitano mitano na utaratibu wa mipango ni muhimu sana kwa bahati mbaya hapa katikati tukaupuza. Ni muhimu kwa sababu nyingi. Wengi hapa ni wasomi, wanaelewa, nchi zetu zinahitaji mipango kwa sababu rasilimali ni chache, kama huwezi kupanga hutaweza kuzitumia kwa busara (*rationally*).

Mheshimiwa Spika, mahitaji ni mengi nayo vile vile kama unataka kwenda mbele, inakulazimisha upange. Nchi ni kubwa na ina mazingira tofauti. Wengine wapo pembezoni, wengine wapo katikati, wengine wana ukame na wengine wana mvua nyingi, lazima upange vinginevyo wengine wataachwa nyuma na wengine watakwenda mbele peke yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi ni lazima iendelee mbele kama nchi. Sisi dira yetu ya maendeleo tumeweka 2025. Tunataka ikifika mwaka 2025 tufikie kiwango cha nchi yenye maendeleo ya kati. Mkishafanya hivyo na kama hamna mipango na hakuna mahala pa kati ambapo panaamua twende vipi, mtaenda kwa kubahatisha na hamtafika. Kwa hiyo uamuzi huu umekuja kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba CCM, katika Ilani tumesema na tumeainisha kuwa jukumu kuu la msingi ambalo ni kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na pili tuwe na sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa, yaani *modernisation*, inataka mpange mnakwenda vipi katika kubadilisha kilimo ili muondokane na kilimo kinachotegemea jembe la mkono na muanze *mechanisation* hatua kwa hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchumi wa kisasa ni wa viwanda, nao ni lazima mkapange. Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Rais ametimiza wajibu wake, ameeleza vizuri kwamba ni lazima kuwepo na *think tank* na watu tunao wenye uzoefu mbalimbali na Bunge lina watu wenye uzoefu mkubwa. Matumaini yangu, ni kwamba tutapata nafasi ya kulizungumza suala hili la Tume juu ya maudhui yake na muundo wake ili tuweze kuelekea mwaka 2025 kwa uhakika hatua kwa hatua. Mheshimiwa Rais amekwishaonyesha njia, sasa mpira upo kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja hii mia kwa mia na kwa kuwa Mawaziri hawa wa Ofisi ya Rais wanafanya kazi nzuri na watendaji wote wa Ikulu na majukumu ya Ikulu yanatekelezwa vizuri na nchi inakwenda vizuri, naomba Wabunge wenzangu tupitishie makisio haya sote kwa pamoja kwa kauli moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu Ofisi za Utumishi wa Umma kujaa urasimu hata ukienda kupeleka barua ya kuomba jambo muhimu, hujibiwi na hata ukijibiwa inachukuwa muda mrefu. Bado katika ofisi hizo, rushwa inalalamikiwa sana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuiomba Serikali, pamoja na bajeti finyu bado wachukue juhudi za makusudi, kuongeza mishahara kwa sababu mishahara wa shilingi laki moja ni mdogo sana, hasa ukizingatia maisha jinsi yalivyopanda, Watanzania wana familia kubwa na wanaishi nyumba za kupanga. Sasa ukimpa huo mishahara bado haukidhi mahitaji. Ndio maana watumishi wengi wanashawishika kupokea rushwa katika sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Spika, kima cha pensheni ni kidogo sana ukizingatia hali ya maisha ya sasa, naiomba Serikali iangalie sana kuwasaidia watumishi waliostaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU ni chombo ambacho tumepitisha sheria ya kuwapa meno, lakini inaonyesha chombo hiki bado hakiko huru kwani wanashughulikia rushwa ndogo ndogo tu, rushwa kubwa kubwa wanaziacha na kusababisha watu kuondoka na woga wa kuweza kuendelea na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora, bado Tanzania tuko nyuma maneno yamekuwa mengi kuliko vitendo. Tunaomba Serikali ichukue hatua ili mafisadi wasione mambo ni magumu wakaondoka nchini na lengo lisipatikane.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Viongozi na Watendaji wote waliosaidia kuandaa Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo kuhusu matumizi ya fedha za *TASAF* katika Halmashauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, nikiri kwamba Wilaya ya Muheza ilikuwepo katika Mpango wa *TASAF* Awamu ya Kwanza na sasa katika Awamu ya Pili, hivyo imejenga uzoefu mkubwa. Hata hivyo, wapo viongozi wanaochangia kuleta malalamiko miongoni mwa Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuhusu mambo kadhaa, hasa Mbunge anapokuwa katika Vikao vya Bunge wakati vikao vinavyohusu Miradi ya *TASAF* vinapofanyika!

Mambo yanayohitaji ufafanuzi: Uwiano wa mgao wa fedha kwa wilaya ni vyema vigezo vya mgao wa fedha za miradi vielezwe bayana ili Halmashauri zisipishane sana katika mgao wa fedha. Ni dhahiri Halmashauri zinazowasilisha miradi mingi zinapata fedha nyingi. Lakini je, Halmashauri zinazowasilisha miradi mingi zitapata fedha zote iwapo vigezo vyote vimetimizwa au zitapunguzwa kufuatana na viwango vya mgao kwa wilaya?

Viongozi wa Halmashauri wakati wa kujadili maombi ya miradi kutoka Kata, wamekuwa wakikataa na kupunguza miradi iliyoibuliwa na wananchi wa Kata moja hata kama Kata nyingine hazikuibua miradi. Kwa msingi huo, Kata zinazopunguziwa miradi yao hulalamika na Madiwani kutoelewana.

Kumekuwa na utendaji dhaifu kwa wawakilishi wa *TASAF* ndani ya Halmashauri kushindwa kutembelea na kuhamasisha uibuaji wa miradi katika Kata. Hali hii inafanya Kata nyingine licha ya kuwa na matatizo, kukosa fursa ya kuibua miradi na hivyo kukosa usaidizi wa Miradi ya Jamii na hata miradi mingine. Hali hii pia inachangia Halmashauri nyingine kufanikiwa kuwa na miradi mingi wakati mwingine kuwa na michache au kukosa miradi. Je, Wizara na Kitengo cha *TASAF* Taifa kitasaidia vipi kupunguza hali hii na migongano ya Madiwani?

Japokuwa Muheza haijakumbwa na tatizo la ramani za ujenzi wa madarasa na zahanati, lakini yapo malalamiko mengi kwamba, *TASAF* inazo ramani za madarasa ya shule za msingi, sekondari na hata zahanati. Ramani hizo ni tofauti na zile za Wizara ya Afya kwa Zahanati au Madarasa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hata Shule za Sekondari. Kibaya zaidi, ramani za *TASAF* zinakuwa ghali zaidi na hivyo kufanya matumizi ya fedha za Mfuko huo kuwa kubwa. Wizara inaeleza nini umma kuhusu ramani hizo?

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa mishahara ya watumishi hasa walimu; mara kadhaa Halmashauri, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, imelalamika kwamba mishahara ya watumishi haipelekwi Halmashauri kwa muda mrefu, kutokana na Hazina kutopata taarifa za ajira zao kutoka Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hali hii inafanya Halmashauri kulipa mishahara hiyo kutoka katika mafungu ya maendeleo. Je, Wizara inafahamu hali hii na kama ndio inachukua hatua gani ili usimamizi wa ajira na ulipaji mishahara uende sambamba?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wapiga Kura wangu wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa kuniamini na kuendelea kuniunga mkono nami nawaahidi nitakuwa pamoja nao katika kazi ya kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, pamoja na Maofisa wote walioshirikiana na Mawaziri wetu na kufanikisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha wafanyakazi kuongeza kima cha chini cha mishahara na kufikia shilingi laki moja. Matumaini yangu

ni kuwa huu ni mwanzo tu na naamini kila baada ya muda zoezi hili litaendelea, kwa sababu hakuna asiyefahamu kama kima hiki ni kidogo kulingana na hali mbaya ya maisha na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, ningeisihi Serikali inapoamua kupandisha mshahara, suala hili liwe siri kwa sababu wafanyabiashara wetu wanaposikia tu Serikali imepandisha mshahara, kabla haujatoka wanapandisha bei bidhaa zao wakati nchi yetu ni ya wafanyakazi na wakulima na asilimia ndogo sana wafanyakazi kwa hiyo walio wengi wanaumia zaidi.

Mheshimiwa Spika, wastaafu ni hazina kubwa ya Taifa na Serikali haina budi kuwaenzi watu hawa kwa kuwapa mafao mazuri ili wajione kuwa Serikali yao inawajali. Ni hatari kubwa kama Serikali itawapa kisogo, kwa sababu wastaafu wetu wanatoka sehemu nyingi ikiwa ni pamoja na majeshi, polisi na vikosi vingine vya ulinzi na sehemu nyingine nyeti za nchi yetu. Nasisitiza kuwaenzi wastaafu kama vile tunavyotunza nyaraka zetu na baadaye kuzitafuta kwa uhakika wa kupata jambo sahihi.

MHE. SABELINA S. MWAJAGE: Mheshimiwa Spika, nitapenda kukufahamisha mambo machache kwenye Wizara hii yanayonisumbua kwenye roho yangu. Kwa mfano, ukaguzi wa mali zetu sisi Wabunge. Mimi nilichukia sana kutokana na watu waliokwenda nyumbani kwangu nikiwa sipo. Nilifuatilia ni nani aliyeongozana nao, nilifika kwa Mkuu wa Mkoa ili nijue ni nani maana alimkuta mtoto wangu na kuanza kumhoji, sasa nasema hivi mtoto anajua je mali zangu. Walimuuliza mambo mengi mpaka wakadiriki kumpigia simu baba akawaeleza msubirini mwenyewe. Wakamwambia mtoto awapeleke kwenye shamba langu, wakamwambia aingie kwenye gari akawaonyeshe; je, huyo mtoto anajua mali zangu zote nilizoorodhesha kwenye Fomu Na. III?

Napenda nipate ufafanuzi, pamoja na kupeleka malalamiko yangu sikutendewa haki katika ukaguzi huo.

Je, ajira Mkoa wa Kagera zimepatikana ngapi, kila mara napiga kelele za ajira napenda kujua ni ngapi? Nitapenda kujua Ofisi ya Utumishi wa Umma Kagera, inafanyaje kazi; watumishi wengi wana malalamiko mengi kwetu Wabunge? Naomba maelezo Utawala Bora huwa uko wapi na wakati wa uchaguzi huwa inafanya kazi gain? Uadhimishaji Sherehe ya Utumishi wa Umma mbona unafanyika Dar es Salaam peke yake; naomba nipatiwe majibu kwa nini usifanyike Mkoani Kagera angalau mara moja, iwe chachu kwa watumishi kupunguza malalamiko ya kusema tulisahaulika?

Pesa za *TASAF* zinazokwenda kwenye mkoa zinapofuatiliwa na Wabunge zinakuwa na migogoro sana, wanaitisha vikao vya mitaa kuzipangia zifanye kazi gani. Nimeshuhudia mtaa wangu pesa hizo walizipangia barabara toka mwaka jana mpaka leo; si hivyo tu na sehemu mbalimbali kwenye Kata nyingine. Ofisi hii ina mafisadi na ipo tu kwa kazi hiyo. **TAKUKURU** wao wana matatizo, wanatoa namba zao za simu kumbe uwongo watu wanapiga hazipatikani; je, hao wanachunguzwa na nani? Nitakapojua mambo haya nitaridhika na moyo wangu wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, nimeamua kuchangia hoja hii kusesitiza kuwa, Sheria na Taratibu za Kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma, zinahitaji kuangaliwa upya kwa faida na maslahi ya nchi.

Mosi, viongozi hujaza Tamko la Mali na Madeni kila mwaka, zoezi ambalo sasa hivi limepoteza maana yake ya msingi ya udhibiti na kuwa *routine* au zoezi la kimazoea tu. Ni muhimu sheria (kanuni) ifanyiwe marekebisho ili tathmini ya kina ifanyiwe kwa vipindi maalum kutambua ongezeko la Mali na Madeni ya kiongozi na maelezo (*justification*) yake. Aidha, kama kuna upungufu wa mali na madeni ya kiongozi; sababu zieleweke na tathmini hiyo isiwe siri. Sheria itamke wazi kuwa, pale kiongozi yeyote anapomaliza kipindi chake cha uongozi; taarifa rasmi ya mali na madeni ya kiongozi itolewe ili ijulikane aliingiaje katika uongozi na ametoka au kumaliza muda wake akiwa katika hali gani.

Pili, ikiwa nia yetu ya kupambana na rushwa na ubadhirifu ni ya dhati, hakuna sababu yoyote kwa sheria kuweka urasimu na ukiritimba katika kupata taarifa za mali na madeni za viongozi. Kiongozi mmoja wa Marekani aliwahi kusema: *“He who hates the heat, should not enter the kitchen.”* (Mtu asiyependa joto, asiingie jikoni). Kwa maana nyingine, kiongozi wa umma anayetaka mambo yake yasimulikwe au anayetaka usiri, asithubutu kujiingiza kwenye uongozi. Maana uongozi ni dhamana na wananchi wana haki kujua kuhusu uadilifu wa viongozi wao. Unapofika muda wananchi kufanya maamuzi mazito wakati wa uchaguzi, waweze kufanya maamuzi ya msingi kuhusu nani wa kumchagua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara, kwa kuandaa hotuba nzuri kwa mwaka 2008/09.

Pamoja na pongezi hizo nina maoni yafuatayo: nyongeza ya mishahara ni ndogo, haikidhi hali halisi ya mahitaji ya binadamu kutokana na bei ya vyakula, kodi za nyumba, matibabu, gharama za elimu na mahitaji mengine zimepanda sana.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma si waaminifu, si Wazalendo, wavivu, si wabunifu, wanakosa maamuzi ya msingi, wahujumu uchumi, si wachapakazi, wazembe, wanatoa siri za Serikali kwa kupewa rushwa, kuendeleza ukabila, tamaa mbaya, ushindani wa kujipatia mali kwa kutumiwa na maadui wasiokuwa na nia njema na nchi yetu. Hawa ni baadhi wa watumishi ambao ni wachache, lakini wanaathiri uchumi wa nchi na kuathiri amani yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vingi vya mapato ambavyo vingeweza kuboresha mishahara ya watumishi wa umma. Mfano, huko mtaani (uswahilini kwa lugha ya mtaani), chumba kimoja kodi ni Sh.20,000 kwa mwezi kwa nyumba nyenye vyumba sita (hii ni nyumba ya watu wa kipato cha chini), maeneo kama Buguruni, Ilala, Magomeni, Temeke Mbagala na kadhalika.

Nyumba za Wageni (*Guest Houses*) ni eneo muhimu sana na linapaswa kusimamiwa na Halmashauri, lakini utekelezaji wake hauleti tija. Kodi hii ikipewa msukumu na umuhimu, itasaidia kuchochea maendeleo ya Halmashauri husika (angalau kila mgeni alipe Sh. 2,000) kwa chumba.

Nyumba za watu wa Kipato cha Kati; Self Contained ni kati ya Sh. 80,000 - 200,000 kwa mwezi. Hii ni katika maeneo ya Sinza, Tabata, Chang'ombe, Mtoni Kijichi, Segera, Kinyerezi, Bunju na kadhalika. Maeneo ya Kariakoo (Maduka); kodi ni kati ya Sh. 200,000 kwa chumba kidogo cha duka mpaka Sh. 1,000,000 kwa mwezi (inategemea na mita za mraba),

Maoni haya hayahusani na Kodi ya Majengo (*Property Tax*). Baba wa Taifa aliwahi kusema nanukuu:-

“Ili tuendeleo tunahitaji vitu vine; Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora.”

Mheshimiwa spika, katika haya manne wapi kuna tatizo? Nadhani moja na tatu kuna tatizo kidogo, tujirekebishe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia, Makatibu Wakuu wote na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Kwa kuwa Mpango *TASAF II* ni mzuri na umeonyesha mafanikio katika *TASAF I*, kwa wananchi kujua maana ya kuchangia Maendeleo ya Maeneo yao; na kwa kuwa baadhi ya miradi haijakamilika katika awamu ya kwanza; Serikali iiangalie *TASAF II* imalizie miradi hiyo hasa iliyokuwa imebakia kidogo na kwa gharama ndogo. Mfano nyumba za walimu, maji na kadhalika.

Ninashauri *TASAF II* iangalie maeneo ambayo hayakuguswa kwa kina katika *TASAF I*, hasa mikoa iliyo nyuma kimaendeleo na umaskini uliokithiri. Wataalam wetu wa maeneo hayo ambao kazi yao kubwa ni kutoa ushauri na uibuaji miradi, wapewe nyenzo ili wafike kwenye miradi na kuona maendeleo ya miradi (pikipiki).

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Chuo cha Uhazili Tabora unasuasua sana, kiasi kwamba wanafunzi wanasoma kwa tabu na mazingira magumu. Chuo hicho kina historia ya kutoa wanafunzi wazuri. Fedha ziongezwe. Huduma za chakula zirudishwe kama ilivyokuwa zamani, kwani hivi sasa wafuata nje ya chuo na kufanya wasipate muda wa kusoma.

Watumishi waliokaa muda mrefu waondolewe kwenye sehemu hizo hasa Wakuu wa Idara wa Serikali Kuu.

Malimbikizo ya fedha za watumishi wa Serikali zilipwe mapema. Fedha za uhamisho wanazodai watumishi zilipwe wakati wa uhamisho huo.

Makatibu Tarafa wapewe vyombo vya usafiri angalau kwa kukopeshwa kutokana na ukubwa wa maeneo.

Majimbo ambayo ni makubwa yagawanywe Kitarafa ili huduma ziweze kuwafikia wananchi na wao wafike kwenye maeneo husika.

OC ziongezwe ili kukabiliana na mfumko wa bei, hasa kupanda kwa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahara kiongezwe angalau kifikie Sh. 200,000, wataweza kukabiliana na hali halisi.

Wastaafu wa Serikali wanasumbuka; Serikali iweke mikakati mizuri tangu chini, hasa kwa wale watumishi walioko vijijini ambao husumbuka kufuatilia na kukata tamaa. Serikali ikipata uwezo iongeze kiwango kiko chini sana. Vilevile iweke angalau Kitengo au Idara Maalum kila Wilaya kupokea taarifa za wastaafu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake kwa vizuri. Pia ninampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, pamoja na Maofisa wote walioshirikiana kwa pamoja kutengeneza bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Tume ya Kuchunguza Mishahara kwa kuanza vizuri na kima cha chini cha mshahara kuwa Sh. 100,000 bila ya kodi. Kwa kuwa huu ni mwanzo, ninaionba Tume hii iwe makini sana wakati ikitekeleza kazi zake na ifanye kazi kwa kuzingatia hali ya nchi kimapato na upandaji wa bei za bidhaa ili kila hali inaporuhusu waweze kuongeza kima cha chini kwani bado ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jambo zuri sana la kuuendeleza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) kwa kusaidia Miradi ya Maendeleo Vijijini na Mijini. Elimu kubwa inahitajika kwa wananchi, kwa sababu uelewa wa fedha zinazotolewa na

kazi yenyewe ni mdogo. Wananchi hawataki kuchangia ile asilimia ishirini kwa wakati kama masharti yalivyo pia katika ujenzi wa Taifa na kusababisha Wabunge na Wawakilishi kwa Tanzania Visiwani, asilimia ile kuwaelemea wao na kusababisha miradi kuchelewa.

Mheshimiwa Spika Rushwa ni Adui wa Haki na inakomaza maendeleo ya nchi. Rushwa imeshamiri katika miji, mitaa, vijiji hata katika majimbo yetu. Katika majimbo yetu hivi sasa kuna watu wanajiandaa uchaguzi 2010, kwa kuwarubuni kwa fedha na vifaa mbalimbali wale ambao wanadhani wanawapigia kura za maoni na kuchafua maendeleo yanayoendelea na kuwapaka matope viongozi waliopo. Kwa hiyo, ninaomba TAKUKURU ianze kazi hiyo, kama wataona kuna mianya ya rushwa, isisubiri kipindi cha uchaguzi, kama kweli tumekusudia kukomesha rushwa kwenye uchaguzi

Mheshimiwa Spika, hii tabia ya nyaraka za siri kuonekana mitaani ni jambo la kutisha na hatari kwa nchi yetu, inafaa lifanyiwe kazi wajulikane ni akina nani wanatoa siri za nchi.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanajitokeza kwa kuajiri watu wasio na maadili mema na inaonyesha baada ya kuangalia elimu hakuna uchunguzi mwingine unaofanyika. Kwa hiyo, sasa imefika wakati, mfanyakazi afanyiwe uchunguzi wa kutosha wakati wa ajira ili tuajiri watu wenye maadili mema ya nchi hii; tusipoziba ufa tutajenga ukuta.

Mheshimwa Spika, naunga mikono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza, kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Hawa A. Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kazi nzuri wanazozifanya tangu walipoteuliwa kuchukua nyadhifa zao hizi kumsaidia Mheshimiwa Rais. Hotuba hii vilevile ni nzuri na inaonyesha jinsi walivyo karibu sana na jumuiya ya watumishi wa umma wa nchi hii. Aidha, nawapongeza washauri na wasaidizi wao, ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika uandaaji wa Hotuba hii. Mimi kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja hii.

Pamoja na kuunga mkono, ninamsihi Mheshimiwa Waziri katika hitimisho lake asaidie kuueleweshwa umma katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, lipo suala la mishahara ya Walimu ambalo limekuwa likilalamikiwa na walimu wengi. Je, Serikali inayo maelezo gani kuhusiana na *ceiling* ya Mshahara wa Mwalimu wakati akiwa *field ceiling* yake ya mshahara ina kikomo cha H, wakati mwenzake akipata bahati ya kuhamia Halmashauri ya Wilaya (Serikali za Mitaa), *ceiling* yake inaenda had L kutoka G, achilia mbali wale walimu ambao kwa bahati wanaopata fursa za *Presidential Appointments* wanaenda hadi Q. malalamiko yanayojitokeza ni kukosekana kwa maelezo kwa nini walimu hawa wawili; mmoja wa Serikali Kuu mfano Ofisi ya Mkoa au Mwalimu wa Sekondari, licha ya kuwa na uzoefu na umri kazini unalingana watofautiane katika ngazi za mishahara.

Kwa nini Afisa Elimu wa Wilaya (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) awe na ngazi za mshahara zinazomwezesha kupanda hadi L wakati mwalimu wa sekondari licha ya uzoefu na umri sawa kazini kikomo cha mshahara wake kiishie H?

Kwa nini Mwalimu wa Sekondari akiwa Shule ya Msingi akipata nafasi Wilayani kikomo cha mshahara wake kiende hadi L wakati mwenzake anayebakia sekondari au kupata nafasi katika *Secretariat* ya Mkoa asivuke H. Je, utaratibu wa sasa wa kuhamishia Elimu ya Sekondari kwenda Halmashauri za Wilaya itakuwa na mabadiliko yoyote katika utaratibu wa mishahara ukizingatia ukweli kuwa taaluma nyingine zinaenda mpaka Q?

Je, mazingira yaliyopelekea utaratibu huu kuletwa mwaka 2000 na kama ilivyo katika Waraka wa Utumishi Na. 2 wa 2007 bado hayajabadilika na kuhitaji marekebisho?

OPRAS ni utaratibu unaoelekeza kuwa mtu atakuwa anapanda ngazi kutokana na utendaji wake wa kazi. Kwa upande wa walimu tofauti na kupanda daraja lazima ajaze EF. 117 na 7C; fomu zinazotumika katika kumpandisha daraja. Fomu hizi hazipo wazi, zinakuwa na vigezo vinavyoendana na *OPRAS*. Je, utaratibu wa *OPRAS* unatumikaje katika taaluma ya ualimu?

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kubuni na kuanza kutekeleza mradi/mpango huu. Mpango ni mzuri sana na wenye manufaa kwa wananchi wengi, hasa wale ambao hawana rasilimali nyingi zaidi ya ardhi. Kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa mtu kupata ardhi, basi kila mtu anaweza kupata fursa ya kuipata na kuitumia rasilimali hii (ardhi) katika kumwondoa kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, binafsi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, nimetembelea Vijiji vya Kihangaiko, Msinune, Fukayosi na Msoga katika Wilaya ya Bagamoyo. Aidha, nimefika katika eneo la Hanna Nasif (Kinondoni). Pamoja na faida za kiuchumi zinazotajwa moja kwa moja katika mpango huu, mpango huu vilevile unaondoa kabisa migogoro ya ardhi mijini na vijijini. Naomba Mpango huu uharakishwe kusambazwa kwa nchi nzima kwa kuanzia maeneo yenye migogoro ya ardhi.

Wilaya ya Kwimba ni moja ya Wilaya zenye migogoro ya ardhi. Tuhuma nyingi za mauaji ya vikongwe na watu mbalimbali kwa tuhuma za uchawi vingi ukienda kwa undani zaidi vinaishia katika migogoro ya ardhi. Ninaomba sana, pamoja na kuwa tayari mikoa miwili; Dar es Salaam na Mbeya tayari imekwisha tangazwa katika hotuba kuwa inaingizwa katika Mpango wa Bajeti hii. Aidha, kwa kuzingatia hotuba hii vimetajwa vijiji 60 kuingizwa katika Mpango huu, ninaomba sana Mkoa wa Mwanza utakapofikiriwa; Wilaya ya Kwimba, Kijiji cha Bupamwa iongozwe.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni muhimu sana kwa nchi na usalama wa wananchi wake, hasa kwa kuzingatia kuwa haki na usalama wa raia wengi vinaweza kupotea kabisa bila udhibiti wa rushwa. Nionavyo mimi, watumishi wa taasisi hii aidha wanapungukiwa na elimu ya umuhimu wa chombo hiki au hawana uzalendo. Nasita

kusema kuwa hawa uwezo wa kitaaluma, kwa kuwa hiyo ni changamoto inayotakiwa kujulikana kutoka ndani ya taasisi yenyewe. Iwapo taasisi hii, inahisi bado haijapewa nguvu za kutosha ni vyema ikaeleza ni maeneo yapi yanahitaji kuongezewa nguvu.

Kufanya kazi katika taasisi hii si ajira tu bali nidhamu ya kujituma, upendo kwa nchi na kutambua uwepo wa Mwenyezi Mungu kumwogopa na kufanya kazi kwa uadilifu wa hali ya juu ni mambo ya muhimu. Bado tunatakiwa kuweka imani katika chombo chetu hiki. Binafsi, bado naipongeza kwa dhati taasisi hii muhimu kwa taifa letu. Naomba sasa wapitie ajira zao ili kadiri itakavyobidi, wawaondoe haraka watumishi wote tena mapema, wanaochafua sifa ya umuhimu wa chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hotuba hii ni nzuri. Hongera sana.

TASAF mwaka uliopita walitoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 102 bilioni. Mwaka huu zinatengwa Sh. bilioni 49 pekee, karibu nusu yake. Hii maana yake nini? *Executive Secretary* wa Tume ya Mipango kuwajibika kwa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Mawaziri (au Rais wa Jamhuri) hakudhoofisha *effectiveness* ya utendaji wa Tume?

Tume ya Mipango imetengewa *10 billion TShs.* wakati huo huo Kitengo cha Kumshauri Rais Mambo ya Uchumi nacho kimetengewa *385 million TShs.* Hii siyo *duplication*?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mwenye Dhamana ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia. Pia nampongeza Mheshimiwa Sophia M. Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora wa Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, kwa utendaji wa kuridhisha kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa mchango kwenye maeneo yafuatayo hapa nchini:-

Kwanza, naishukuru Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hatua anazozichukua juu ya Mapambano Dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni adui mbaya sana na inadumaza maendeleo ya wananchi; Taifa letu linazidi kuchechemea kimaendeleo. Bado yapo matatizo makubwa ya namna ya kushugulikia matatizo ya rushwa hasa kupitia Idara ya TAKUKURU. Chombo hiki bado kina harufu ya rushwa. Inakuwaje Maafisa wa chombo hiki kujenga

urafiki na Maafisa ambao ndio wanaolalamikiwa na wananchi kuhusu rushwa; mfano, Idara ya Polisi, Idara ya Mahakama, Hospitali na Maafisa mbalimbali wa Halmashauri wanaohusika na Idara nyeti kama zile za Fedha, Ujenzi, Kilimo na Miradi mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, nashauri TAKUKURU Wilayani zifuatiliwe kwa ukaribu ili ufanisi wake katika Mapambano haya ya Rushwa yawe ya kweli na pia isaidie kuondoa dhana ya kudhania TAKUKURU ni chombo kinachoshiriki katika Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Usalama wa Taifa ni muhimu kwa nchi; ndio inayosaidia katika uongozi wa kuiongoza nchi, wawe watu wenye elimu na upeo wa kutosha wa masuala mbalimbali ya kijamii kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba Idara hii sasa ibadilike iendane na hali ya Dunia inavyokwenda hivi sasa hasa kwa kuzingatia Sayansi na Teknolojia. Bado tunaona hasa Mikoani na Wilayani juu ya uadilifu mdogo wa Maafisa wa Usalama wa Taifa. Utoaji siri, kushirikiana na wahalifu na hata juu ya rushwa na kadhalika. Maafisa hawa hujiingiza katika shughuli za kisiasa kushabikia upande fulani kwa nia ya kupotosha ukweli.

Mheshimiwa Spika, ninayosema katika mchango huu ni kweli wala sio uvumi na nitafanya mawasiliano na Wizara au Mkuu wa Usalama wa Taifa ili kumpa viashiria na wahusika ambao nimekuwa nikishuhudia maadili yao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuuendeleza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund – TASAF*). Pamoja na dhamira nzuri ya Serikali kuhusu Mfuko huu, hapa nasisitiza namna ya ugawaji wa Miradi na usimamizi wake unavyokuwa. Bado udhibiti wa fedha za Mfuko huu zimefujwa na kwa kushirikiana na Kamati za Vijiji ambazo hazina elimu ya kutosha. Nasisitiza juu ya kuzielemisha Kamati.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la Sh. 19,240 kwa kima cha chini ni kiwango kidogo sana. Hali ya maisha ya Mtanzania hivi sasa kimaisha iko juu sana, kutokana na kupanda kwa gharama ya maisha kulikosababishwa na mfumko wa bei. Kiwango hiki bado hakitoshi kimahitaji, kiongezwe angalau kifikie Sh. 350,000.

Hotuba haijazungumzia suala la wastaafu; Waziri lazima atueleze namna ambavyo Serikali inalishughulikia suala la wastaafu ambalo hivi sasa ni kero.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona Mheshimiwa Waziri anaeleza katika hotuba yake kwamba, bado kuna Viongozi wa Umma ambao hawaitekelezi Sheria Na. 13 ya 1995 kwa kushindwa kurejesha Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Hivi sheria inasemaje kuhusu hilo? Nashauri Sheria ichukue mkondo wala hakuna haja ya kuwabembeleza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu ya kuweza kuchangia Wizara hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Waziri na Timu yote kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, mchango wangu naenda kwenye mishahara. Mshahara wa kima cha chini shilingi laki moja ni ndogo sana, hautoshi kabisa kutokana na hali ya maisha sasa yalivyopanda; chakula bei juu, mafuta yamepanda na matibabu yako juu na yote yanamgusa mwananchi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ni dhahiri wanaikaribisha rushwa? Tafadhali angalieni tena kwenye bajeti hii kuhusu mishahara inawaumiza wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii haikugusa wastaafu hata pahala pamoja. Wamewasahau wastaafu wetu, ikiwa mshahara waliyokuwa wanalipwa zamani ni mdogo mno, lazima tuangalie maisha ya zamani na leo ni tofauti kubwa; kwa hiyo, tunaomba wastaafu waonewe huruma hawana nguvu tena, angalau walipwe kulingana na mishahara iliyopo hivi sasa kama tunataka kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kupitia Wizara hii kuziwezesha jamii zote Tanzania Bara na Visiwani; Unguja na Pemba kutekeleza jumla ya miradi 1,950 ya *TASAF*. Hili ni jambo la kufurahisha, natoa rai kwa *TASAF*; zile shule za Serikali zilizokwama kwa ukosefu wa fedha na zina upungufu wa madarasa, watoe fedha ili kumalizia majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, nawatakia kila la kheri Mawaziri wote wawili; Mungu awape afya njema na watekeleze majukumu yao vizuri. Amina.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa juhudi za kuboresha hali ya Watumishi wa Umma. Hali ya maisha ya watumishi bado ni mbaya kulingana na kima cha mshahara. Mshahara hautoshi kutokana na hali ilivyo sasa. Mfano, mwalimu anayelipwa Sh. 150,000 ni shida sana. Nyama kilo moja Sh. 3,000 ili aiunge atatumia Sh. 1,000, nauli ya kufuata pesa huko benki, alale *guest* anunue mkaa, kupeleka watoto shule. Hali ambayo inamfanya atumie zaidi ya elfu kumi na moja hivi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ijitahidi kukusanya mapato na kusimamia kinachopatikana na kutumia vizuri ili kima cha chini kianzie Sh. 320,000.

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha vyeo katika Wilaya ya Misungwi, Idara ya Elimu tangu mwaka jana walimu 193 walipandishwa; cha ajabu stahili zao za mishahara zilibaki vile vile.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifuatilie hali hii, nimetoa mfano huo mdogo kwa idara moja tu lakini hata Afya ni hivyo, Kilimo, Maji na Utumishi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ni Mkombozi katika Miradi mbalimbali katika wilaya yangu. Tumefanya vizuri sana katika Sekta ya Elimu na Afya kutokana na vipaumbele vya vijiji husika. Vipo vijiji vilivyopenda vijengewe barabara katika Miradi ya Barabara, pesa za miradi hii inabidi zitazamwe upya kwa sababu sehemu ya kuchangia nguvu inakuwa na pesa kidogo kazi ni kubwa zaidi kitu kinachofanya wananchi kukwepa kufanya kazi na kutafuta vibarua kwingine hivyo, Mfuko uanglie jinsi utakavyoboreshwa ili watu waweze kufungua mawasiliano na ndugu zao na pia biashara itafanyika kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia ajira; nashukuru Serikali inaendelea kuajiri watumishi mbalimbali. Ushauri katika ajira ni vyema Serikali iangalie ajira za mikataba, kwani kuna baadhi ya watumishi hustaafu na kupewa ajira ya mkataba kwa miaka miwili au zaidi kwa kuwa eti huo ni uzoefu. Kitu hiki kinakatisha tamaa vijana wetu wenye nguvu na uwezo wa teknolojia. Ajira hizo ziachwe kwani sasa wapo vijana wanaoweza kazi.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni kikwazo kikubwa kwa juhudi za wananchi kujiletea maendeleo. Kurugenzi iwachukulie hatua haraka wale wanaokamatwa na rushwa; hii itatia moyo umma. Wananchi sasa hivi wametoa woga, wapo tayari kusaidiana na chombo husika, chombo kiwalinde na wahalifu hao watakaobainika ushirikiano ni mkubwa sana kwa umma, tuwaunge mkono kwa kuwachukulia hatua hao watakaobainika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na timu yake. Nina imani kwa hayo niliyoshauri kutokana na umakini wa Waziri wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wazee wastaafu wa Afrika Mashariki wameendelea kupata usumbufu, kiasi cha kupanga kulala nje ya Jengo la Ikulu, jambo ambalo linaashiria unyanyasaji wa hawa wazee wetu waliotumia nguvu, akili na uwezo wao kutumikia Taifa letu. Kwa kuwa ahadi ya kuwalipa viwango stahili imeshatolewa tamko na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa na aliyekuwa Waziri wa Fedha wakati huo, Mheshimiwa Basil Mramba.

(a) Je, ni tatizo gani limetokea kiasi cha Serikali kushindwa kuheshimu Kauli ya Rais na kuendelea kuwanyanyasa wazee hawa ambao hawastahili kabisa kupata usumbufu?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Bunge hili sasa, kuwa imefuta kauli ya Rais Mstaafu kwa viwango walivyostahili kulipwa, kiwango ambacho Mheshimiwa Mramba alisema watalipwa kwa awamu, jambo ambalo limetekelezwa kidogo tu na kiwango ambacho hakikupangwa kwa kushirikisha wazee hao?

(c) Kwa nini Serikali yetu iliwapa wazee hawa tofauti na walivyolipwa wenzao wa Kenya na Uganda fedha za kuwalipa zilitolewa kwa viwango na vigezo vinavyofanana?

Pili, kwa vile Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni nchi inayofuata mfumo au inayojenga jamii ya kijamaa; na kwa vile kwa muda mrefu sasa kunajengeka matabaka kati ya walio nacho na wasio nacho, matajiri na maskini, jambo linaloendelea kujidhihirisha hata kati ya watumishi wa umma ambapo tofauti kati ya watumishi wa juu, kati na chini inazidi kuwa kubwa:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya kina ya mfumo mzima wa mishahara, posho mbalimbali na maslahi ya watumishi wake kujua ukubwa wa tatizo hili, athari yake katika ujenzi wa jamii ya au nchi inayofuata mfumo wa kijamaa na kutoa taarifa rasmi Bungeni ili Bunge kwa niaba ya wananchi liweze kutoa ushauri unaostahili?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa kutokana na tofauti kubwa kati ya mishahara kuna tatizo kubwa la utendaji kazi Serikalini, dalili ya mgomo baridi kwa watendaji wa ngazi ya chini na kati, kukua kwa rusha ndogo ndogo kunakosababishwa na watumishi hao kuhimili gharama ya maisha ambayo imekuwa kubwa sana ikilinganishwa na hali yalisi ya gharama za maisha katika soko?

(c) Je, Serikali ipo tayari kutamka hasa mishahara wa kima cha chini shilingi ngapi kwa mwezi?

Tatu, kwa kuwa mwaka hadi mwaka tunatenga fedha nyingi kwa ukarabati wa Ikulu na mwaka 2008/09 tumetenga 5.7 milioni:-

(a) Makisio halisi ya ukarabati wa Ikulu hadi utakapokamilika ni shilingi ngapi na ukarabari utakamilika lini hasa?

(b) Kwa vile hakuna fedha zinazotengwa kabisa kwa ajili ya ujenzi wa Ikulu katika “Makao Makuu” ya nchi ndio kusema Rais amekwisha amua hakuna kuhamia Dodoma kiasi cha kutotenga kabisa fedha za ukarabati wala ujenzi wa Ikulu Dodoma?

Nne, kwa vile Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaonekana haitoshelezi kabisa katika maeneo kadhaa na hasa sekretarieti kutokuchukua hatua:-

(a) Viongozi wangapi wamekuwa hawatekelezi masharti ya kujaza fomu kwa wakati na wamekiuka sharti hilo waliochukuliwa hatua toka 2005 hadi Mei, 2008?

(b) Kwa vile sheria imeweka sharti gumu sana kwa wananchi na wadau kuona fomu za mali za viongozi; je, lengo hasa la fomu hizo ni nini kama haziwezi kukaguliwa na wadau kuona kama viongozi wamedanganya au la; isitoshe sheria inakataza kabisa mtu aliyeona kutumia taarifa hiyo popote?

(c) Lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria hiyo kufuatana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwa vile Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba, amenukuliwa kwenye vyombo vya habari kuhusu uchunguzi/upelelezi unaofanyika dhidi ya wanaotuhumiwa kwa ununuzi wa rada na kuhusiana na Mtanzania aliyeweka fedha Kisiwa cha New Jersey UK, Waziri/Serikali inaeleza nini Bunge hili kuhusu yafuatayo:-

(a) Kwa nini Serikali haijaanza upelelezi kutumia vyombo vyetu kuhusu watuhumiwa hao wakati sheria zilizovunjwa au zonazotuhumiwa kuvunjwa ni za nchi yetu ambayo ni huru na sovereign? Uchunguzi wa *SFO* ya Uingereza una uhusiano gani na Sheria ya Tanzania?

(b) Serikali inaeleza nini Bunge hili kuhusu taarifa kuwa mhusika wa Rada alifikishwa mbele ya Hakim wa Mahakama ya Kisutu, ambapo inasemekana alikiri kuweka Dola za Marekani 12 milioni kwenye akaunti Uswizi na nyingine akaweka hapa ndani. Hivi kwa nini mhusika huyu aliachiwa bila kuchukuliwa *passport* yake kiasi kwamba leo ndio tunamtafuta na hadi leo Serikali imepata kigugumizi kueleza Bwana Vithlani yuko wapi; kakamatwa au la? Ninaitaka Serikali iliambie Bunge hili, imechukua hatua gani kumpata Bwana Vithlani, kuchunguza kama kweli fedha zilizowekwa Uswizi na Bwana Vithlani ni *percent* iliyotokana na gharama ya ununuzi wa Rada hiyo na hivyo kuifanya Serikali kununua Rada hiyo kwa bei ya juu kuliko bei halisi.

Mheshimiwa Spika, ninahitaji majibu ya kina katika swali hili vinginevyo sitaunga kabisa mkono bajeti hii.

Kuhusu mtanzania aliyeweka fedha New Jersey, Bunge hili lielezwe kwa kina kwanza kama ni kweli Mtanzania huyu aliweka fedha hizo na je, jambo hili si kinyume na sheria zetu za fedha za kigeni na Sheria inayoongoza Benki Kuu? Haya masuala ni ya kwetu Tanzania na hakuna mantiki yoyote kusubiri uchunguzi wa *SFO* kama Waziri alivyotaka Watanzania waelewe. Sheria zilizovunjwa au zinazosemekana kuvunjwa ni za Tanzania na sio za Uingereza. *SFO* inafanya uchunguzi kufuatana na Sheria za Uingereza. Iwapo tunapewa taarifa zisizo sahihi au tunashindwa kusimamia sheria zetu, Bunge lina faida gani kama halipewi taarifa ili liweze kuisimamia vizuri Serikali?

Mheshimiwa Spika, kwa hili nalo iwapo sitapata taarifa ya kuridhisha, sitaunga mkono hoja hii.

Natanguliza shukrani za dhati.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, zipo *reforms* na *restructuring* zinazoendelea Utumishi. *Trend* yake ikoje na inashabihiana vipi na lengo zima la kujenga Taifa letu, lililodhamiria kujenga utamaduni wa ujamaa na kujitegemea? Zipo hoja za *Capitalization, indigenization, nationalization, stratification, socialization* na kadhalika, *reforms* zinaelekea wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja ya Waziri ambayo inawajali wananchi. Napenda kuanza mchango wangu kuhusu ajira kwa watumishi kwenye Halmashauri nchini. Kuna Halmashauri ambazo wana upungufu wa watumishi na inashindikana kuajiriwa kutokana na Wizara ya Utumishi kutokutoa Kibali cha kuajiri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kupandishwa vyeo kwa watumishi kwenye Halmashauri. Kuna maeneo mengi wanapandisha vyeo kwa upendeleo na wengine kutopandishwa kwa kipindi kirefu na kutorekebishiwa mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandishwa mishahara na nyongeza ya Sh. 100,000 ni ndogo sana kulingana na kupanga kwa bei ya vitu na kufanya kiwango hicho kuwa ndogo zaidi ya wakati ule. Naomba mishahara uende sambamba na upandaji wa bei ya vitu kwani mishahara unategemea hali ya bidhaa za matumizi.

Utawala Bora ni suala muhimu kwa maisha ya wananchi lakini taratibu ambazo zinatumikiwa na Mahakama hasa kuwekwa wananchi rumande kwa muda mrefu bila kupelekwa Mahakamani zinakiuka Utawala Bora. Kwa muda mrefu nimezungumza Bungeni kuhusu wananchi waliokamatwa wakichoma nyama porini na kupelekwa Mahakamani, wakahukumiwa kifungo cha miaka arobaini na wakati wanahukumiwa walikuwa hawajui Kiswahili na hakukuwa na mkalimani Mahakamani kwa hiyo hawakuweza kujitetea.

Mimi nategemea kwa nchi yoyote ambayo wanajali Utawala Bora, wangepewa nafasi ya kujitetea kwa kumtafuta mkalimani ili nao wakiri au watoe maelezo yao. Naomba nipate majibu ya haki ya wananchi hao ambao wamekamatwa Loliondo na kupelekwa Mkoa wa Tabora kuhukumiwa huko kwa sababu mifugo waliofuatwa ni wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, familia za watuhumiwa hao hawakujua watu wao wako wapi kwa muda wa miaka mitatu bila kufahamika! Naomba maelezo.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, wakati kamati ya kutafuta maoni ya mfumo wa vyama vingi ikiongozwa na Jaji Nyalali ikihitimisha ripoti yake

alipendekeza Serikalini Sheria 40 zifutwe na mpaka leo hazijafutwa. Miongoni mwa Sheria hizo ni ile Sheria ya kuingizwa au kutiwa ndani bila ya kupelekwa Mahakamani kwa Amri ya Rais.

Sheria hiyo licha ya kuleta muingiliano wa kazi za Mahakama na Serikali bali pia haileti ishara nzuri kwa Utawala Bora. Kwa msingi huo, bado Utawala Bora utaendelea kuwa mashakani kama Sheria hizo 40 hazijafutwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mkutano wa Pili wa Bunge hili Aprili, 2006, niliwahi kumwuliza Waziri wa Usalama wa Raia juu ya hatua gani imechukuliwa kwa Vikosi vya Zanzibar waliomuua mwanafunzi Juma Omar wa Shule ya N'gombeni huko Wilaya ya Mkoani wakati wa undikishaji. Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa, suala hili lipo katika uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo haijachukuliwa hatua yoyote kwa wahusika hao. Inaonyesha wahusika hao wapo juu ya sheria na kwa sababu wameuwa na hawakuchukuliwa hatua yoyote, basi wanaweza wakafanya lolote kwa raia bila ya kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa spika, ni dhahiri kwa hali hiyo Utawala Bora haupo. Ieleweke Jeshi la Polisi nido lenye jukumu la kulinda usalama wa radia na mali zao. Maisha yanapokatishwa (anapouliwa mtu), wana wajibu wa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza mshahara kuanzia kima cha chini lakini kutokana na ongezeko la bei ya bidhaa, bado mishahara hiyo ni midogo. Serikali ifikirie upya juu ya ongezeko hilo.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wote kwa kuandaa hotuba na bajeti nzuri ya mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unahusu malipo madogo ya wastaafu, ambayo yanalalamikiwa sana na wastaafu tunaishi nao majimboni.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako ni kwa sababu gani Serikali mpaka sasa imeshindwa kuongeza kiwango cha malipo ya pensheni kwa wastaafu? Pili, ni lini Serikali itaamua kupandisha kiwango cha malipo ya pensheni?

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri atoe taarifa, idadi ya wastaafu hivi sasa kutoka katika ajira Serikalini ni wangapi na wanaigharimu Serikali shilingi ngapi kila mwezi? Idadi ya wastaafu hivi sasa kutokana na ajira zilizotokana na mashirika ya umma ni wangapi na wanagharimu shilingi ngapi kwa mwezi?

Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ibara ya 105 (a), (b) na (c) za Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005, ziliwataja wazee wastaafu kama ni rasilimali zenye thamani kubwa Kitaifa kwa mchango walioutoa walipokuwa waajiriwa; na kwa kuwa ibara ndogo (b) imetamka bayana kuwa Serikali itaweka utaratibu wa malipo ya pensheni kwa wastaafu kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na hali ya maisha; je, Serikali haitambui mabadiliko makubwa ya kupanda sana kwa gharama za maisha?

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri anatambua kupanda kwa gharama za maisha. Kwa hiyo, naiomba Serikali itoe nyongeza ya kutosha kwa malipo ya pensheni kwa wastaafu ili wamudu, gharama za maisha, angalau kwa kiasi fulani, badala ya malipo ya Sh. 21,000.00 ambazo wastaafu wengi wanalipwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa dhamira aliyoionyesha katika hotuba yake kwa kuendelea kuwahudumia inavyostahili Viongozi Wastaafu wa Kitaifa 12. Hii inapendeza sana, kuwaenzi viongozi hawa kwa utumishi wao uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ikumbukwe kuwa, Viongozi wa Kitaifa, waliosaidiwa na baadhi ya wastaafu kwa njia moja au nyingine, kwa utumishi wao katika Serikali au Mashirika ya Umma waliyokuwa wakiyatumikia. Kwa hiyo, ni budi wastaafu hawa wakaenziwa kwa malipo mazuri ya pensheni, kuonyesha kuwathamini. Naiomba Serikali itimize ahadi hii, iliyotamkwa katika Sera ya Chama cha Mapinduzi kabla muda wa kuwepo madarakani kumalizika.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naamini Serikali itachukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya hadi leo hii.

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahara cha shilingi laki moja hakitoshi. Kima hiki hakimpatii mtumishi chakula, mavazi, usafiri wa kwenda na kurudi kazini, kusomesha watoto wake na kupata matibabu na kadhalika hivyo nashauri kima cha chini kiwe baina ya Sh.250,000 na Sh.300,000.

Mheshimiwa Spika, wastaafu ni watumishi ambao wametumia muda wao mwingi kuwatumikia wananchi. Wamefanya kazi kwa kipato kidogo, katika mazingira magumu lakini kwa uaminifu mkubwa. Inasikitisha kwamba, watumishi wa umma wanapostaafu wanakuwa na maisha duni zaidi ya wale wananchi wa kipato cha chini. Hivyo, nashauri mafao ya wastaafu yaangaliwe upya ili na wao baada ya kustaafu wafurahie utendaji wao walipokuwa watumishi wa umma, badala ya kujuta kwa kupoteza muda wao bila mafanikio. Naomba pensheni za wastaafu ziongezwe ili ziweze kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni utawala unaoendeshwa kwa kufuata sheria, unaojali maslahi ya wananchi wote na hauwabagui watu kutokana na nafasi zao baina ya wenye kipato kidogo na kikubwa, baina ya waliopo madarakani na walala hoi. Hatua za kisheria zichukuliwe kwa wakubwa na wadogo bila ya kujali vyeo vyao bali yaangaliwe makosa yao na adhabu au hukumu zitolewe kulingana na makosa mfano suala la ufisadi.

Mheshimiwa Spika, madaktari, manesi na wafanyakazi wengine wa afya wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi. Hivyo, wanastahili kuangaliwa vizuri katika maslahi yao ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi na kwa ufanisi zaidi. Pamoja na hayo, wapo baadhi ya manesi wanaonyanyasa akinamama wanaokwenda hospitali kujifungua. Wafanyakazi hawa wanahitaji kusimamiwa kwa makini zaidi hasa ikizingatiwa wengine huwa wamekaa katika vituo vya kazi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, lakini kwa sasa taasisi hii inaonekana kushughulikia rushwa ndogo ndogo zaidi wakati rushwa kubwa kubwa bado hazijashughulikiwa ipasavyo. Hii inapelekea rushwa kubwa kubwa pamoja na rushwa ndogo ndogo kuendelea kuongezeka badala ya kupungua. Taasisi hii inapaswa kushughulikia rushwa kwa uzito wake; vinginevyo, nchi yetu inaelekea pabaya. Ahsante.

MHE. ANNA MAULIDAH KOMU: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwa pamoja na kuchangia hoja/hotuba hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naanza na Utawala Bora. Utawala Bora ni muhimu kwani mtawala anapokuwa bora, muwajibikaji na anayejali maisha na maslahi ya anaowatawala, basi siku zote wale wanaomchagua au kumteua atawale huwa wanashukuru na kufurahia mtawala wao.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko unapoona mtawala anashindwa kujua shida na dhiki zinazowakabili anaowatawala na mwisho wa siku watawaliwa wanapochoka basi ni hali mbaya kwa mtawala.

Rushwa ni mdudu mbaya aliyekomaa kichwa kwenye nchi yetu hii. Rushwa imekithiri inamnyima haki yule anayetawaliwa, ambaye ndiye aliyemuweka mtawala. Rushwa imekuwa kama haki ya yule anayedai kwani mtoa rushwa asipotoa basi kwa upande wa huduma hukosa kabisa na akabaki analalama au kufa.

Rushwa humuweka mnyonge mahala pabaya katika maisha yake, kwani hata kama hajakosa hubambikiziwa kosa na kusweka gerezani bure. Kama leo tungezunguka magerezani na kuuliza haki basi walio wengi hufungwa kwa kukosa fedha za kuhonga au kubambikiziwa kosa la uwongo.

Rushwa inaleta wasomi wa uwongo na wale wanaosoma kikweli wakakosa vyeti kwa sababu hawakuwa na fedha za kununua mitihani au kuhonga wapewe vyeti vya uwongo na wao si wa kupata vyeti husika.

Rushwa imetoa leseni za uwongo na kusababisha ajali za magari na wananchi wengi kukosa maisha yao au vilema maisha yote.

Rushwa imetuleta Viongozi wabovu kila mahali kwa kuhongwa wananchi hasa wakati wa Kampeni za Uchaguzi na kumfanya aliyekuwa na fedha nyingi za kuhonga kuwa kiongozi na anapokuwa kiongozi na yeye hatendi haki huendelea kudai hongo.

Mheshimiwa Spika, tukitaka kuondoa hongo au rushwa tuhakikishe mishahara inakuwa ya kujali maisha ya mfanyakazi, sisemi utoshe kwa sababu siku zote fedha haitoshi lakini angalau zimpunguzie matatizo yale ya muhimu.

Kuhakikisha vifaa vya huduma kama dawa, vifaa vya uzazi, mashine za kupimia wagonjwa, elimu ya kutosha kwa manesi na wahudumu wa zahanati na mahospitalini na vifaa vya mashuleni vya kufundishia na kujifunza. Mahakamani kuwe na uwazi wa ukweli wa Mahakimu wetu kutenda haki na kutoa hukumu iliyo ya ukweli. Hawa Mahakimu wanahitaji mishahara na marupurupu ya kutosha na pia elimu ya kutoa haki sio uwongo na kote hata polisi.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni kazi ngumu na inahitaji kujitua kwa wale wanaotawala sio kuwa wababaishaji kwani siku zote penye ubora wa kutawala na Mungu huwa nao.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Ofisi ya Rais, ina shughuli kubwa ya kuimarisha Utawala Bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Kuna tatizo kubwa siku hizi la kufanya kazi kwa ufanisi katika Idara nyingi za Serikali. Kuna *Laxity* kubwa.

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilionyesha hivyo, kuwa kuna tatizo katika kujituma, pale alipotoa mfano wa kutochukua hatua ya kupeleka *formal application* kwenye Serikali ya India kupitia Ubalozzi wake nchini. Sidhani kama huyo afisa hajui kuwa tuna matatizo ya mabehewa na vichwa vya treni katika Reli ya Kati. Ni jambo la kutojali wajibu wake, yaliyomfanya Afisa huyo kuacha mambo yaende kama yalivyo.

Wizara inazindua mipango mingi ya uboreshaji huduma katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma; kama maonyesho ya maboresho hayo hayaendani na vitendo ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni Taasisi muhimu sana katika Utawala Bora. Tume ya Jaji Warioba ilibaini wazi Idara ambazo zinaongoza kwa vitendo vya rushwa. Idara kama Mahakama na Polisi zina vitendo vya waziwazi vya rushwa na ambavyo kama taasisi hii ingejizatiti rushwa ingepungua sana.

Kwa mfano, sikutegemea hii leo kusikia kuwa kuna wafanyakazi hewa, baada ya sensa iliyofanyika miaka ya 80 na 90. Kwa nini TAKUKURU isiingie ndani ya Idara za

Serikali na kubaini hao maafisa wanaowatengeneza hao wafanyakazi hewa? Kutokana na wafanyakazi hewa, Serikali imepata hasara kubwa ya fedha kulipa watu hewa. Kiasi cha fedha iliyopotea, ingeweza kuchimba visima vingapi kwenye maeneo yenye matatizo ya maji? Je, hao watumishi wanaojiri watumishi hewa wamechukuliwa hatua gani?

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni mzuri na unaweza ukatoa fursa nzuri kwa wananchi waishio mijini na vijijini. Ni muda mrefu sasa, mpango huu unaongelewa kuliko kufanyiwa kazi.

Katika mkutano wa kumi na moja tulipitisha Sheria ya *Financial Leasing*. Inawezekana taasisi, makampuni yatakayojihusisha na ukodishaji rasilimali wakahitaji wadau kuwa na rasilimali zilizorasimishwa. Kama mpango huu utaharakishwa, basi wananchi wengi watanufaika na dhana nzima ya *Financial Leasing*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tuwafikirie wastaafu kwa ku-peg mishahara yao kwa thamani ya fedha ya sasa. Wengi wa wastaafu wetu ambao wametoa mchango mkubwa wa huduma katika nchi yetu, wanaishi maisha magumu sana. Kiasi cha Sh. 21,706 ni fedha ndogo sana. Serikali itekeleze kila kinachoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha CCM kuhusu wastaafu.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote, nitoe pongezi kwa Mawaziri; Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais katika Wizara husika, kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa hotuba ya ofisi hii.

Kabla sijaendelea na mchango wangu, naomba nitamke kuunga mkono hotuba hii kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Mipango ni vyombo ambavyo maamuzi yake yanatazamwa na kila mtumishi kuwa dira ya maendeleo au kukwama kwake. Maamuzi sahihi ya vyombo hivi viwili ndio muhimili wa uhai na ufanisi wa Sekta ya Utumishi wa Umma na hata Sekta Binafsi kwani hali ya maisha na mwelekeo wa maendeleo ya uchumi kwa jumla, vinategemea taswira ya menejimenti na mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ngumu ya maisha ya Watanzania kwa jumla, hali ya watumishi wa umma hususan wale wa kima cha chini ni mbaya. Hali hii ni mbaya zaidi kwa watumishi wa vijijini. Mfano hai ni hali mbaya za watumishi katika vijijini vya Jimbo la Mbozi Magharibi, ambao licha ya mishahara wao kutokidhi mahitaji yao kwa angalau hata wiki mbili, hulazimika kukopa fedha ili kudandia usafiri wa kuwafikisha makao makuu ya wilaya kufuata mishahara yao, (pale wanapobahatisha usafiri wa aina hiyo, kwani kutokana na kutokuwepo kabisa miundombinu ya barabara au kuwepo barabara mbovu karibu jimbo zima halina usafiri wa uhakika). Matokeo yake, watumishi wengi wanagoma kufanya kazi atika Jimbo hilo, ama wale wachache

wanaokubali kuja hufika kuripoti na kukaa muda mfupi. Wakishachukua masurufu yao ya usumbufu, huondoka na kwenda maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na hali hii ambayo hatima yake ni uwiano mbaya wa maendeleo ya wananchi katika majimbo mbalimbali ya nchi hii, suala la maslahi mazuri kwa watumishi wa umma, ikiwa ni pamoja na mshahara mzuri, litazamwe kwa kina na kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. Watumishi wa umma wanaopangiwa kazi vijinini, kwa hali ilivyo sasa wanaona kama wameadhibiwa badala ya kuona kuwa wamepewa jukumu kubwa la kuwaondoa wananchi wetu kwenye lindi la umaskini, ujinga na magonjwa mbalimbali ambayo husababisha vifo visivyo vya lazima.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati Serikali ipitie upya utaratibu wa kuwachukulia Waheshimiwa Madiwani kuwa si waajiriwa na hivyo kutopewa mshahara, badala yake kupewa posho ambayo kiwango chake ni cha kusikitisha. Kundi hili la Wawakilishi wa Wananchi lina kazi kubwa za kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwenye Kata zao mbali na shughuli za Halmashauri za Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Kwanza kabisa, nawapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Makatibu Wakuu wote, pamoja na Watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, kuna watumishi ambao waliachishwa kazi kutokana na kuugua lakini baada ya kuachishwa kazi walitibiwa na kupata nafuu kabisa. Watumishi hao wameomba kurudi kazini walipwe kwa mkataba, lakini Serikali haiwajali; je, wanatendewa haki? Kwa mfano, sasa hivi kuna uhaba wa watumishi katika zahanati nyingi hakuna Wauguzi na Mabwana Afya, lakini wamekosa ajira tena.

Watumishi wanaofanya kazi ambao walimaliza darasa la saba walioko kazini, Serikali haitaki tena wajiendeleze na wala haiwapandishi vyeo. Wanaotakiwa kujiendeleza na kupandishwa vyeo ni *form four*; je, hawa darasa la saba walioko kazini ni nani atakayewaendeleza bila Serikali kuwaendeleza na kuwapandisha vyeo? Je, huo ni Utawala Bora wa kunyimwa watumishi nafasi ya kutaka kujiendeleza?

Mheshimiwa Spika, watu hawa wapewe nafasi ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, wastaafu waliokuwa *East African Community* wanapata shida sana. Katika Kanda ya Tabora, wastaafu hao wakifika pale kutafuta mafaili yao wanaambiwa kumbukumbu hakuna, wanalala stesheni wakitoa rushwa mafaili yanapatikana; je, huo ni Utawala Bora? Tulidhani wakati huu wa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, utendaji utakuwa wa ari na kasi kumbe mambo ni yaleyale ya zamani. Jamani, wastaafu hao walipwe haki zao.

Kuna wastaafu ambao barua zao za ajira zilipotea na nyingine ziliungulia ndani. Watumishi hao walijiriwa mwaka 1965 na nyaraka hizo zipo ofisini lakini wao hawana kwa sababu ziliungua, wastaafu hao wafanye nini ili wapate malipo hayo na kule kwenye kanda zao hawataki kuwatafutia mafaili; sasa wafanye nini ili walipwe?

Kuna wastaafu wengine tunawaelewa ni jirani zetu; je, hatuwezi kuwaleta hazina ili watoe maelezo yao jinsi walivyoanza kazi na waeleze vyeo vyao?

Mheshimiwa Spika, ninaomba majibu ya Serikali. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Waziri mwenzake, pamoja na Watendaji wa Ofisi zao kwa kuandaa hotuba hii ambayo imewasilishwa leo. Baada ya hapo, naomba nichangie machache.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie upya kuhusu kima cha chini cha mshahara ambacho ni Sh. 100,000, ambazo hazikidhi gharama za maisha kwa sasa. Kila kitu kimepanda ukiacha gharama za kupanga nyumba, matibabu, elimu kwa watoto na gharama ya chakula, kwa maana hiyo kima hicho hakiwezi kabisa kugharimia maisha. Mshahara huo ndio unaosababisha watumishi kula rushwa, kuiba na kwa hivi sasa ndio mtindo wa mafaili kupotea ili angalau apate kitu chochote aweze kuishi.

Mheshimiwa Spika, ningepomba Serikali iangalie kima cha chini cha wastaafu ni kidogo na kiasi wanachopata hakina nyongeza ya kila mwaka (*increment*), naomba Serikali iweke uratibu wa kuongeza kima cha chini cha wastaafu na nyongeza ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie wazee waliopigana Vita ya Pili na posho ambayo baadhi yao walikuwa wakipata na wengine hawakupata. Ningependa kujua kilichotokea ni nini mpaka posho hiyo haipatikani na wale ambao walikuwa hawapati kabisa wafanye nini ili wazipate? Ningepomba kama kuna haja ya kuleta majina au jina nipate maelekezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nampongeza Waziri (Mawaziri) na naunga mkono hoja.

Hoja za msingi; watumishi kumi (Watendaji Kata) na watumishi wawili wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea; Philoteo Mhagama; Teofanes Mlelwa; Mrisho Luambano; Moses Komba Regina Nyoni; Geoffrey Mapunda; Canisius Lingowe; Notkev Tewele; Barnabas Chipeta; na Filoteus Haule; ambao ni *WEOs* na Mariamu mbawala, ambaye ni *Accounts Assistant* na Kassim Khalifa, ambaye ni *Record Management Assistant*; watumishi hawa walijiriwa kwa kufuata taratibu zote za kihalali katika siku

za nyuma miaka ya 90, lakini mpaka leo hawajaingizwa katika *payroll* na kusababishiwa kutotambulika na vyombo vyovyote. Hawajui uhakika wa mafao yao siku za usoni na wanadharaulika kuwa bado ni vibarua.

Kisheria hawa ni watumishi halali kwa kuwa wakati wanaajiriwa walikuwa na sifa zote halali. Barua ya tarehe 3 Mei, 2007 ya Katibu Utumishi, Ndugu Mchau, anadai watumishi hawa hawakuajiriwa kwa mujibu wa Sheria na Waraka wa Rais Na. 1 wa Mwaka 1998. Hata hivyo, barua hiyo inasisitiza kwamba, haupo ushahidi kwamba taratibu za ajira zao kama zilizingatiwa kwa mujibu wa Kanuni D 11(a) (i – iv) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo la 1994. Katibu Mkuu baada ya kunukuu vifungu hivi, hatoi ufumbuzi wa tatizo, hizo ni sababu tu za kurejesha taarifa za watumishi hawa kwa Mkurugenzi.

Katika orodha hiyo, yupo mtumishi aliyeajiriwa miaka ishirini na saba tangu aajiriwe hajaingizwa katika *payroll* ya Serikali ingawa maombi yameletwa kwako mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ninamwandikia Mheshimiwa Waziri nikiomba watumishi hawa hawakuwa na makosa yoyote katika mfumo wao wa ajira, leo Serikali inawaadhibu kwa kosa ambalo haliwahusu. Naomba sana watumishi hawa watambuliwe na waingizwe katika *payroll*. Wanakosa haki, hawathaminiwi na wananyanyasika, tafadhali naomba suala lao lifikie mwisho kwa kujali huduma yao waliyofanya katika maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda mrefu sasa watumishi waliostaafu miaka mingi iliopita wamekuwa na tatizo kubwa la malipo yao kutolingana na hali halisi ya maisha; napendekeza kuwa kima hicho cha pensheni kipitiwe upya kulingana na mfumko wa maisha kwa ujumla wake.

Naishukuru Serikali kupandisha kima cha chini, kinapanda kulingana na viwango vya mishahara na hasa Mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa MKURABITA nashauri sasa uhame kutoka katika dhana ya mwanzo ya majaribio. Serikali itenge fedha/fungu maalum la kuhakikisha kuwa, Elimu na Utekelezaji wa Mkakati huo uenee nchi nzima (faida zake). Mradi huu utawasaidia wananchi kuonja hali ya umiliki halisi wa ardhi na faida zake. Mradi utasaidia nchi pia kuwa na orodha halisi ya hali ya umiliki wa rasilimali nchini.

Mheshimiwa Spika, masijala za uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi zitasaida pia kuhifadhi pia nyaraka za vizazi na vifo na hata mambo mengine vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itusaidie kutoa mwelekeo na maendeleo ya utekelezaji wa mikataba ya huduma bora kwa wateja kimkoa, kiwilaya na hata kitaifa. Bado urasimu ni mkubwa serikalini na bado watumishi hawapati huduma zao kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *TASAF* tunaupongeza sana, umeonyesha kuleta maendeleo katika vijiji. Tatizo dogo ni la kuchelewa kwa utoaji wa fedha kulingana na nyakati katika mwaka na hasa mipango ya kimisimu ya wananchi katika kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala la watumishi wa umma, haki zao na mishahara yao kuweza kuboreshwa ili wananchi hao waepukane na rushwa.

Kuhusu suala la Hospitali za Mikoa na Wilaya, naomba kufahamishwa kama katika Hospitali za Serikali kuna suala la Watendaji hawa kuwajibika? Kiutendaji huwajibika kwa *RAS* Mkoani, nadhani sheria hiyo haijamtendea haki *RMO* waliopo Mkoani. Malalamiko mengi ya wananchi yanaanzia hapo, hawawezi kumheshimu hata kidogo maana Mganga Mkuu naye anawajibika wa *RAS* Mkoani au kwa Mkuu wa Mkoa na chombo kinazingatia haya ili kujibu matatizo ya wauguzi yanaanzia wapi.

Naomba kufahamu kwa nini fomu za maadili wapo ambao hawajazijaza nanyi mmenyamaza kimya na mnaona ufahari kutusomea hapa; na je, mmechukua hatua gani na ni wangapi wamesimamishwa uongozi kama fomu zinavyosema? Naomba majibu ya ufuatiliaji huo. Watendaji wangapi ambao hawajazaza fomu hizo?

Utumishi wanasimamiaje wastaafu wa Afrika Mashariki? Hili ni jambo ambalo hutia aibu sana katika nchi hii, kuona bado wana kero kubwa sana, tufike mahali tuamue moja; kumaliza haya kabla ya 2010 na yawezekana kama tunaamua na kusimamia hayo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wote wawili na kwa kuwa ni wanawake wenye uwezo, nina imani watatenda mazuri na watazingatia hoja za Wabunge na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, Mawaziri walioleta hotuba hii yenye mwelekeo mzuri kwa Taifa letu juu ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, sambamba na Mawaziri, nampongeza pia Ndugu Philemon Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi; Ndugu Michael Mwanda, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais; Ndugu Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na Ndugu Charles Mutalemwa, Katibu Mkuu (Kazi Maalum), Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la wenye viwanja vya ufukweni mwa Bahari ya Hindi, pamoja na wenye hoteli kutofuata Sheria za Ardhi na Sheria za Matumizi ya Ardhi za Fukwe Tarafa ya Kigamboni, ambazo ni muhimu kutekelezwa kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi kufika kwenye fukwe kwa matumizi ya uvuvi au mapumziko.

Sheria hizo ni kama ifuatavyo: Kila mwenye kiwanja kuwajibika kuacha mita moja na nusu kila upande sawa na upana wa mita tatu baina ya kiwanja na kiwanja. Kuacha mita sitini (60) kutoka baharini hadi kwenye fukwe kwa ajili ya matumizi ya jamii (matumizi ya kila mwananchi).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapa sheria na taratibu hizo, lakini haitekelezwi kutokana na kuwepo rushwa baina ya wamiliki hasa wa hoteli na Idara ya Ardhi na Mipango Miji ya Manispaa ya Temeke au Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba Idara ya Rushwa ishughulikie kero hii, wananchi wananyanyasika sana, Sheria ifuate mkondo wake au hatua zichukuliwe.

Chuo cha Utumishi wa Umma (Utumishi) ni kikongwe sana (cha muda mrefu) ni vyema sasa kipewe msukumo zaidi kwa maana ya kuelekea kwenye hadhi ya Chuo Kikuu kama vilivyorekebishwa vyuo vingine. Hii ni kwa madhumuni ya kuweka uhakika wa kuzalisha wataalam utumishi, utawala na uendeshaji kazi au angalau kuanza kutoa *diploma*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana kwa kusimamia Maendeleo ya Jamii Tanzania. Watumishi hawa kwa sasa wanawajibika moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya na Manispaa. Ni wasimamizi wa miradi ndani ya Halmashauri zetu, lakini kwa bahati mbaya sana hawana ushusiano wa moja kwa moja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naiomba Serikali – Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itoe maamuzi ya kuwapa Mamlaka, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ya kuwamilikisha Maafisa Maendeleo ya Jamii. Aidha, nashauri kutokana na umuhimu wake, tuangalie uwezekano wa kuanzisha ngazi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii Mkoa.

Mheshimiwa Spika, pale Mjimwema, Tarafa ya Kigamboni kulikuwa na *State Lodge* ambayo Baba wa Taifa, Marehemu Julius K. Nyerere na Mheshimiwa Kawawa, pamoja na Mheshimiwa Aboud Jumbe, walikuwa wakiiitumia sana sasa imetupwa. Nashauri uangliwe uwezekano wa kuifufua katika maeneo ya fukwe ya Kigamboni ni muhimu.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia, pamoja na Makatibu Wakuu, Watendaji na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Hongereni sana.

Naomba nipate ufafanuzi wa upande wa Halmashauri zetu kwa nini baadhi ya watumishi wakiwemo Mkurugenzi wa Halmashauri na wengine, huajiriwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, badala ya kuajiriwa moja kwa moja na Halmashauri husika kwani uwajibikaji huwa ni mgumu sana?

Pili kuhusu Hati Safi au Chafu; je, Watendaji wanapewa adhabu gani hasa pale watumishi wanapokiuka taratibu za kazi hadi kupelekea Hati Chafu? Wale wanaofanya kazi vizuri; je, Wizara yako ina vigezo vya Kisheria kuwapa motisha?

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Baada ya hapo naomba nichangie kama ifuatavyo:-

TASAF ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Madhumuni yake ni kuwahamasisha wananchi maendeleo yao kwa kuchangia. Mfuko huu ungefaa sana kwa kusukuma maendeleo sehemu za pembezoni mwa nchi, lakini inaonekana kuna urasimu sana katika kupitisha Miradi ya Maendeleo ya Wananchi. Mfano, Wilaya ya Chunya ni mojawapo ya Wilaya Kongwe sana lakini pia iko *underserved* sana. Wilaya hii imeidhinishiwa miradi michache sana na *TASAF* inaisha mwaka kesho; naomba sana *TASAF* waidhinishe miradi yote iliyo mezani toka Wilaya ya Chunya. Naogopa sana isije ikawa Mpango wa MEM ambao haukufaidisha sana sehemu za pembezoni mwa nchi.

Nchi ya Ireland miaka ya sabini mwanzoni ilikuwa na uchumi duni sana ulaya. Kwenye mwaka 1971, Serikali iliwaita wataalam na wasomi wote na kuunda Tume ya Mipango; walijifungia kama *Think Tank* kwa muda mrefu kiasi na kutafakari namna ya kuinua uchumi wa nchi hiyo. Mapendekezo yao yalipofanyiwa kazi, sasa nchi hiyo uchumi wake unaongoza Ulaya. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuiwezesha sana Tume ya Mipango na kuwashirikisha wasomi wetu hasa wachumi, wasaidie kutoa mawazo namna ya kuinua uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha na hii sasa ya Wiziri wa Utumishi, MKUKUTA na Mini-Tiger 2025 haijaonekana sana. Hivyo, itakuwa vigumu kuendeleza *SEZ* na *EPZ* kwa kuinua uchumi wa nchi. Naomba sana Tume ya Mipango iendeleze mipango hii.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Nawapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, pamoja na Watendaji wote katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa matayarisho mazuri ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

Napenda kuchangia maeneo yafuatayo: MKURABITA ni nzuri, kimsingi tatizo utekelezaji wake ndio ambao unasuasua sana. Je, mpaka leo ni wananchi wangapi na katika sehemu zipi za nchi yetu wamekwisha kufaidika na utaratibu huu? Ningependa kufahamu wananchi ambao wamekwishapata mikopo toka kwenye Mabenki chini ya Mpango wa MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kukamilisha ukarabati wa majengo ya Chuo cha Utumishi wa Umma yaliyopo Dar es Salaam. Shughuli za ukarabati wa majengo zinaendelea pia katika Kitengo cha Chuo kilichopo Tabora, lakini ukarabati huu unakwenda polepole. Naiomba Serikali iongeze kasi ya ukarabati wa majengo ya Chuo Mjini Tabora.

Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Tume ya Mipango. Mpaka sasa inaelekea Muundo wa Tume hii bado umewaacha nje maafisa wengi waliokuwa katika Wizara ya Mipango na Uchumi. Ni vizuri hatima ya wafanyakazi hawa ikaamuliwa

mapema ili wafanyakazi hawa wasiendeleo kukaa katika hali ya wasiwasi kuhusu hatima ya ajira zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa hotuba nzuri na iliyobeba majukumu mazito katika Uongozi na Taifa. Taarifa zilizotolewa katika hotuba zimeeleweka na ndiyo maana michango inayotolewa ni ya kuboresha hoja tu. Wapinzani wanakosa yale mazuri yote, maana kama yanayoelezwa ni mambo mabaya wasingekuwa na hoja!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala bora, Makatibu Wakuu; Bw. Yambesi na Bw. Mwanda, Wakuu wa Taasisi chini ya Ofisi ya Rais, pamoja na Wasaidizi wao, kwa kumsaida Waziri mtoa hoja kwa uadilifu, uaminifu na juhudi kubwa hadi kumwezesha kutoa hoja yake Bungeni kwa ufanisi mkubwa.

Narudia tena kutamka kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea na ushauri wa kiutendaji kwa Wizara hiyo, napenda kutamka rasmi kuwa naiunga mkono hoja kwa asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Hotuba ya Waziri mwenye dhamana, pamoja na Wataalam wake, kwa kuwa hotuba yake imegusa maeneo yote muhimu.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Dola vya Usalama wa Taifa, pamoja na TAKUKURU, napenda kuvipongeza kwa utendaji wake mzuri kwa maana kwa utendaji wa kila chombo kwa nafasi yake. Mbali na utendaji mzuri ambao vyombo hivyo vinafanya, lipo tatizo kubwa la vyombo hivyo kufanya kazi katika mazingira magumu na hasa usafiri wa magari ya kuaminika kwa kazi za *operations*. Magari yanayotumiwa na vyombo hivyo hayakidhi mapambano dhidi ya wahalifu.

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilieleza umuhimu wa vyombo hivyo kutokutengewa fedha za ununuzi wa magari. Kwa mara nyingine, nasisitiza kuwa Wizara hii kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, wasaidie upatikanaji wa fedha za kununulia magari. Kwa mfano, wakati TAKUKURU wana jukumu la kupambana na watoa rushwa na wala rushwa, lakini maafisa wake hawana nyumba za kuishi, badala yake hukaa uraiiani, mahali ambapo wanaweza kudhuliwa kwa urahisi na watuhumiwa. Aidha, aina ya magari yaliyopo kwenye Mikoa na Wilaya ni madogo yasiyoweza kukidhi mahitaji. Hali kadhalika ofisi katika wilaya. Magari ya Usalama wa Taifa nayo yote yamechoka, hivyo, nashauri pia

yanunuliwe magari mapya na ya kukidhi utendaji na hasa yale ya Maafisa Usalama wa Wilaya ambao kazi zao ni zile za kuzunguka vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza pia utendaji wa *TASAF* kunakotokana na utendaji wao mzuri kwa nchi nzima. Miradi yote inayosimamiwa na *TASAF* kwa ngazi ya Wilaya inakwenda vizuri isipokuwa Miradi inayochelewa kukamilika ni kutokana na kuibuka kwa Miradi mipya kunakojitokeza. Hata hivyo, napongeza sana utendaji wa *TASAF* na pongezi pekee ziufikie Uongozi wa Taifa hadi ngazi ya chini. Ni Watendaji wanaojituma na wenye ushirikiano mzuri.

Angalizo kuwa kwa chombo cha TAKUKURU ni kuwa makini sana na watu wanaotumia jina la chombo wakati siyo watumishi na hasa nyakati za kinyang'anyiro cha chaguzi. Watu wa aina hii wana haribu sifa za chombo ni vema wakawa wanakamatwa na wakati mwingine kutolewa picha zao kwenye vyombo vya midia ili kujulikana kwa umma.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, mie naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ya kuchangia. Napenda kuongelea kuhusu muda wa kazi. Wafanyakazi kuanza kazi saa 1.30 hadi saa 9.30 ikiwa na maana wanafanya kazi kwa saa nane. Ukweli ni kuwa, Wafanyakazi hawa hawafanyi kazi kwa saa nane bali hufanya kazi kwa saa sita au chini ya hapo. Hii ni kwa sababu katika saa nane hizi mfanyakazi hutumia dakika 30 kupata chai, saa moja kupata chakula cha mchana, pia wengi hufika kazini saa mbili hadi saa tatu asibuhi kwa sababu ya matatizo ya usafiri. Pia wafanyakazi wengi huondoka kazini saa tisa kuwahi usafiri. Hivyo, kusema kweli wafanyakazi wetu hufanya kazi kwa saa tano tu, sasa nchi itaendelea kwa mtindo huu kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri saa za kazi ziwe kama ifuatavyo: Kufika kazini saa 2 asubuhi; Kufanya kazi saa 2 hadi saa 4.30; Kupata chai saa 4.30 hadi 4.45; Kufanya kazi saa 4.45 hadi saa 7.15; Chakula cha mchana saa 7.15 hadi saa 8.00; na kufanya kazi saa 8.00 hadi saa 11.00.

Tukifanya kazi hiyo, itasaidia wafanyakazi kufika kazini bila kuchelewa, watumia muda wao katika kupata chai na chakula na Serikali haitalipia muda watafanya kazi kwa saa nane.

Hii inawezekana kwani sekta binafsi hutumia mtindo huu na hakuna matatizo yoyote. Kitendo cha Wafanyakazi wa Serikali kuwa kazini kwa saa nane tu na kutumia

huo muda kunywa chai na chakula ni kuiibia Serikali pesa nyingi, kwani Serikali inawalipa saa hizo wakati hawakufanya kazi. Fikiria kama kila siku wafanyakazi huiibia Serikali saa mbili; hivi kweli nchi itaendelea?

Mheshimiwa Spika, tuache kuwaonea aibu mafisadi nchi itakufa, mtu akikosa ashughulikiwe kwa kufuata sheria za nchi bila woga wowote. Tusipofanya maamuzi mazuri kuhusu ufisadi wa *Richmond* na *EPA*, nchi itaingia katika matatizo wakubwa sana siku zijazo. Serikali ishughulikie suala hili kwa uangalifu sana.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilipata fursa ya kuchangia, lakini kwa kuwa muda haukutosheleza napenda kuongezea katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, moja ni TAKUKURU, yapo mafanikio na upungufu kadhalika katika Taasisi hii. Napenda kuiomba Taasisi hii ijitazame kwa nini kesi zinazopelekwa Mahakamani watuhumiwa wanaachiwa huru. Katika Jedwali Na.1 kesi zilizotolewa uamuzi ni 75, walioachiwa huru na Mahakama 47 ni zaidi ya nusu; tatizo liko wapi wataalam wapelelezi au Mahakama, lakini Mahakama huamua kutokana na ushahidi unaowasilishwa mahakamani? Tunahitaji umakini sana kuhakikisha kesi nyingi tuhuma zithibitishwe vinginevyo, kwa mtiririko uliopo katika Jedwali, haionyeshi tija ambayo wananchi walitaraji toka TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni *TASAF*, sina malalamiko yoyote na ufanisi na utendaji kazi wa. Napenda kukumbusha tu kwamba, Wilaya ya Mpanda inazo Halmashauri mbili; Halmashauri ya Mji wa Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, lakini mgao unaopelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ni vyema sasa ugawanywe kwa Halmashauri zote mbili, kila moja kwa kile kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, ambayo ameiwasilisha vyema. Naomba nichangie katika suala la upatikanaji wa watumishi wa umma hasa katika Halmashauri hususan ya Namtumbo.

Sisi Halmashauri ya Namtumbo tumekuwa tukiomba kibali cha kuajiri katika Idara zilizo na upungufu tunaambiwa kutoa vithibitisho. Sisi ni Halmashauri mpya; sasa inakuwaje au tunatoaje uthibitisho wa ukosefu wa nafasi tunazoomba wakati sisi ndio tunaanza?

Naomba Serikali ituchukulie kama Halmashauri inayohitaji kipaumbele katika kuajiri watumishi ili tuweze kufanya kazi na kutimiza haja ya matumaini ya Utawala Bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa *TASAF* zinacheleweshwa kupelekwa kwenye Wilaya hasa Chunya, ambako miradi kadhaa imeibuliwa lakini bado haijapata fedha husika. Nashauri jitihada ziongezwe kuharakisha kupeleka fedha Mawilayani.

Mheshimiwa Spika, nashauri utaratibu wa kufanyiwa *Vetting* kwa watumishi wanaoshughulikia nyaraka za siri kwa lengo la kutambua uaminifu na uadilifu wao kabla hawajapangiwa kazi hiyo.

Malipo ya Pensheni yaongezwe hasa kwa wastaafu wa zamani wananyanyasika sana.

Watumishi wa Umma kujiingiza kwenye siasa ni sahihi?

Watumishi kukaa sehemu moja kwa muda mrefu; sehemu nyingine zaidi ya miaka 20; je, wale viongozi wanaoshindwa kurejesha fomu na wale wanaodanganya katika ku-*declare* mali zao hatua zipi zinachukuliwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, rushwa itakwisha ama itapungua sana kama wafanyakazi watalipwa mishahara inayolingana na hali halisi ya gharama za maisha ili waepukane na vishawishi vya rushwa na kuona kuwa wakipoteza ajira nzuri kwa rushwa ni sawa na kupata hasara kubwa.

Mwaka 1974 nilipoanza kazi kama Afisa Tawala Serikalini mshahara nilioanza nao ulikuwa Sh. 1,200. Mwezi wa kwanza wa kupokea mshahara nilinunua kitanda na godoro Sh. 150, seti ya makochi Sh. 450, kabati Sh. 100 nikabakia na Sh. 500, ambazo nazo sikuweza kuzimaliza kwa chakula na nguo. Nilitumia Sh. 300 nikabakiwa na akiba ya Sh. 200 mwisho wa mwezi. Kulikuwa hakuna rushwa kwenye *civil service*. Naishauri Serikali ivunje *vicious cycle* hii ya rushwa kwa kuajiri watumishi wachache kulingana na mahitaji na kuwalipa vizuri.

Serikali iketi na wahisani watusaidie ili tuondokane na rushwa na kuimarisha Utawala Bora. Tunaposema tunapunguza utegemezi kutoka 42% hadi 34% wakati hata mishahara tunashindwa kulipa vizuri kulingana na gharama za maisha hatuwi *realistic*. Tutaendelea kufuja fedha zetu za ndani na nje kwa njia zisizo halali na wizi ili wafanyakazi waweze kuishi vizuri kama wafanyakazi wa Mataifa mengine. Napendekeza kima cha chini kitoke Sh. 100,000 kwenda Sh. 500,000 kwa mwezi. Nchi tajiri marafiki zitusaidie kwenye hili tuondokane na ufukara wa watumishi wetu.

Dunia sasa imebadilika, kuendelea kwetu kusingizia wakoloni au Nchi za Magharibi zina lengo la kututawala kinyemela kupitia misaada yao si halisi. Waafirika sasa wanapewa fursa ya kujiamulia mambo yao kuliko wakati mwingi wowote,

kukubalika kwa waafrika kama Barack Obama, Nelson Mandela na kubuka kwa wimbi la Mameya weusi Amerika na Wawakilishi weusi Uingereza na ufaransa ni ishara tosha kwamba, dunia sasa ni *one big village*. Wenzetu matajiri waombwe watusaidie kwa kulipia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mbinu zake za kuomba misaada kutoka nchi mbalimbali marafiki na nchi yetu sasa haina maadui wavamizi. Rais atumie mbinu hizo hizo kuliangalia tatizo la mishahara ya wafanyakazi ili kukabiliana na hali ngumu ya maisha. Hatuwezi kuimarisha Utawala Bora wakati watu wanapata kipato duni. Hata hivyo, pamoja na maoni ya hapo juu, naipongeza Wizara hii na Serikali kwa jumla, kwa nyongeza ya mishahara ya kufikia hadi asilimia 30 kuwa ni hatua nzuri ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwenye eneo hili.

Naipongeza *TASAF* kwa kazi nzuri Manyoni na pia hatua za MKURABITA katika kuanza kurasimisha ardhi vijijini ili wananchi waweze kukopa kwenye mabenki.

Tume ya Bei ijizatiti kuja na mkakati wa mgawanyo mzuri wa Rasilimali za Taifa na kukabili mfumko wa bei.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga hoja mkono.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu muhimu ambayo ningependa kuizungumzia ni Mipango. Tumepata Uhuru kwa kumbukumbu zangu tumekuwa tukiwa na Wizara ya Mipango. Katika kupunguza baraza la Mawaziri; Wizara ya Mipango imeondolewa na kuundiwa Tume ya Mipango. Mipango ni dira ya utekelezaji. Bila ya kuwa na Mipango imara na inayoandaliwa kikamilifu utekelezaji unakuwa bora.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Serikali iangalie upya suala hili la Wizara ya Mipango. Ni kweli Wizara hii inaweza kuwa Wizara ya Nchi chini ya Rais au Makamu wa Rais, lakini ni vyema Wizara hii ikawepo na iwe ina Waziri wake na wataalam ili tuwe na uhakika na Mipango endelevu na itakayokuwa ndiyo elekezi ya utendaji wote wa Serikali hasa katika Uchumi Endelevu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ningependa kuliongelea ni Idara ya Usalama wa Taifa. Ili nchi iwe salama na utulivu wa kisiasa na kiutawala, chombo hiki ni muhimu kiwe imara. Chombo hiki hakiwezi kuwa imara kama hakitawezeshwa kifedha katika utendaji kazi wake. Naisihi Serikali iangalie kila njia ili iweze kukitengea chombo chetu cha Usalama wa Taifa letu, fedha za kutosha ili utendaji uwe bora kwani bila ya fedha za kutosha chombo hiki kitakosa nguvu stahiki, wakati kazi inayofanywa na chombo hiki umuhimu wake ni sawa na jeshi la nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu mdogo, naunga mkono hoja.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, naipongeze hotuba hii nzuri, yenye kulenga maendeleo ya Mtanzania.

Mishahara ya watumishi ni kweli imeongezwa na ni kweli hali ya uchumi wa nchi yetu ni ndogo lakini hali ya maisha imepanda bila ya mpangilio, kila mfanyabiashara anauza anavyoona inafaa tu; kitengo kinachodhibiti bei kiko wapi? Hata kama mafuta yamepanda lakini chakula kimepanda mno bei haina kidhibiti.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa kipato cha chini ni ukweli usiopingika wanaumia sana na hali ya maisha na wengine wasio na mradi mbadala wa kuwaongezea kipato huwa hawawezi hata kusomesha watoto, hebu tuangalie upya kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, Mtumishi kama askari kukaa sehemu moja kwa muda mrefu wakati mwingine haipendezi, lakini askari wetu hawa wanapohamishwa hupewa posho ya uhamisho huo baada ya kuhama. Huo ndio Utawala Bora? Huu sio Utawala Bora, tuwajali wafanyakazi wetu. Baadhi ya wafanyakazi wanapostaafu huwa ni kero kwani wengine huwa wanafika miaka minne na kuendelea, hawajapewa kiinua mgongo chao; hivi huu ndio Utawala Bora au ni kumnyanyasa huyu Mtanzania aliyeitumikia nchi yake kwa uzalendo mkubwa?

Mheshimiwa Spika, naipongeze sana Serikali kwa Mradi huu wa *TASAF*, kule Zanzibar umefanikiwa sana. Naomba Mradi huu uendelee kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie mambo mawili tu; kwanza, usalama wa Taifa na pili, Jamii ya Wavuvi wanaovua Bahari ya Hindi

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa wapo kwa ajili ya usalama wa watu wote wa Tanzania, lakini kwa masikitiko makubwa, Usalama wa Taifa wa nchi yetu wakati wa uchaguzi wao wanakuwa mbele kuhakikisha Chama Tawala kinashinda kwa njia yoyote. Wao ndio wanaoongoza kwa kupiga propaganda za kuwadanganya wananchi kuwa msikichague chama fulani kama wao ndio kazi yao.

Mheshimiwa Spika, ninao ushahidi; Usalama wa Taifa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2000 walipita Vituo vyote vya Uchaguzi Pemba na walikuwa wakichukua matokeo ya Rais tu. Baada ya kuona hali ni mbaya kwa Chama Tawala, wakatoa taarifa na baadaye kura zote zikachukuliwa na polisi kwa bunduki zikapelekwa Wilayani kwa muda wa wiki nzima. Matokeo yake walibadilisha matokeo na kupatiwa ushindi watu waliokuwa hawakushinda Majimbo ya Wawi, Vitongoji, Kiwani, Mkanyageni na

Mkoani. Nina uhakika na hili. Usalama wa Taifa, wafanye kazi zao kwa mujibu walivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni la Utawala Bora ambalo linahusu Wavuvi wa Bahari ya Hindi, wanaozuiliwa na Serikali kuvulia nyavu za *ring net*, kuzama kwa kutumia vioo au *champion*, kuogelea kwa viatu na kutumia gesi ya *Oxygen* wakati wa kuzama.

Mheshimiwa Spika, swala hili linawaumiza sana wananchi wetu, kwani Serikali imepiga marufuku uvuvi huu bila hata kuwashirikisha wavuvi wenyewe. Wamewaandikia tu kuwa waliwaita wakazungumza nao na wakakubaliana nao. Utawala Bora haukuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tayari wananchi wetu wameshaanza kuchukuliwa nyavu zao na wengine wameshapigwa na madhara mengi yanaendelea. Hivyo basi, ninakuomba Waziri wa Utawala Bora, ulifuatilie suala hili kwa wanaohusika ambao ni Serikali na wavuvi.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kunijalia uzima na kuchangia Hutoba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Manajimenti ya Utumishi wa Umma. Nampongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii iliyojitosheleza, nina mchango mdogo sana kuhusu MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nimepata bahati ya kutembelea Miradi hii huko Bagamoyo. Kwa kweli Mradi huu ni mzuri na ni ukombozi kwa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili ni zuri, ninaishauri Serikali kwa kuwa suala hili ni la Muungano, lingefanya kazi kama Mradi wa *TASAF*, kwa sababu umeenea Tanzania nzima. MKURABITA umejikita zaidi Tanzania Bara napo ni maeneo machache tu. Kwa hiyo, MKURABITA uenee maeneo yote kwani matatizo yapo mengi ya ardhi, migogoro haishi baina ya wafugaji na wakulima na dawa yake ni MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa maboresho mbalimbali katika utumishi wa umma. Napenda kuishauri Serikali iongeze pesa za kuboresha shughuli

nzuri inayofanywa na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABIRA).

Mheshiwa spika, kwa kuwa Watanzania wengi ni maskini wanyonge, hivyo, kama Serikali itaongeza fedha katika Mpango huu, basi na Watanzania wengi watakuwa na uwezo wa kufanya biashara rasmi na kuongeza kipato. Watanzania wengi watakuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Serikali, naomba ziboreshwe maana baadhi yake hazifanyi kazi vizuri na wengine wanafanya kazi vizuri. Naomba tupewe taarifa za kiushindani juu ya utendaji wa wakala wa watumishi mbalimbali wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Waziri/Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumisi wa Umma, pamoja na Wataalam wao, kwa kuandaa *speech* nzuri. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado rushwa ni tatizo kubwa. Kwa maoni yangu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa haijafanya kazi yake ipasavyo. Tatizo kubwa ni kwamba, hata viongozi wenyewe wa taasisi hujihusisha kwa namna mbalimbali kwenye vitendo vya rushwa. Kwa mfano, maafisa wa taasisi kuwalinda baadhi ya watoa na wapokea rushwa. Hali hii hujitokeza sana kwenye matukio kama vile uchaguzi na kadhalika. Baya zaidi, viongozi wa taasisi hujihusisha zaidi na rushwa ndogo ndogo (*Petty Corruption*), wakiacha rushwa kubwa kubwa (*Grand Corruption*). Hili halifanyiki kwa bahati mbaya ila ni kwa makusudi, kwani hata viongozi wengi wa taasisi ni wadau wakubwa wa rushwa hiyo (rushwa kubwa).

Nashauri kitengo/taasisi ijielekeze zaidi kupambana na rushwa kubwa, huko ndiko pesa nyingi zaidi za Serikali hupotea. Viongozi wa Taasisi watimize wajibu wao kikamilifu kwa kuisimamia Sheria ya Kupambana na Rushwa. Aidha, Viongozi wa Taasisi waone aibu ya kuendelea kupigiwa kelele kila siku kwa kutotimiza wajibu wao vizuri. Elimu iendeleo kutolewa kwa wananchi wote, juu ya madhara ya rushwa kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, baadhi ya viongozi wakubwa katika utumishi wa nchi hutoa taarifa ambazo siyo sahihi sana kuhusu mali walizonazo na jinsi walivyopata. Hii inatokana na ukweli kwamba, viongozi wengi Serikalini hutuhumiwa kwa vitendo vya ufisadi na kuwa na mali nyingi kuliko vipato vyao halali. Wakati huo huo, hakuna namna iliyo wazi kabisa ya kupitia fomu zao zinazotaja mali. Taratibu za kuchunguza fomu zenyewe siyo nzuri/siyo wazi hata kidogo!

Nashauri Sheria ya Maadili ya Viongozi hasa kuhusu kutaja mali zao, irekebishwe ili iwe ya uwazi zaidi. Aidha, viongozi wataje mali zao hadharani, wanapoingia madarakani na wanapotoka. Sheria pia iwe na vifungu vitakavyotoa adhabu kali kwa

wale wote watakaobainika kutoa taarifa za uongo na mali ambazo zitaonekana hazikutajwa kwenye fomu za kutaja mali basi zitaifishwe.

Mheshimiwa Spika, pensheni kwa wastaafu bado ni ndogo sana, kwa mtu ambaye umelitumikia Taifa lake kwa uadilifu mkubwa na kwa miaka mingi. Nashauri Serikali iongeze kima cha sasa kutoka Sh. 21,000 walau hadi Sh. 50,000 na kiwango hicho kiendelee kuongezwa kadiri hali ya uchumi itakavyokuwa inakua.

Mheshimiwa Spika, bado mshahara wa kima cha chini wa Sh. 100,000 kuanzia Januari, 2008 ni mdogo sana; kwa mfano, bajeti ndogo tu kwa mwezi ni kama ifuatavyo: Kodi ya nyumba/vyumba viwili kwa mwezi Sh. 30,000; nauli ya kwenda na kurudi kazini Sh. $300 \times 2 \times 22$ siku = Sh. 13,200; Chakula (chai) Sh. $500 \times \text{watu } 5 \text{ wastani} \times \text{siku } 30$ = Sh. 75,000; Chakula mchana Sh. $1000 \times 5 \times 30 \times 2$ (milo) = Sh. 300,000 = Sh. 375,000.

Gharama za maji na umeme; umeme Sh. 10,000; Maji Sh. 6,000.
Nauli za watoto kwenda shule Sh. $100 \times 2 \times 2$ watoto $\times 22$ siku Sh. 8,800.

Matibabu wastani wa Sh. 10,000 kwa mwezi Sh. 10,000.

Matumizi mengineyo Sh. 10,000 kwa mwezi = Sh. 10,000.

Mheshimiwa Spika, jumla ya matumizi yote ni Sh. 463,000.

Bajeti ndogo ya familia ya kimaskini kabisa inafika Sh. 463,000. Serikali inategemea familia hii inaishije? Nawashauri Serikali ifanye jitihada za kuongeza mshahara zaidi hasa wa kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mshahara kwa watumishi wa ngazi za juu ni kubwa sana. Kwa mfano, mtu anayepata mshahara kati ya Sh. 4,320,000 hadi Sh. 6,480,000, kodi yake ni Sh. 468,000 + asilimia ya pesa ya ziada ya Sh. 4,320,000. Kwa mfano, mtu anayelipwa Sh. 5,000,000 atakatwa Sh. $468,000 + 136,000 = 604,000$; hii ni kodi! Inakatisha tamaa. Nashauri Serikali iangalie upya viwango vya kodi kwenye mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa ni wakati ambapo Mawaziri wawili ambao muda wao ni saa moja na dakika kumi na tano, wamegawana, mmoja dakika 35 na mwingine dakika 40 kuanza kufanya majumuisho.

Kabla ya kumwita mtoa hoja, nadhani nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba, karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa baadhi ya majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa baada ya hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais kuwasilishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Waziri Mwenzangu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa hotuba iliyowasilishwa hapa Bungeni. Naomba pia kuipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa ushauri, mawazo na maelekezo iliyotoa ambayo yametusaidia kujenga mwelekeo mzuri katika mpango wetu wa kazi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mawazo, michango yao na ushauri waliotupa, kwa njia ya maandishi na kusema ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika naomba sasa nijibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naomba nijibu hoja zilizolenga hasa Ikulu, Utawala Bora, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango, *TASAF* na *MKURABITA*.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niruhusu nijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni, katika kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, tuhuma nzito za rushwa ikiwemo ile ya Richmond na malipo ya Akaunti ya *EPA*, Benki Kuu kwamba Serikali haijachukua hatua za kuwafikisha wahusika Mahakamani na kwamba ni kipimo tosha kwamba nchi yetu haina utawala Bora, ukweli ni kwamba tuhuma ya Richmond kama alivyotoa ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiyo msimamo wa Serikali kwamba mapendekezo haya yanafanyiwa kazi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, atayatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma za *EPA*, hili nalo limetolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, bado inaendelea na uchunguzi wake na kwamba tuwe na subira hadi hapo taarifa ya Tume itakapowasilishwa rasmi kwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba kuna ubaguzi katika kuwashughulikia watuhumiwa wa tuhuma za rushwa na kwamba walalahoi mara wanapotuhumiwa hukamatwa na kupelekwa rumande na Mahakamani, lakini kwa vigogo wenye kutuhumiwa kwa mabilioni, mambo ni tofauti kabisa. Hii si kweli, ukweli ni kwamba sheria haibagui wala kuweka makundi ya walalahoi na vigogo. Rushwa ndogo au rushwa kubwa yote ni makosa machoni mwa sheria. Tofauti ya rushwa ndogo na rushwa kubwa ni kwamba penye rushwa ndogo ushahidi ni wa hapo hapo na hauchukui muda kwa kuwa unapatikana katika sehemu ya tukio. Mfano mkubwa ambao umekuwa ukitolewa, ni mwizi wa kuku, ushahidi ni yule kuku, tofauti na rushwa kubwa, ushahidi wake huchukua muda na huhitaji kuupata ushahidi mwingine unaokuwa nje ya mipaka ya nchi na kupelekea kazi hiyo kuchukua muda mrefu kinyume na ushahidi wa rushwa ndogo.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge, ni vema tukatambua kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa sana katika mapambano dhidi ya rushwa. Hatua hizi ni pamoja ya kuwa nchi ya kwanza duniani kutunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inayozingatia misingi ya Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Rushwa (*United Nation Convention Against Corruption*) ya mwaka 2003 ambayo inaiwezesha TAKUKURU kushirikiana na taasisi za nje katika kuchunguza na kukusanya ushahidi unaokuwa nje ya mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, suala lingine la Kambi ya Upinzani, ni kuhusu Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wake kwa Tanzania (*NACSAP*). Napenda kujibu hoja hii pamoja na swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama aliyetaka kujua utekelezaji wa *NACSAP I*. Serikali inatambua tatizo la rushwa na madhara yake katika Taifa na ndiyo maana ikachukua hatua ya kuandaa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Tanzania (*NACSAP*) ambao kwa sasa upo katika awamu ya pili ya utekelezaji, kwa kifupi ni *NACSAP II*.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa ya mwaka 1999 – 2005, mkakati huu ulilenga yafuatayo:-

- Mabadiliko katika utoaji huduma kwa wananchi ndani ya Serikali na kuongeza uadilifu na nidhamu katika matumizi ya fedha na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma;

- Kuongeza uelewa wa umma juu ya dhana ya rushwa na ushiriki wao katika mapambano dhidi ya rushwa; na

- Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika shughuli za Serikali, kushirikisha asasi zisizokuwa za Kiserikali na sekta binafsi katika mapambano dhidi ya rushwa, kusisitiza na kudumisha utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya mkakati ambao ni mwaka 2006 – 2010, imelenga yafuatayo:-

- Kuongeza uwigo wa kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na. 11 ya mwaka 2007, kwa mfano ni matokeo ya utekelezaji wa kipengele hiki;

- Kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

- Kuziongezea nguvu za kisheria taasisi zinazosimamia masuala ya rushwa na utawala bora (*watchdog institutions*), vyombo hivyo ni TAKUKURU, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, Tume ya Haki za binadamu na Utawala Bora;

- Kushirikisha sekta binafsi, taasisi za kiraia na vyombo vya habari katika mapambano dhidi ya rushwa;

- Kuongeza uelewa wa umma kuhusiana na rushwa; na
- Kuhimiza na kusimamia uwazi, uadilifu, uwajibikaji kama nguzo muhimu katika kuzuia kupambana na rushwa pamoja na kukuza utawala bora nchini.

Mheshimiwa Spika, hili limetekelezwa kwa kuanzisha Kamati za Maadili katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Serikali pia imeboresha ushirikano wake na Mataifa mengine kupitia kusaini kwake Mikataba ya Kimataifa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, jambo linaloweza taasisi zenye dhamana hiyo nchini kama vile TAKUKURU kushirikiana na taasisi za nje katika uchunguzi na vitendo vya rushwa vilivyofanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango mahususi iliyowekwa na Serikali ili kukabiliana na wala rushwa, tunatarajia kufanya yafuatayo, nitataja baadhi yake tu.

- Kuendelea kuchunguza rushwa kubwa na ndogo kama ilivyoainishwa katika mpango mkakati wa TAKUKURU sambamba na mkakati wa Kitaifa wa mapambano dhidi ya rushwa na utekelezaji wa awamu ya pili wa *NACSAP II*.

- TAKUKURU kwa mwaka 2007/2008, inachungaza kesi kubwa 10.

- Aidha, sheria haichagui rushwa ndogo au kubwa tofauti na dhana iliyojitokeza miongoni mwa baadhi ya wadau kwamba inashughulikia rushwa ndogo tu na kuacha rushwa kubwa.

Ningependa pia kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na.11 ya 2007, ina mwaka mmoja tu tangu ianze kutumika yaani kuanzia tarehe 1 Julai, 2007. Hivyo ni matarajio yetu kuwa Sheria hii itaendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi yanayotolewa kwamba TAKUKURU haifanyi kazi yao vizuri, ni kutokana na kutofahamu ukweli kwamba tuhuma zote zinazolalamikiwa kutofanyiwa kazi vizuri ni kwamba matukio ya tuhuma hizo yalitokea kabla ya Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuanza kutumika rasmi Julai 2007. Kwa maana hii, tuhuma zote zinazolalamikiwa, zimechunguzwa kwa Sheria ya zamani yaani Sheria Na.16 ya mwaka 1971. Sheria hiyo ya zamani ina upungufu mwingi, ina makosa manne tu ya rushwa hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba ili wananchi waweze kushiriki vyema katika kuzuia na kupambana na rushwa, inabidi waelimishwe na kuhusishwa vya kutosha juu ya suala zima la mapambano dhidi ya rushwa. Hivyo, kwa kutekeleza jukumu hilo, TAKUKURU itaendelea kuelimisha jamii kwenye ngazi zote kuanzia kata hadi kijiji.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na mwamko huo, ndiyo maana vyombo vya habari vinafanya kazi hiyo na kuweka agenda ya rushwa kuwa ni ya kudumu na hayo ndiyo mafanikio makubwa ya Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa Nchini (*NACSAP*).

Mheshimiwa Spika, tafiti 28 za TAKUKURU zilizofanyika na zile zitakazoendelea kufanyika ili kuziba mianya ya rushwa, ni kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa chini ya Kifungu Na. 7(a) cha Sheria hiyo. Kifungu hicho kimeielezea TAKUKURU kufanya utafiti huo ili kuziba mianya ya rushwa katika sekta za umma, sekta binafsi na sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwamba TAKUKURU inapata kigugumizi kuwapeleka Mahakamani wahusika wa tuhuma za rushwa katika manunuzi ya rada baada ya mtuhumiwa aliyepokea dola milioni 12 kukiri kuweka fedha hizo katika akaunti yake Uswisi na kwamba Serikali ilimwachia huru na kumpa *Passport* yake baada ya kutoa kiapo mbele ya Mahakama Kisutu, imewafanya wananchi wengi kupoteza imani na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, hoja hii haina ukweli hata kidogo. Bunge hili pamoja na Kambi ya Upinzani, lilitunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, chini ya Kifungu cha 37, Bunge hili liliweka utaratibu wa kuizuia TAKUKURU kutamka na kuelezea uchunguzi wowote unaoendelea kwa raia au mtu yeyote na kuwa ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, ni kwa mantiki hii na kwa kuzingatia utawala wa sheria na utawala bora, TAKUKURU isingezungumzia jambo lolote linaloendelea kuchunguzwa. Uchunguzi wa kesi ya Rada, unakamilishwa na taarifa itatolewa mara baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai, anapopitia ushahidi wote na kutoa maelekezo yake.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba kwa nini kesi kubwa huchukua muda mrefu, TAKUKURU hufuata taratibu za Kimataifa za kupata nyaraka na mashahidi walioko nje ya nchi. Utaratibu huu si kwa TAKUKURU peke yake bali ni kwa vyombo vyote vya dola vinapohitajika kupata ushahidi wa kutosha ili kuthibitisha kosa la rushwa au kosa la jinai. Kwa mantiki hii, Waheshimiwa Wabunge, watambue kazi hii huchukua muda na si kwamba TAKUKURU imezembea au inakumbatia mafisadi. Ushahidi unaendelea kufuatiliwa na nchi husika zinatoa ushirikiano wake na nchi hizo pia huhitaji kujiridhisha kwamba taratibu zao za kisheria kuhusu jambo hilo limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge kwa maandishi na kwa kuongea. Hoja zilikuwa nyingi sana hasa za maandishi, kwa hiyo, nyingine tutawapelekea majibu yao kwa maandishi kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, nianze na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, *CHADEMA*, alitaka kujua ni kwa nini mwaka hadi mwaka tunatenga fedha nyingi kwa ukarabati wa Ikulu. Pia alitaka makisio halisi ya ukarabati hadi utakapokamilika ni shilingi ngapi na ukarabati utakamilika lini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu kinachotumika kwenye miradi ya maendeleo kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu, kinahusisha ukarabati wa jengo la Ikulu lenyewe na Ikulu ndogo 10 zilizoko Mikoani ambazo ni Arusha, Moshi, Lushoto, Nachingwea, Mwanza, Tanga, Shinyanga, Tabora, Dodoma Mjini na Chamwino. Kabla ya ukarabati wa jengo la

Ikulu, jengo hili pamoja na majengo mengine, yalikuwa kwenye hali mbaya. Ili kuyaweka majengo hayo katika hali nzuri, yanahitaji matengenezo makubwa, ambayo gharama zake ni kubwa pia.

Aidha, majengo yaliyofanyiwa ukarabati ili yaendeleo kuwa katika hali nzuri, yanahitaji matengenezo (*preventive maintenance*) ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya ukarabati wa jengo la Ikulu, ilianza mwaka 1999 mpaka 2000 na ilikamilika katika mwaka wa fedha 2004/2005. Ukarabati huu, ulihusisha jengo kuu la Ikulu ya Dar es Salaam.

Awamu ya pili ya ukarabati wa Ikulu, ilianza mwaka wa fedha 2005/2006 na kazi zilizohusika, ni ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais, ununuzi wa samani kwa nyumba hiyo, ukarabati wa jengo la Sekretarieti la Baraza la Mawaziri, jengo la ofisi la mawasiliano, nyumba ya makazi ya Katibu Mkuu Kiongozi, ukarabati wa Ikulu ndogo Chamwino na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, kiasi cha shilingi bilioni 5.712 zimetengwa kwa ukarabati wa Ikulu kwa ajili ya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Ikulu Ndogo Dodoma Mjini ili kumwezesha Mheshimiwa Rais kuwa na Ofisi Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni kama ifuatavyo:-

- Uwekaji wa mitambo ya usalama, CCTV awamu ya pili;
- Uimarishaji wa lango kuu la ukaguzi wa magari
- Ukarabati wa Ikulu wa Chamwino;
- Ujenzi wa Ikulu Ndogo Dodoma;
- Ukarabati wa zahanati;
- Ujenzi wa jengo la ofisi ya uhasibu;
- Matengenezo madogo madogo ya Ikulu; na
- Ukarabati wa mitambo ya kupozea maji (*Chillers*).

Mheshimiwa Spika, swali linalofuata ni swali la Mheshimiwa Khadija Salum Al-Quassmy, Mbunge Viti Maalum, yeye anasema utawala bora Tanzania bado uko nyuma, maneno ni mengi kuliko vitendo. Napenda nimfahamishe kwamba, Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti ili kujenga na kuimarisha utawala bora nchini. Baadhi ya hatua ambazo zimechukuliwa ili kuleta uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria na kudhibiti rushwa, nitampatia kutokana na muda ulivyo finyu.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma. Yeye anasema kuna matatizo makubwa ndani ya TAKUKURU ambapo Tume Maalumu imeundwa kufuatilia watumishi wa TAKUKURU. Tuhuma za Mheshimiwa Zitto Kabwe, tunazipokea na tutazifanyia kazi.

Aidha, wapo watumishi wachache ambao wamejihusisha na uvujaji wa siri za ofisi, tayari hatua zimechukuliwa kwa mujibu wa sheria na kesi zote zinafuatiliwa. Takwimu zinathibitisha kazi nzuri inayofanywa. Nina takwimu ambazo nitampatia Mheshimiwa Zitto, kuonyesha kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, pia amesema kuwa kuna mgogoro mkubwa kwenye uongozi wa juu wa TAKUKURU, Serikali ina maelezo gani? Serikali haina taarifa ya kuwepo mgogoro wa uongozi ndani ya TAKUKURU. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge Zitto, ametoa hoja ya kuwepo kwa mgogoro, ni vema aziwasilishe taarifa hizo na ushahidi ili Serikali izifanyie kazi.

Pia Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, yeye alitaka kujua Serikali imechukua hatua gani juu ya rushwa ya uchaguzi. Matarajio ni kwamba TAKUKURU ingeratibu zoezi hilo katika kazi zilizopangwa katika mwaka 2008/2009. Yeye ameona kuwa suala hilo halipo. Suala hili pia limezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, ambaye naye ameulizia kuhusu rushwa ya uchaguzi, ni lini itatiwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwajibu maswali yao kwa pamoja. Serikali imeunda Kamati ya Utendaji (*Steering Committee*) ya NACSAP na moja ya jukumu lake, ni kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya sheria kuhusiana na kipengele cha rushwa wakati wa uchaguzi na mchakato huo utashirikisha vyama vya siasa na wadau wengine watahusishwa rasmi kuanzia mwezi Oktoba 2008 baada ya maandalizi yote kumalizika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Masilingi, tumeupokea na huo ndiyo umekuwa msingi wa utendaji kazi kila siku kuhakikisha haki inatendeka kwa mujibu wa sheria. Alitushauri kwamba TAKUKURU ichukue muda mrefu lakini ihakikishe haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, pia alishauri Serikali iongeze magari katika ofisi za Wilaya. Serikali itaendelea kuisaidia TAKUKURU katika suala la vitendea kazi kwa kadri ya uwezo wa bajeti.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, alishauri kwamba TAKUKURU ipewe uwezo wa kuangalia Miswada na Sheria kama ina mianya ya rushwa. TAKUKURU itaweka kipaumbele kwa pendekezo hili na Idara ya Utafiti, itaendelea kuzingatia ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, aliulizia kuhusu ugawaji wa viwanja katika Jimbo la Kibaha. Alitaka kujua kama TAKUKURU inafahamu au inachukua hatua zozote. Maelezo yake yamepelekwa kwa Kamanda wa TAKUKURU, Mkoa wa Pwani ili afuatilie ukweli wa tuhuma hizo na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, halafu TAKUKURU ifuatilie taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuzifanyia kazi hususan kwenye suala la *value for money*, ushauri huo pia tumeupokea.

Mheshimiwa Feteah Mgeni, alishauri TAKUKURU ishughulikie zaidi suala la kuelimisha umma. TAKUKURU imekuwa ikitoa elimu ya umma kuhusiana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Madhara ya Rushwa katika jamii na kwamba imeweza kufikia hadi katika baadhi ya shule na kuanzisha vilabu vya wapinga rushwa mashuleni katika Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, alihoji Maafisa wa TAKUKURU, Wilaya, kujenga urafiki na Maafisa ambao wanalalamikiwa na wananchi kuhusu rushwa hususan katika Idara ya Polisi. Ushauri wake, tumeupokea na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, atalifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, maswali ya TAKUKURU ni mengi lakini tutaendelea kuwajibu kwa maandishi. Kuna swali lingine lilitolewa na Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni, yeye anazungumzia tatizo la viwanja vya ufukweni mwa bahari ya Hindi na wenye mahoteli kutofuata Sheria za Ardhi, TAKUKURU ishughulikie kero hiyo. Napenda kumtaarifa Mheshimiwa Mbunge kuwa taarifa hiyo imepokelewa na TAKUKURU itawasiliana naye ili kupata taarifa za kina.

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia masuala ya chombo chetu cha Usalama wa Taifa. Mheshimiwa Zitto Kabwe, amezungumzia kuhusu vipengele vya Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996, ambayo inaifanya Idara kuwa butu, ameshauri kuwe ma mabadiliko ya Sheria na sisi tunasema tunachukua ushauri wake.

Hata hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mgawanyo wa majukumu baina ya vyombo mbalimbali vya dola, unatoa madaraka ya kuwakamata na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Kijiko, yeye alisema kwamba viongozi wa Usalama wa Taifa, hawana vyombo vya usafiri ambavyo vinastahili. Serikali inalichukua hilo na pale ambapo itawezekena, magari yao yataboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Killimbah naye pia alizungumzia Idara ya Usalama wa Taifa kuwa nyeti kwa Taifa hivyo watumishi wake wawe na upeo. Katika kuhakikisha watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa, wanaendelea kutekeleza wajibu wao kulingana na mabadiliko na mbinu mbalimbali zinazotokea katika jamii, Idara imeendelea kutoa mafunzo ya kazi na ya kitalaamu ndani na nje ya nchi, ya kujikumbusha na yale yanayolenga kutoa mbinu mpya kwa watumishi wake.

Aidha, pia alisema uadilifu wa watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa, Mikoani na Wilayani, unatia shaka. Kuhusu watumishi wa idara wanaotuhumiwa kutoa siri,

kushirikiana na wahalifu na kujiingiza katika ushabiki wa kisiasa, Serikali imeyapokea maoni hayo na inapenda kutoa kauli kwamba watumishi wanaofanya hivyo wanavunja sheria na kanuni za utumishi. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge, tuwasiliane ili kupata orodha ya watumishi hao kama itathibitika, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anna Kilango Malecela na yeye pia ametoa ushauri wa kuimarisha chombo chetu cha Usalama wa Taifa. Jibu lake ni kwamba Idara ya Usalama wa Taifa, inatengewa fedha kulingana na uwezo wa Serikali kiuchumi. Hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kuiwezesha kutekeleza wajibu wake. Tunashukuru kwa kutukumbusha hilo na Serikali ni sikivu.

Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, yeye amezungumzia watumishi wastaafu wa Idara ya Usalama wa Taifa kutolipwa pensheni. Ninapenda kumjibu kwamba kabla ya kuunganishwa na Idara ya Usalama wa Taifa Tanzania Bara na Visiwani, watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa, Zanzibar walikuwa wanalipwa pensheni na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, ilipofikia mwaka 1984, vyombo hivyo viliunganishwa na kuwa chombo kimoja. Kwa msingi huo, malipo ya pensheni kwa watumishi wa Zanzibar, kwa kipindi kabla ya mwaka 1984 yalishughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Peter Kimiti na yeye pia alitoa ushauri na rai kwamba vyombo vya Usalama, visaidie Serikali kufanya upekuzi wa watumishi viongozi wenye sifa za kupewa madaraka. Serikali imepokea ushauri huo na jitihada zitaendelea kufanywa ili kuimarisha mchakato wa upekuzi wa watumishi viongozi kabla ya kupewa madaraka na zoezi hili litakuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Richard Ndassa, mwanangu, alitoa *concern* kwamba kwamba sura ya Ikulu imebadilika hasa katika suala zima la usafi. Tunamhakikishia kwamba Ikulu itaendelea kuwa safi na wale wanyama ambao anadhani wamepotea, bado wapo na ninamkaribisha aje, tutamuonyesha wanyama hawa wako wapi. Kutokana na *movement* nyingi za magari, wanyama wanajificha lakini bado wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye maswali yanayohusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hoja ya kwanza ilikuwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ina upungufu na inahitaji marekebisho. Wachangiaji walikuwa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, nijibu kwamba Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeshaanza mchakato wa kuandaa mapendekezo ya kuifanyia marekebisho sheria hii. Mchakato huo ni pamoja na kuangalia taratibu za nchi nyingine kuhusu suala la kutenganisha uongozi wa umma na biashara kwa lengo la kuondoa na kupunguza mgongano wa maslahi ya umma na binafsi. Aidha, mapendekezo ya marekebisho, yatawasilishwa pia kwa wadau mbalimbali kupata maoni yao kabla ya kuwasilishwa Bungeni. Hata hivyo, ni muhimu kwa viongozi wa umma, wawajibike kwa kufuata na

kuzingatia matakwa ya Sheria ya Maadili ya Vviongozi, Na.13 ya mwaka 1995 hadi hapo sheria itakaporekebishwa.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, pia alihoji taarifa za mali na madeni za Waheshimiwa Wabunge, zinarekebishwa katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa mujibu wa Ibara 70(1) ya Katiba, kila Mbunge huwasilisha kwa Mheshimiwa Spika, nakala mbili za tamko la mali na madeni. Nakala moja inabaki Ofisi ya Spika na nyingine huwasilishwa kwa Kamishna wa Maadili. Hakuna marekebisho yoyote ambayo hufanywa na Sekretarieti ya Maadili kwenye fomu za tamko la Mbunge au kiongozi yeyote mwingine zikishapokelewa. Hata hivyo, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, itafanya uchunguzi ya hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ili kupata ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha na yeye pia alizungumzia kama kiongozi anataja mali zaidi ya uwezo wake, kuwe na utaratibu wa kumchunguza. Viongozi wa umma wanatakiwa kutoa tamko la mali na madeni yao pamoja na maelezo jinsi walivyopata mali hizo. Pale ambapo inaonekana mali hizo hazilingani na kipato chao, hutakiwa kutoa maelezo ya ziada kuhusu mali zao. Ikiwa bado maelezo hayaonyeshi jinsi mali hizo zilivyopatikana, Sekretarieti ya Maadili, hufanya uchunguzi wa kina kubaini jinsi mali ilivyopatikana ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa mali hizo, *physical verification*. Hatua za kisheria huchukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge Viti Maalum alisema uhakiki wa mali na madeni ulifanywa wakati yeye Mheshimiwa Mbunge hakuwepo na kwamba Wahakiki walionyeshwa mali zake na mtoto wake. Uhakiki wa mali hufanywa baada ya viongozi wanaohakikiwa mali zao kujulishwa mapema kwa maandishi kabla ya tarehe ya uhakiki. Taarifa zinazotumika kufanya uhakiki, ni zile ambazo hutolewa na viongozi wenyewe katika tamko lao la mali na madeni katika kipindi husika. Kwa vile kiongozi hakuwepo, Wahakiki walionyeshwa tu shamba lake kwani tayari walishafika katika eneo husika. Sekretarieti ya Maadili, itawasiliana na Mheshimiwa Mbunge, ili kuhakikisha kuwa taarifa zilizotolewa wakati wa uhakiki, ni zile ambazo Mheshimiwa angezitoa yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, walizungumzia kuwa kwa vile sheria imeweka sharti gumu sana kwa wananchi na wadau kuona fomu za mali za viongozi, je, lengo hasa la fomu hizo ni nini kama haziwezi kuangaliwa na wadau kuona kama viongozi wamedanganya au la? Isitoshe Sheria inakataza kabisa mtu aliyeona kutumia taarifa hiyo popote.

Mheshimiwa Spika, masharti ya kukagua daftari la mali na madeni, ni kama ilivyotolewa katika Tangazo la Serikali, Na.108 la mwaka 1996, masharti hayo yanaonekana katika ile Sheria. Hata hivyo, Mashirika matano yasiyokuwa ya Kiserikali, yamefungua kesi ya Kikatiba katika Mahakama Kuu, kupinga masharti yaliyomo katika Tangazo hilo. Kesi hiyo ni Na.28 ya mwaka 2008. Kwa mujibu wa Kanuni 64(a)(c), za

Kanuni za Bunge, Bunge haliwezi kujadili suala hili kwa vile linasubiri uamuzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Mipango, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, wametoa ushauri kwamba Tume ya Mipango iwe chini ya Wizara ya Fedha. Kwa utaratibu uliopo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiye mwenye dhamana ya kuwasilisha bajeti ya taasisi zote zilizopo chini ya Ofisi ya Rais. Tume ya Mipango, iliyoundwa chini ya Ofisi ya Rais, imeingia katika orodha hiyo.

Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, tumepokea ushauri wake mzuri sana na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TASAF. Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ameer Ali Ameer, Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, wao walizungumza zaidi kuhusu taratibu mbalimbali za *TASAF* na matatizo yanayojitokeza. Niseme tu kwa kifupi kutokana na muda ni kwamba miradi yote ya *TASAF*, inabuniwa chini ya uelekezi wa Halmashauri. Wao wakiwa kama ni wajumbe wa Halmashauri, ni vema kama wangufuata utaratibu wangeweza kupata taarifa kutoka kwa Wakurugenzi wao na kwamba miradi inabuniwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kuna mmoja ambaye alizungumzia kuhusu ramani za ujenzi. Miradi yote iliyochangiwa na *TASAF*, inatekelezwa kwa kuzingatia kanuni na viwango vya ubora wa sekta husika.

Hivyo basi, Wizara ziliteua Wajumbe wanaounda Timu ya Wataalam wa sekta ambao wana jukumu la kutoa michoro ya kuhakikisha kuwa miradi yote inayochangiwa na *TASAF*.

Lakini niongezee tu, wafanyakazi wote wanaoongoza miradi hiyo ni wafanyakazi wa Halmashauri, kwa hiyo, wako chini ya uwezo wa Wabunge kuweza kuwauliza maswali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbarak na Mheshimiwa Devota Likokola wamezungumzia kuhusu suala la MKURABITA. Nitoe majibu tu kwa ujumla kwamba MKURABITA imebuniwa kutekelezwa katika awamu nne na zote ni muhimu katika kuhakikisha kwamba malengo yanafikiwa na wala si kwa kusuasua.

Miradi na mafunzo ilitekelezwa katika kuthibitisha ukweli wa yaliyojiri katika awamu ya kwanza ya tathmini ya sekta isiyo rasmi. Katika kutekeleza miradi hiyo,

mafanikio yafuatayo yalipatikana. Ardhi ya vijiji saba ndani ya Halmashauri na Wilaya za Handeni ilipimwa na hati za vijiji kutolewa.

Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji hivyo saba umeandaliwa. Hii itasaidia sana kupunguza migogoro inayoweza kutokea. Uwekaji wa mipaka ya miliki moja moja ilifanyika na ujenzi wa Masjala ya Ardhi katika vijiji hivyo saba umekamilika. Vile vile Wilaya ya Bagamoyo ilifaidika na utaratibu huo.

Aidha, majaribio yalifanyika pia katika Manispaa ya Kinondoni katika eneo la Hananasifu ambapo jumla ya makazi 1,427 yametambuliwa kwa ajili ya kutoa hati miliki. Niseme tu kwamba kwa sasa kuna mmoja ambaye ameuliza kwamba kwa nini haienei kama *TASAF*? Hapana, haiwezekani. Kwa sababu kwa sasa tuko katika *stage* ya tathmini na hapo itakapofikia wakati wa utekelezaji, basi Wilaya nyingi zaidi zitashirikishwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, yeye aliipongeza TAKUKURU kwa kazi nzuri inazozifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa ni zamu ya mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Ghasia. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Wabunge waliochangia katika hotuba yangu nilioiwasilisha katika Bunge lako Tukufu hapo jana.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kwa namna ya pekee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake iliyomfanya aniteue katika Ofisi yake kwa mara nyingine tena mwaka huu kuwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa uaminifu, uadilifu na ufanisi mkubwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza tena Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa na hatimaye kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge lako tukufu kuwa Waziri Mkuu. Tunafahamu majukumu aliyokabidhiwa ni mazito na yenye changamoto nyingi. Napenda kumhakikishia kuwa tutampatia ushirikiano wa kutosha ili kumwezesha kukabiliana na changamoto zilizoko mbele yetu katika kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala kwa maoni na mchango wake ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Napenda pia kumshukuru na kumpongeza Waziri Kivuli wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetupa changamoto kuendelea kuboresha Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenzangu Mheshimiwa Sophia Simba kwa ushirikiano wake wakati wa kuandaa hotuba ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 na namna alivyojibu baadhi ya hoja za Wabunge. Napenda pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote Ofisi ya Rais kwa ushirikiano wao ambao umetuwezesha kuwasilisha hotuba ya Ofisi yetu na kuweza kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine tena kwa njia ya pekee kabisa kuwashukuru wapiga kura wangu pamoja na viongozi wenzangu wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa ushirikiano wanaonipa na juhudi tunazozifanya katika kujiletea maendeleo ya Wilaya yetu. Ni imani yangu kwamba kwa ushirikiano huo tutasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wazazi wangu, baba yangu - Mzee Abdulrahman Mohamed Ghasia na Mama yangu - Kashi Balosi kwa malezi yao na pia napenda kumshukuru mume wangu - Mr. Yahya Mhata pamoja na wanangu kwa kunitia moyo lakini pia kwa kunivumilia pale ambapo natumia muda wao katika kutimiza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yetu kwa kuzungumza na kwa maandishi. Napenda kuwahakikishia kuwa michango yote tumeipokea na tutaifanyia kazi ili kuweza kuboresha utendaji katika Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuwatambua waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa John Paul Lwaji, ambaye ametoa maoni kwa niaba ya Kamati. Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu - Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli, Mheshimiwa Kabwe Zitto Zuberi, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama na Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mheshimiwa Said Amir Arfi, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa maandishi. Hii ni kwa mara yangu ya kwanza tunapata wachangiaji wengi sana kwa kuongea kwa maandishi. Waliochangia kwa kuongea wako 18 na kwa maandishi wako 51, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Dr. Luca Jelas Siyame, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Yacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Dr. Fetus B. Limbu, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Mwanahamisi K. Said, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Maulida Anna Komu, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Gasto Raphael Ligalama, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Sevelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge zililenga katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:- Hoja ya kwanza ilitolewa na Mheshimiwa Grace Kiwelu, wakati akiwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani ambapo alipendekeza kima cha chini cha mshahara kiwe Sh. 250,000/=.

Kama Serikali itaongeza kima cha chini cha mshahara kuwa Sh. 250,000/=, Serikali itahitaji kiasi cha fedha cha shilingi trilioni 3.500 kwa ajili ya kugharamia malipo ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la shilingi trilioni 2.02 ambayo ni sawa na asilimia 138.71 ikilinganishwa na kiasi ambacho tumekitenga cha shilingi bilioni 1.46 ambacho kimetengwa katika bajeti ya mwaka huu.

Aidha, kiasi hicho cha fedha cha shilingi trilioni 3.50 ni sawa na asilimia 14.41 ya pato la Taifa na asilimia 86.42 ya mapato ya ndani. Ndiyo kusema kama tutaongeza mshahara kwa kiasi hiki, huduma nyingi zitakuwa zimeathirika hasa huduma za afya, elimu na huduma nyingine. Lakini pia hata hao watumishi wenyewe tutashindwa hata

kuwapatia vitendea kazi vya kuweza kutekeleza majukumu yao. Ndiyo kusema kiwango hiki cha mshahara ambacho wenzetu wanapendekeza kwa kweli hakiwezekani kutokana na hayo niliyoyaelezea hapo juu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa katika hotuba ya Wapinzani, lakini pia Mheshimiwa Zuberi Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Mheshimiwa Masilingi, pia Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mgeni F. Saad, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Salim Hamisi - Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Feteah Mgeni na Mheshimiwa Ameir pamoja na Mheshimiwa Salum Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa James Wanyancha, Mheshimiwa Salum H. Khamis, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mgeni Kadika na Mheshimiwa Bahati Abeid, walitoa hoja kwamba kima cha chini cha mshahara hakitoshelezi mahitaji muhimu ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahara cha shilingi laki moja kilifiikiwa kutokana na makubaliano baina ya wafanyakazi na Serikali kupitia Baraza la Majadiliano ya Pamoja baina ya Serikali na Vyama vya Wafanyakazi, baada ya kuzingatia vigezo vya kiuchumi na mahitaji mengine ya kijamii. Utaratibu huo ndiyo unaotumika kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Na. 19 ya mwaka 2003. Hata hivyo, Serikali inatambua kwamba kima cha chini bado ni kidogo. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba kadri uchumi utakavyokuwa unaendelea kukua, basi na kima cha chini cha mshahara kitakuwa kinaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, ni kwamba Mheshimiwa Waziri apanguze bajeti yake na akate fungu 20 na fungu 30 kwa maana kwamba fedha hizo ziletwe kwenye bajeti kusaidia kulipa malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Fungu 20 ni fungu kwa ajili ya matumizi ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kukata fedha ndiyo kusema kwamba Mheshimiwa Rais asifanye kazi yoyote na aendeleo kukaa pale Ikulu, kitu ambacho kitakuwa siyo busara. Aidha, Fungu 30 ni fungu la matumizi Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, pamoja na vyombo vyote vya Usalama. Kukata fedha hizo na kupeleka katika fungu la mishahara ni kuwakwamisha kazi, kukwamisha kazi za Ofisi muhimu katika uwendeshaji wa Serikali. Kwa msingi wa maelezo hayo, ushauri huu hautekelezeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo ilitolewa kwamba kima cha chini cha mshahara cha Serikali kizingatiwe pia katika Sekta ya binafsi. Mishahara inapopanda Serikalini ipande pia katika sekta binafsi. Kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi kisheria hupangwa chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na. 7 ya mwaka 2004 na Wizara yenye dhamana na suala hili ni Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Ofisi yangu inashughulikia watumishi wa umma pekee, ndiyo maana tunaitwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa kima cha chini cha pensheni, ni kidogo na hakitoshelezi. Serikali iweke utaratibu wa kuongeza kima cha chini cha pensheni kila mwaka. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inafanyia mapitio Sheria ya Pensheni na tunatarajia kuwasilisha marekebisho yake katika Kikao cha Bunge cha mwezi Oktoba, 2008. Taratibu zote zikikamilika, marekebisho haya yatasaidia pia kubadilisha viwango vya pensheni. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira tusubiri mwezi wa 10 ambapo tutaleta marekebisho ya ile Sheria ya Pensheni, nadhani mawazo yao yataingizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo liliulizwa na naomba maeneo mengine nisiwataje Waheshimiwa Wabunge kwa sababu niliwatambua kule ili niweze kuokoa muda. Kulikuwa na swali liliuliza kwamba, kwa nini Afisa Elimu wa Wilaya awe na ngazi ya mishahara zinazomwezesha kupanda hadi *TGS L* wakati Mwalimu wa Sekondari licha ya uzoefu wa umri sawa kazini kikomo cha mishahara wake kiishie *TGS H*?

Mheshimiwa Spika, suala la kupanga ngazi ya mishahara linategemea muundo wa utumishi wa kada husika na siyo sahihi kuwa watumishi walio katika kada moja, lakini wanafanya kazi sehemu tofauti wanalipwa mishahara tofauti. Aidha, kada nyingi katika utumishi wa umma zinaishia katika ngazi ya *TGS H*. Kuanzia ngazi ya *TGS I* ni vyeo vya madaraka na siyo vyeo vilivyomo katika muundo wa maendeleo ya utumishi kwa kada mbalimbali. Kama nilivyokwisha kuelezea awali ngazi ya mishahara ya *TGS I* hadi *Q* ni ngazi ya madaraka na hivyo utaratibu wa sasa ni wa kuhamisha Maafisa Elimu kwenda katika Halmashauri ya Wilaya, unazingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, samahani hapo, kuna suala ambalo liliulizwa, kwa nini mwalimu wa sekondari au wa shule ya msingi akipata nafasi Wilayani, kikomo cha mishahara wake kinakwenda hadi *TGS L* wakati mwenzake anayebakia sekondari au kupata nafasi katika Sekretarieti ya Mkoa isivuke *TGS H*. Kama nilivyojibu mwanzo kwamba katika muundo wa utumishi wa umma kada nyingi zinaishia *TGS H*. Kuanzia *TGS I* hadi *Q* ni nafasi za madaraka. Kwa hiyo, ukipata uteuzi hata kama ni mwalimu wa sekondari kama utateuliwa kuwa Mkuu wa Idara, basi utaweza kupata mishahara wa *TGS I* na kama utachaguliwa kuwa Katibu Mkuu, basi utaruka utakwenda katika hizo ngazi kwa sababu ni nafasi za madaraka na haziko katika muundo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kwamba taarifa ya Tume ya Rais ya kuboresha mishahara ya watumishi wa umma itolewe hadharani. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Grace Kiwelu wakati akiwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani. Taarifa ya Tume ya Rais ya Kurekebisha mishahara ni ya Mheshimiwa Rais. Hivyo kuitoa hadharani kutategemea ridhaa yake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nyongeza za mishahara za Januari, 2008 ni makundi gani yaliyopata nyongeza zaidi? Kulingana na sera ya malipo ya mishahara kwa watumishi wa umma, nyongeza kubwa zaidi ilitolewa kwa wataalam wa ngazi za kati ambao Serikali hupata shida kuwavutia, kujiunga na kubaki katika ajira ya utumishi wa umma.

Jana wakati nawasilisha bajeti yangu, nilisema kwamba mishahara imeongezeka kati ya asilimia 17 hadi asilimia 30.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge alitaka kufahamu ni akina nani hao ambao wamepata hiyo asilimia 30? Kwa hiyo, napenda nimhakikishie kwamba hiyo asilimia 30 haikwenda kwa wa juu sana wala huku wa chini. Ni kwa ajili ya wataalam ambao wako katika ngazi za kati kati ambao tuna ushindani nao kuwapata katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la tofauti kubwa ya mishahara kati ya kima cha chini na kima cha juu cha mishahara na vigezo vinavyotumika kupanga vitajwe. Misingi ya malipo ya mishahara kwa watumishi wa umma ni tathmini ya kazi, yaani *job evaluation*, zoezi ambalo lilifanyika katika mwaka wa 1998 hadi mwaka 2000 na utekelezaji wake kuanza mwaka 2003. Kutokana na taarifa ya zoezi hilo ambalo ni utaratibu wa kimataifa, Serikali inalipa mishahara yake kwa vigezo na misingi hiyo.

Hata hivyo, viwango vya malipo hutegemea uwezo wa kiuchumi. Kuhusu malipo ya posho mbalimbali Serikalini, pia napenda niongezee hapo kwamba ile tofauti ya kima cha chini na cha juu pia Tume ile ya Rais ambayo aliionda, ilitushauri kwamba badala ya kuwachukua watumishi wote tukawaweka katika kundi moja, basi tuwaweke katika makundi mawili. Itakuwa siyo sahihi kuangalia mishahara wa juu na wa chini kwa kumchukua Mhudumu na Katibu Mkuu Kiongozi.

Lazima watumishi tuwagawe katika makundi mawili. Kundi la kwanza ambalo ni hawa ambao tunasema ni *graduate* wamemaliza Chuo Kikuu, yule mishahara wake wa kuanzia ukimlinganisha na Katibu Mkuu Kiongozi utakuwa sahihi kwa sababu ni ngazi ambayo anaweza akaifikia. Lakini kwa Mhudumu, basi umlinganisha na *Office Supervisor* au Mwangalizi wa Ofisi ile, kwa sababu ndiyo ngazi ambayo kama atajiendeleza ataweza akafikia. Kwa hiyo, *gap* tuangalie katika viwango hivyo viwili.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kutokana na tofauti kubwa kati ya mishahara, kuna tatizo kubwa la utendaji Serikalini. Dalili ya migomo baridi na kwa watendaji wa ngazi za chini na kati kukua kwa rushwa ndogo ndogo kunakosababishwa na watumishi hao kuhimili gharama ya maisha ambayo imekuwa kubwa sana ikilinganishwa na hali halisi ya gharama ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza, tofauti hiyo ya mishahara inavyotokea, lakini pia kuhusu suala la rushwa, kwa kweli ni tabia binafsi na wala hailingani na kima cha mishahara cha mtu. Wapo ambao wanapokea mishahara mikubwa na bado wenyewe wanaomba na kupokea rushwa. Kwa hiyo, tunaomba watumishi wale ambao wanapokea rushwa waache kutumia hicho kisingizio. Lakini bado Serikali itaendelea kuboresha mishahara ya watumishi kadri uchumi unavyokua. (*Makofi*)

Suala lingine ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Slaa: Je, Serikali iko tayari kutamka hasa kima cha chini cha mishahara ni shilingi ngapi? Kama nilivyoieleza katika hotuba yangu, kima cha chini cha mishahara kwa mwaka 2008/2009 ni shilingi laki moja kwa mwezi. (*Makofi*)

Ofisi za Utumishi wa Umma zimejaa urasimu, barua hazijibiwi na zinapojibiwa huchukua muda mrefu. Suala hili limeulizwa na Wabunge wengi. Ni kweli tunakiri kwamba zipo baadhi ya Ofisi ambapo kuna urasimu wa kujibu barua na hata zinapojibiwa zinajibiwa kwa kuchelewa.

Kwa hiyo, hatua tunazochukua sasa hivi ni suala la upimaji wa mtumishi, utendaji kazi wa mtumishi mmoja mmoja na pia katika Ofisi zetu za Serikali tumeweka Vitengo vya kushughulikia malalamiko ya wananchi.

Kwa hiyo, tuna imani kabisa na kupitia mikataba yetu ya Huduma kwa Mteja, hali hiyo itarekebishwa. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla tunawaomba waendeleo kudai haki yao lakini pia waitambue ile mikataba ya huduma kwa mteja. Wakifahamu ile mikataba ya huduma kwa mteja watakuwa mstari wa mbele kudai haki lakini pia kuwafichua wale ambao ni warasimu na ambao pia wanachelewesha kujibu barua ili waweze kuchukuliwa hatua zinazopaswa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ambayo tayari nimeshaijibu ambayo ilitoka kwa Mheshimiwa Zuberi Zitto ya pensheni ndogo, nimeshaitolea ufafanuzi. Suala lingine ambalo lilitolewa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ni suala la Serikali ifanyie tathmini miundo ya utumishi ya Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea kuona kama inakidhi haja.

Mheshimiwa Spika, suala la kufanyia tathmini miundo ya Serikali, Wizara na Idara zinazojitegemea ni la kuendelea, tunalifanya kila siku na mara nyingi linatokana na mahitaji. Kwa hiyo, wakati mwingine linaweza likaanzishwa na Idara yenyewe husika au wakati mwingine hata wale wanao tuona pia wanaoona huduma zetu na ile miundo yetu pia huwa wanatoa mapendekezo na tunafanyia kazi. Kwa hiyo, ni mchakato wa kuendelea. Kwa hiyo, ushauri tunauzingatia na pia tumekuwa tukifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, taratibu za ajira ya wataalam wa kigeni zimeendelea kuwepo kwa kuwa hakuna mpango madhubuti wa kuendeleza wataalam wazalendo kama njia ya kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2002, watumishi wa kigeni huajiriwa pale ambapo hakuna mtaalam wa aina hiyo ambaye anaweza kupatikana hapa nchini. Aidha, wataalamu wa kigeni wanaweza kuajiriwa kwenye miradi ya maendeleo ambayo Serikali inatekeleza kwa ushirikiano na wafadhili kulingana na makubaliano yaliyomo kwenye mikataba.

Hata hivyo, idadi ya wataalam wa kigeni imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Mfano, mwezi Januari hadi Desemba, 2005 tulikuwa na wataalam wa kigeni 1,848. Januari, 2006 hadi Desemba, 2007 tulikuwa na wataalam wa kigeni 722 na Julai, 2007 hadi Juni, 2008 tunao wataalam wa kigeni 636. Pia kupitia mpango wa pamoja wa misaada Tanzania, yaani *PAMITA* Serikali inaandaa Sera ya kusimamia ajira za kigeni kama ilivyo kwa misaada mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Yono Kevela - Mbunge wa Njombe Magharibi, kwamba baadhi ya watumishi wakiwemo Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na wengine huajiriwa na TAMISEMI badala ya kuajiriwa moja kwa moja na Halmashauri husika na hivyo kufanya uwajibikaji wao kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2008 Mamlaka za Uteuzi na Ajira zimekuwa bayana ambapo Rais kama Mamlaka ya Uteuzi, ana mamlaka ya uteuzi kwa watendaji wakuu wa Majiji na Waziri mwenye dhamana za Serikali ya Mitaa ana mamlaka ya uteuzi kwa watendaji wakuu wa Serikali za Mitaa, chini ya Sheria hiyo ya Utumishi. Watumishi wengine wote wakiwemo Wakuu wa Idara ndani ya Halmashauri huteuliwa na kuajiriwa na Halmashauri husika. Chini ya Sheria hiyo, kuna tofauti kati ya mamlaka za uteuzi na ajira kwa kuwa kila anayeteuliwa huwajibika kwa mwajiri wake moja kwa moja.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia mtiririko wa mamlaka na madaraka katika suala la uteuzi na ajira watumishi wote wa Halmashauri ni waajiriwa wa Serikali za Mitaa, hata kama mamlaka yao ya uteuzi ni Rais au Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, akishateuliwa Mkurugenzi wa Jiji au Halmashauri, basi anabaki kuwa mamlaka yake ya ajira ni Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hati chafu. Nimeulizwa: Je, Halmashauri inapopata hati chafu watendaji waliohusika wanachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 cha Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2004 kinaelekeza adhabu zinazoweza kutolewa kwa mtu yeyote anayesababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. Adhabu hizo ni pamoja na kukatwa mishahara au kushitakiwa. Kwa wale wanaopata hati safi, Serikali inaandaa utaratibu wa kuwapongeza na kuwapatia motisha mbalimbali kwa mujibu wa kanuni zitakazotayarishwa na Wizara ya Fedha na Uchumi chini ya kifungu cha 32 cha sheria niliyoinukuu hapo juu.

Mheshimiwa Spika, zamani Kamati ya Serikali za Mitaa, Halmashauri zilikuwa zinapewa adhabu na zile adhabu kwa wale watendaji zilikuwa zinatekelezwa. Sijui hiyo sheria ikoje, lakini namwomba Mwenyekiti wa Kamati hiyo aiangalie, kama bado inamruhusu kwa wale wanaopata hati chafu, basi aone ambacho anaweza akashauriana na Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ucheleweshaji wa mishahara ya watumishi, hasa walimu. Mfano Halmashauri ya Muheza, imelalamika kwamba mishahara ya watumishi haipelekwi Halmashauri kwa muda mrefu kutokana na Hazina kutokupata taarifa zao kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hali hii inafanya Halmashauri kulipa mishahara hiyo kutoka katika mafungu mengine.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya watumishi huandaliwa na Hazina, baada ya waajiri mbalimbali kuwasilisha taarifa kuhusu uhalali wa watumishi wanaojiriwa, hususan kwa kuzingatia ikama na sifa pia za watumishi wanaojiriwa. Kwa utaratibu huu, taarifa zote zinazohusu ajira mpya zilizofikishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zimeshughulikiwa. Zile ambazo zilikuwa sahihi zimepelekwa Hazina na zile ambazo zinaonekana zina mapungufu huwa zinarejeshwa kwa waajiri wanaohusika na kuelekezwa waondoe zile dosari. Kwa hiyo, tunawaomba Halmashauri ya Muheza, kama kweli kuna hilo tatizo la watumishi kukaa muda mrefu kabla hawajapata mishahara yao warekebishe matatizo ambayo yanachelewesha katika kuwaingiza katika orodha ya malipo ili watumishi hao waweze kulipwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo inasema Serikali haiwajali watumishi walioacha kazi kwa sababu za ugonjwa na baadaye kupata unafuu kwani hawajiriwa kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera, Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Serikali inaruhusu ajira ya mkataba kama mojawapo ya masharti ya kazi yanayotambulika. Aidha, watumishi walioacha kazi kwa ugonjwa, baada ya mapendekezo ya *Medical Board* kuzingatiwa, Mwajiri mpya anayetakiwa kuwaajiri anahitajika kupata mapendekezo mapya ya Bodi ya Madaktari kuhusu afya na uwezo wa mtumishi huyo kumudu kazi anazohitaji kufanya chini ya mkataba mpya. Kwa hiyo, kama Bodi itaridhia, anaweza akaajiriwa kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, alitoa ushauri kwamba utaratibu wa kufanyiwa *vetting* kwa watumishi wanaoshughulikia nyaraka za siri kwa lengo la kutambua uaminifu na uadilifu kabla hawajapangiwa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhakikishia Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu huu upo wa kuwafanyia upekuzi watumishi wanaojiriwa ambao kazi zao ni kushughulikia nyaraka za siri. Aidha, pia tunatambua kwamba tabia ya mtumishi inaweza kubadilika baada ya kuajiriwa.

Kwa hiyo, wanapotakiwa kupata uteuzi wa aina yoyote huwa wanafanyiwa tena upekuzi kabla ya kupata nyadhifa mbalimbali Serikalini. Pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika eneo hili, hatua zimechukuliwa kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa maafisa wanaoshughulikia nyaraka za siri Serikalini. Lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuache kuwashawishi watendaji Serikalini kutuibia nyaraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hilo hilo la uvujaji wa siri na hatua ambazo tumekuwa tukizichukua, Mheshimiwa, alitaka kuzifahamu. Ofisi yangu ina jukumu la kuandaa sera, miongozo na miundo ya kiutumishi katika utumishi wa umma. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kumbukumbu katika utumishi wa umma na Taifa kwa ujumla, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba matumizi yako sahihi na utunzaji wake pia unakuwa mzuri.

Uvujaji wa siri ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Taifa Na.3 ya mwaka 1970, kifungu cha 6(2)(b). Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka, Kifungu Na. 3(21) na (22) ya mwaka 2002 na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake. Aidha, hivi karibuni Ofisi yangu ilitoa nyaraka zenye maelekezo ya utunzaji wa siri wa kumbukumbu na kuzitaka Mamlaka mbalimbali kutoa taarifa ya utunzaji wa kumbukumbu kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, ni lazima nikiri kuwa kuwakamata wanaovujisha siri ni kazi ngumu kwa sababu suala hili hufanywa kwa umahiri kati ya mtoaji na mpokeaji. Kama ilivyo katika utoaji wa rushwa, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba wanaohusika katika Mamlaka husika kusimamia siri za Serikali wanawajibika. Lakini pia teknolojia inasababisha uvujaji wa siri uwe rahisi. Linalotakiwa ni kuwaelimisha watumishi wa umma, kitu ambacho tunakifanya, ili kukabiliana na tatizo hili la utandawazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ajira ya wastaafu kwa mkataba ukomeshwe ili kutoa fursa kwa vijana kuajiriwa. Napenda kusema kwamba sio sera ya Serikali kuajiri wastaafu, lakini huwa tunafanya hivyo pale ambapo inajitokeza kwamba ile nafasi hakuna mtu wa kuijaza, kwa hiyo, tunaajiri kwa muda mpaka pale ambapo wanapatikana watu wa kuziba ile nafasi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kwamba taarifa zinazoletwa utumishi za upandishaji wa vyeo sio sahihi na hivyo kuna watumishi ambao wanakaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Utumishi Na.8 ya mwaka 2002, Mamlaka ya Upandishaji Vyeo ya watumishi ni ya waajiri husika. Ofisi ya Rais, Utumishi, tuliingilia kati baada ya kuona kwamba kuna watumishi wamekaa muda mrefu katika cheo kimoja bila kushughulikiwa kuwapandisha vyeo.

Kwa hiyo, tukaamua kufanya zoezi maalum la kuhakikisha kwamba tunawaondoa wale watumishi ambao wamelundikana katika cheo kimoja. Kwa sasa hivi kila muajiri anatakiwa awashughulikie, awapandishe vyeo watumishi wake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo lilielezewa kwamba watumishi waliokaa muda mrefu waondolewe kwenye sehemu hizo, hasa Wakuu wa Idara. Suala la kuhamisha watumishi waliokaa muda mrefu, tunalifanya hasa kwa kuangalia wale ambao ukaaji wao wa muda mrefu unazorotesha utendaji wa kazi. Kwa kuwa suala hili ni la gharama, hatuwezi tukalifanya kwa Wizara zote, Halmashauri zote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, tunalifanya awamu kwa awamu, kadri pesa zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la fedha za uhamisho, kwamba watumishi wanakaa muda mrefu bila kupewa fedha zao. Serikali kwa kweli inashughulikia na mara nyingi taarifa sahihi zinapoletwa, watumishi husika huwa wanalipwa na sasa hivi tumetoa maelekezo kwamba kama hakuna pesa watumishi wasihamishwe.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala ambalo lililetwa na Mheshimiwa Galinoma, kuhusu kuwepo kwa sekretarieti za Mikoa kunachangia utendaji na usimamizi mbovu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, muundo wa sekretarieti za Mikoa umepitiwa na hivyo kuanzia leo tarehe 01 Julai, 2008 miundo mipya ya sekretarieti za Mikoa inaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la matumizi ya kawaida Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuzidi bajeti kutoka shilingi bilioni 9.8 hadi shilingi bilioni 12 ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed - Mbunge wa Kojani, Zanzibar, wakati anachangia jana. Wakati anachangia alisema kwamba lilitokana na kiongozi mstaafu - Mheshimiwa Mkapa, kwamba alitumia shilingi bilioni 2.6 kwenda kusuluhisha wenzetu kule katika mgogoro wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba gharama za Mheshimiwa Mkapa, pamoja na msaidizi wake mmoja kwa shughuli ile ambayo aliifanya Kenya, Serikali ya Tanzania haikutoa hata senti tano. Ziligharamiwa na Umoja wa Mataifa. Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Ulaya, ndio walichangia katika gharama hiyo. Ongezeko la matumizi katika fungu lile lilitokana na kupanda kwa gharama za matibabu ya viongozi wetu wastaafu nje ya nchi, lakini pia viongozi wetu wastaafu wa kitaifa wameongezeka kutoka 11 hadi 12. Lakini pia kulikuwa na suala la kupanda kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kwamba watendaji wanaosababisha kuwepo na watumishi hewa wanachukuliwa hatua gani? Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu jana, Serikali inaendelea na uchunguzi na pindi uchunguzi ukikamilika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi na kwa muda niliopewa nisingeweza kuzimaliza zote kwa pamoja, lakini napenda niwahakikishie kwamba tutazijibu kwa maandishi na zitatolewa kwa Wabunge wote kabla ya Bunge hili kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ili iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu ni ya kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono na tutaiamua baada ya hatua inayofuata. Katibu, hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 20 – State House

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... Shs. 6,211,007,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yeyote)

Fungu 30 - President's Office and Cabinet Secretariat

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... Sh. 137, 286,553,500/=

SPIKA: Naona wawili, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Tunaanza na Mheshimiwa John Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kwanza, nataka kutumia nafasi hii, au niseme *program* kwanza, ni *program* ya 10 *sub-vote* 1000 na *basic salary* ya Mheshimiwa Waziri, ambayo ni kifungu 250,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nimezungumzia juu ya kuimarisha vyombo vya usalama wa nchi yetu na zaidi imebidi nizungumzie jambo hili kwa sababu kama unavyofahamu Bunge lako Tukufu kwa muda takribani wa kama miezi sita hivi tumekuwa tunazungumzia mambo ambayo yanaichafulia jina nchi hii. Kwa mfano, ufisadi, tumezungumzia sana juu ya rushwa, mpaka tumefika mahali Waziri Mkuu kajiuzulu na bado unaona kuna utata katika sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, nilivyoandika au nilivyotoa maoni yangu, labda ni muundo wetu wa vyombo hivi vya usalama kwamba viko karibu mno na watendaji wakuu wa Serikali ya kwamba *independence* ya vyombo hivi. Nikasema, labda ingefaa zaidi sheria ile ingerekebishwa ili vyombo hivi viwe nje, kama vile hapa tumezungumzia juu ya matumizi mbalimbali, lakini kwa mfano tuna *vote* ya Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *vote* hii 30, huwezi ukaona kwa mfano fedha ya Taasisi ya Usalama wa Taifa, huwezi ukaona kwa mfano fedha za TAKUKURU na vitu kama hivyo. Vyote vimefungwafungwa humu ndani na *transfers to something* na nini, zipo najua lakini hazionekani. Lakini hili jambo tumelipitisha kisheria. Sasa kuna tatizo gani kuwa wazi tu? Kama tunatumia bilioni kadhaa kwa ajili ya TAKUKURU ijulikane na *vote* yake ijulikane, kama tunatumia bilioni kadhaa kwa ajili ya Usalama wa Taifa, ijulikane. Kuna tatizo gani katika mambo kama hayo? Lakini zaidi naona ni vizuri tuweze kuipa nguvu Idara ya Usalama wa Taifa, hata ya kumwajibisha a *sitting President*, imeshaonekana kwa mfano Nickson, aliwajibishwa na CIA kwa ku...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, madhumuni ya Kamati kwa wakati huu kwa mujibu wa kanuni ya 101, ni kupata ufafanuzi wa jambo mahususi. Nimekubali umezungumzia kuhusu shughuli nyingi kuwa zimefungwa pamoja katika *sub-vote* fulani kiasi kwamba huwezi hata kujua humu inazungumzia kitu gani. Hilo kwamba, kumbuka

nilikwishafanya *rulling* lipelekwe Kamati ya Fedha na Uchumi, wazungumze na Serikali ili kuangalia kwa upana wake, maana yake haliihusu Ofisi hii peke yake. Sasa tena umeingia la Rais kuwajibishwa na Usalama wa Taifa. Sasa hili linahusika wapi hapa? Labda sijakuelewa vizuri.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nimetoa ushauri, nimeanzia kwa kusema sheria irekebishwe mpaka tufike mahali ambapo vyombo hivi vina uhuru hata wa kuanzisha kesi ya kumwajibisha Rais kama kuna vitu ambavyo amekosea, ndio kitu ambacho najaribu kukieleza. Lakini ukiangalia hapa, kwa sababu vyombo hivi viko karibu sana na Rais, ni vigumu sana. Sio Rais, tu mimi nazungumza inaweza pia kuwa ni Mawaziri, inaweza kuwa Waziri Mkuu, inaweza kuwa viongozi mbalimbali, tungependa kwa mfano hapa fursa ya Kikatiba, tunaweza kupiga *vote of no confidence* kwa Waziri Mkuu, kwa mfano. Tungependa chombo kama hiki ndio kiwe na uwezo wa kukupatia wewe Mheshimiwa Spika...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, hilo limo kwenye Katiba. Kumwondoa Waziri Mkuu, imo kwenye Katiba.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio imo, lakini nasema uhuru wa chombo hiki kuku-*advise* kama wewe, haiko bayana. Ndio maana nimesema kwamba nataka *comment* za Waziri, juu ya kubadilisha sheria kupata *independence* zaidi kwa vyombo hivi. *This is a subject* ambayo nazungumzia.

MWENYEKITI: Nadhani hakuna haja ya Waziri kushughulika na jambo hili kwa wakati huu. Mimi ninachosema, Waheshimiwa Wabunge, tutambue tuna madaraka makubwa sana na ni pamoja na kuleta Miswada binafsi, Miswada ya Kamati, nakadhalika. Mawazo mazuri kama haya fanya *networking*, ona kama lina kubalika kubalika, tulettee Muswada binafsi. Utasubiri Serikali itunge Muswada kuhusu Rais, unaweza kusubiri mpaka tumalize karne hapa. Tunaendelea. Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia *vote 30* hiyo, *program* ya 10 - mshahara wa Waziri, kuhusiana na suala zima la Idara ya Usalama wa Taifa. Waziri alijibu kwamba amepokea ushauri wangu, sasa sijui ni ushauri gani ambao amepokea. Kwa hiyo, nilikuwa naomba anifafanulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilisema kwamba kufuataia udhaifu wa sheria na hasa sheria ya *TIS* ya mwaka 1996, ndio matatizo ambayo nchi yetu imeyapata ambayo Mheshimiwa Cheyo, ameyazungumza kama masuala ya ufisadi. Nikasema wazi kabisa kwamba kwa mfano suala la *MEREMETA* ni la wizi, sio suala la Usalama wa Taifa.

Pia nikawa nimesema kwamba sheria Na.3 ya mwaka 1970 na sera nzima ya Usalama wa Taifa, iweze kuangaliwa upya kwa ajili ya kuongeza suala zima la *economic espionage* ili Idara ziweze kutetea maslahi ya nchi ya kiuchumi. La tatu ni suala la kifungu cha 5 na kifungu cha (2)(a) katika sheria Na.15 ya mwaka 1996 kwa ajili ya

kuweza kuipa *temporarily power of arrest*, yaani ku-*enforce security measures* Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri anifahamisha, ni ushauri upi ambao ameuchukua katika hizi *part* nilizokuwa nimezisema? Au ni zote?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumfafanulia Mheshimiwa Cheyo kwamba nimemjibu kwamba kuhusu mabadiliko ya sheria, Serikali imepokea na itayafanyia kazi. Serikali ina vyombo vyake, itakaa na kuangalia kama kuna matatizo. Suala lingine ambalo amelizungumzia, linasema kuipa nguvu ya kukamata, nimfahamisha tu kwamba vyombo vyote hivi kimsingi vina uwezo wa ku-*arrest* kwa kutumia taratibu ambazo zimewekwa za kisheria.

MWENYEKITI: Kwa kifupi, ninavyomwelewa Mheshimiwa Waziri, ushauri wako wote Mheshimiwa Zitto, kwa vipengele vile vitatu, Serikali imekubali kuufanyia kazi. Sasa hatima yake hatujui kama kutakuwa na matatizo mbele ya safari, basi baadhi ya mapendekezo yatarekebishwa kulingana na jinsi hali halisi itakavyoonekana. Nadhani ni jibu la kutosha.

MWENYEKITI: Bado? Mheshimiwa Zitto, ulichoomba ni kwamba akufafanulie ni ushauri upi? Yeye amesema ni kwa vipengele vyote vitatu. Kwa hiyo, sioni uhalali wa wewe tena kusimama kuomba ushauri mwingine tena ikiwa yeye amekwishakubali yote matatu. Usubiri, utakuja kuuliza baadaye hali imetekelezwa ama vipi?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yeyote)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Shs.	484,031,700/=
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Division</i> ...	Shs.	442,797,600/=
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Shs.	317,735,600/=
Kifungu 1005 – <i>Management Information System</i> ...	Shs.	287,624,900/=
Kifungu 2001 – <i>Cabinet Secretariat</i>	Shs.	1,132,508,600/=
Kifungu 2002 – <i>Communication Division</i> ...	Shs.	403,891,600/=
Kifungu 2003 – <i>Good Governance</i>	Shs.	434,752,000/=
Kifungu 2004 – <i>Public Service Appeal</i>	Shs.	300,708,500/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yeyote)

Fungu 32 - President's Office – Public Service Management

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... Shs. 8,469,257,900/=

MWENYEKITI: Kifungu hicho, ngoja tuwaorodheshe. Naanzia NA Mheshimiwa Galinoma, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ester Nyawazwa, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Tunaanza na Mheshimiwa Galinoma.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Fungu 32, *Program 10, sub-vote 1001 - Administration and General*, kifungu 250100, mshahara wa Waziri. Nashawishika kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyotoa, lakini kwa kuwa ni mafupi kiasi kwamba sina hakika amejibu nini, ninashindwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia mambo matatu ya msingi, kuhusu muundo wa hovyo wa sekretarieti kule Mkoani, muundo wa kanda ambao unatupa shida sana sisi tusiokuwa na *Zonal Headquarters* na pia suala la kuwa na Serikali mbili mpaka katika ngazi ya Tarafa. Jibu kwamba kuna mabadiliko katika muundo kuanzia leo ningeupokea kwa furaha sana kama ningejua mabadiliko haya ni nini. Kama yanajibu *point* hizo tatu, lakini kwa kuwa majibu ni sentensi hiyo moja, sina hakika amesema nini na kwa hiyo, siwezi kumpongeza, *let us be serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama angeweza kunihakikishia kwamba *issue* zote hizo tatu zina majibu au kuna mabadiliko yanayohusu *issues* hizo, ningemwelewa, lakini akisema tu leo tarehe mosi Julai, muundo mpya unanza bila kusema ni muundo gani, kwa kweli simwelewi. La sivyo, nitaona taabu kidogo kukubali, naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Nimekuelewa na nina hakika hata Mheshimiwa Waziri, amekuelewa. Ufafanuzi Mheshimiwa waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu suala la muundo wa Sekretarieti, yeye katika uchangiaji wake alizungumzia lile suala la kuwaita washauri, washauri. Lile kwa kweli naliafiki na katika kurekebisha sasa hivi wale kama ni Afisa Kilimo ataitwa ni Afisa Kilimo, kama ni Mhandisi ataitwa Mhandisi na wale wakuu wa *cluster* waitwe wasaidizi wa Katibu Tawala wa Mkoa, hilo kwa upande wa sekretarieti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuwa na kanda, maana ya kuwa na kanda mfano ukisema Kanda ya Kusini haiwezekani Kanda ya Kusini yenye Mikoa ya Lindi na Mtwara kila Mkoa ukawa na kanda.

Kwa hiyo, kama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kama Makao Mkuu ni Mbeya hatutegemei na Iringa kama inaweza ikawa na kanda, lazima katika ile Mikoa inayounda Kanda kunakuwa na Mkoa mmoja ambao ndio unakuwa Makao Makuu ya Kanda, lakini ule uwepo wa Kanda unapunguza gharama za watu kutoka Iringa akaenda Dar es Salaam.

Mimi nadhani kutoka Iringa kwenda Mbeya ni karibu zaidi au kwa mtu wa Ruvuma au Rukwa kwenda Mbeya ni karibu zaidi kuliko kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, huu muundo wa Kanda unapunguza gharama za Serikali, lakini pia unaboresha katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lake la tatu kuhusu suala la kwamba Serikali kuu inaishia Tarafani, Serikali Kuu haiishii tarafani, kwa sababu tunazo Mahakama za Mwanzo. Mahakama haziko chini ya Serikali za Mitaa wala tunaposema tuna vituo vya Polisi, *Police Post* zile ambazo ziko mpaka kwenye kijiji, ile si vituo vya Serikali za Mitaa! Kwa hiyo, huu mfumo wa Serikali Kuu unakwenda mpaka kwenye Mtaa na unakwenda mpaka kwenye kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nadhani ufafanuzi umeupata. Tumia *mic*, hatukusikii, haujawasha *microphone*.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani iligoma kidogo.

MWENYEKITI: Wakati unaendelea, nikumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba madhumuni ya Kamati ya Matumizi ni kupata ufafanuzi. Ufafanuzi unaopatikana unaweza kuwa huupendi kabisa kwa sababu hautoshelezi yale unayoyataka, lakini hapo ndio mwisho. Ndio mwisho wa Serikali kusema, kwani sio suala la hapa kwamba uongee tu mpaka uridhike Kanda ihamishwe sijui nini, basi hebu nikusikie kwa sababu ukienda huko nitakukatiza tu.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hilo la kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Waziri, ninashukuru sana na sasa nafikiri ni sahihi kabisa nimpongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la Kanda nilichokuwa nime-*suggest* ni kwamba kila Mkoa uwe na *full compliment* ya *staff* badala ya Mikoa mingine kuwa inategemea sehemu nyingine, *it was as simple as that*. Najua Serikali za Mitaa kuwa Serikali kuu kuendelea mpaka kwenye tarafa, nazungumzia *administration*, siyo mambo ya Mahakama na mambo kama hayo, kwa hiyo, bado ninahitaji ufafanuzi.

MWENYEKITI: Ufafanuzi kwa hili la pili, nadhani kwa kweli hali ndiyo hiyo Kanda lazima iwe ni mahali pamoja tu katika Mikoa kadhaa. Lakini hili la pili la utawala.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukizungumzia kwa maana ya utendaji wa Serikali hii kuu kwa maana ya Mahakama kwa mfumo wa Mahakama, mimi nadhani

kuwa na Mahakama ya Mwanzo bado ni masuala ya kiutawala kwa mtiririko wa ile Mahakama, lakini pia Mheshimiwa Mbunge yeye alikuwa ni mtumishi na alikuwa katika ngazi ya mpaka Katibu Mkuu kama sikosei, mimi sikumbuki kama Serikali Kuu imewahi kwenda mpaka katika Mtaa, sikumbuki. Lakini kama yeye analo wazo la kutusaidia ili Serikali Kuu iweze kwenda mpaka kwenye Kitongoji, basi tutamwomba baada ya Bunge atusaidie ili tuweze kuboresha.

MWENYEKITI: Huna haja ya kuahidi vitu kama hivyo Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Serikali za Mitaa ndio Serikali za watu, sasa hatuwezi ghafla tukabadili sera tena tukawa na Serikali Kuu iko mpaka kwenye Kitongoji. Mimi nadhani inawezekana Mheshimiwa Mbunge yeye haridhiki na hilo, lakini ndio utaratibu wa sasa na wako baadhi yetu tunaridhika na hilo, ndio utaratibu mzuri. Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tu niseme kwamba na mimi niko kwenye *vote* hiyo hiyo kama ilivyosemwa ili kuokoa muda na niko kwenye *program* hiyo hiyo ya 10 na *sub-vote* kama ilivyoonyeshwa hapo juu na kifungu ni kile cha mwanzo kabisa cha mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema, kwamba mimi napenda kupata ufafanuzi wa suala moja mahsusi kabisa. Toka mwaka 2007 nimekuwa nikifuatilia sana watumishi 10 wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambao ni watendaji wa Kata na watumishi wawili ambao wako katika Halmashauri yetu ambao mpaka sasa kwa takriban miaka kumi na kitu au ishirini hawalipwi kupitia *payroll*, hawajui hatima ya maisha yao katika ofisi wanazofanyia kazi na tumekuwa na mawasiliano kati ya TAMISEMI na Ofisi ya Utumishi, lakini cha kusikitisha Mr. Mchau tarehe 07 Mei, 2007 aliandika barua Ofisi ya TAMISEMI akisisitiza kwamba hauko ushahidi kwamba taratibu za kuajiri ...

MWENYEKITI: Mr. Mchau ni nani?

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mr. Chau alikuwa ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi. Wakati anaandika barua hiyo alisisitiza kwamba watendaji na hao watumishi wengine wawili hauko ushahidi kama kweli walijajiriwa kufuatana na taratibu zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwa sababu kama hauko ushahidi, wanaendeleaje kulipwa mishahara na waweze kukosa haki yao ya kuingizwa kwenye *payroll* mpaka sasa hivi? Tatizo hilo ni la karibu Halmashauri zote za nchi hii, ninayo orodha hapa na nitawapa Waheshimiwa Wabunge wataiona.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini watumishi hao wataingizwa kwenye *payroll* kwa sababu kama haya yote yalitokea, sio kwa sababu zao ni kwa sababu ya Serikali yenyewe. Kwa nini sasa adhabu iwapate wao? Ni lini watumishi wataingizwa kwenye *payroll*, watendaji wangu hao 10 na hao watumishi wawili ili haki yao ipate kutendeka? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ni dakika 10 kabla ya muda wa kuahirisha Bunge kwa jioni, natumia mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 28 fasili ndogo ya tano kuongeza muda huo kwa nusu saa ili tuweze kuwasikiliza Wabunge wote ambao wamesimama kutaka ufafanuzi, baada ya hapo ninamwomba Mheshimiwa Waziri aweze kutoa ufafanuzi wa suala la Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala ambalo amelitoa Mheshimiwa Jenista Mhagama na si katika Halmashauri yake tu ziko Halmashauri nyingine kama ya Tandahimba na tatizo lilitokea kwamba baadhi ya Halmashauri ziliajiri watumishi bila kufuata miundo, bila kuangalia sifa na wengine walijiri bila kuwa wale watumishi kuwekewa bajeti katika ikama.

Lakini baada ya kulifuatilia tatizo hili, baadhi ya Halmashauri matatizo hayo tumeshakuwa tukiondoa kwa sababu wakipata kibali cha kuajiri wanawaingiza, lakini kwa kuwa linaonekana ni tatizo kubwa kwa Halmashauri nyingi, ofisi yangu inalitafakari ili kuona jinsi ambavyo tunaweza tukaondokana nalo hili tatizo bila kuathiri kanuni, sheria na taratibu zilizopo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama, dada yangu, tena juzi tu kapata ushindi kwa kweli asininyime mshahara tutashirikiana kulitatua. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naona ameridhika na nyinyi wengine mliosimama, natumaini hamtaki kuuliza hili hili tu la hawa watumishi ambao hawajaingizwa kwenye *payroll*. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Esther Nyawazwa halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate ufafanuzi mdogo katika *vote* hiyo hiyo ya 32 kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuajiri walimu na Waganga, Serikali imejipanga vizuri sana kuwapata hao wanafunzi kutoka kwenye Vyuo Vikuu wanapomaliza mafunzo yao: Je, sasa Serikali hatuwezi kujipanga tena vizuri wanafunzi wetu wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu na nafasi hizo tunazo Serikalini, kwa nini basi Serikali isiende kuwachukua walioshinda vizuri kwenye vyuo moja kwa moja kuliko kutoa ajira kwenye magazeti ukizingatia kwamba wanapomaliza mafunzo yao wanarudi vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kazi kwa kuanzia huwa tunafanya kwa ushindani. Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu wenyewe tunawachukua moja wa moja kwa sababu watumishi waliopo katika soko hawatoshlezi mahitaji yetu, ndio maana tunawachukua na kuwapangia kazi. Lakini baadhi ya kada wako wengi kiasi kwamba

ukisema tu uwachukue wote kama walivyomaliza, wengine utakuwa huna pa kuwapeleka kwa kutegemeana na mahitaji ya kila ofisi za Serikali.

Kwa hiyo, bado tutaendelea kutangaza katika magazeti kwa ushindani, isipokuwa sasa hivi tunachokifanya, kwa mfano watumishi kama Wahasibu tumewaomba wenzetu wa Wizara ya Fedha iwe inatangaza mara moja, inawafanyia usahili, halafu sasa wanakabidhiwa TAMISEMI inawapangia pamoja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Kilimo na TAMISEMI na wenyewe wamekubaliana kwamba na wanaomba iwe inatangazwa Wizara moja, ikiwapata iwe inawagawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ni kwamba mimi siombi upendeleo wa hawa wafanyakazi wapatikane, ninachoomba, kwa nini Serikali isiwasimamie badala ya watoto wa kule vijijini kuhangaika kutafuta magazeti, kutafuta hizo nafasi za kazi, Serikali ikaenda kwenye Vyuho Vikuu hivi ikawasimamia kwa nafasi hizi chache ambazo zinapatikana zinaandikwa kwenye gazeti, Serikali ikawasimamia kuwapatia ajira kuliko watoto kuhangaika kwenye magazeti? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Nadhani anachopendekeza Mheshimiwa Waziri ni habari hii iwafikie kabla hawajarejea tu vijijini.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka huu tunategemea kuanzisha Sekretarieti ya Ajira ambayo tutakuwa tuna-*data* za vijana wote ambao wanamaliza Chuo Kikuu na Vyuho mbalimbali. Kwa hiyo, itatuwezesha kuwatambua hata wale ambao wako vijijini kwa sababu tutakuwa na taarifa zao zinazoonyesha kwa kiasi gani wame-*pass*, kwa hiyo, tutakapokuwa tunayahitaji, nadhani itaturahisishia hayo anayoyazunguma.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* ya 32 kifungu kidogo 250.

MWENYEKITI: Sasa naomba hiyo msiirudie, najua wote mko humo humo, hebu tuokoe muda, nenda kwenye hoja sasa.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka tu kupata maelezo kwamba Mheshimiwa Waziri anafahamu kuwepo au kutokuwepo kwa Halmashauri ya Mji wa Mpanda na kwa nini haikuonekana katika jedwali namba mbili ya mgao wa fedha za *TASAF* na kama alikuwa hafahamu kwamba kuna Halmashauri ya Mji wa Mpanda, naomba afahamu hivyo kwamba tuna Halmashauri ya Mji wa Mpanda na ananiahidi nini katika mgao ufuatao wa *TASAF*?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu uwepo wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda, lakini nadhani kwa vile ndio kwanza huo Mji umezaliwa karibuni ndio maana labda haukuonekana peke yake, lakini napenda nimuahidi kwamba kadri siku zinavyozidi kuendelea mbele, huo Mji utaonekana. Lakini haina maana kwamba kutokuonekana hautakuwa umetengewa pesa, nadhani watagawana na kule ambako wametoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SUSANA A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siko kifungu hicho, kwa hiyo, niko 260800 inayohusu *training expenses*. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu watumishi kutoendelezwa kitaaluma na hivyo kuwafanya wafanye kazi zao chini ya kiwango, lakini pia kutopata *promotion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naangalia, naona kwamba katika kipengele hicho cha kasma ya *training* mwaka jana walipata shilingi milioni 66 lakini mwaka huu hawana senti hata moja. Sasa nilikuwa naomba kuuliza, ni kwa nini iko hivi? Ina maana Wizara ya Utumishi ambayo kwa kweli ndio utumishi mkuu haiwezi kuwaendeleza watumishi wake? Lakini pia nimeangalia kipengele kingine kinachohusu *training* nikadhani labda hela zitakuwa kule, lakini nimekuta ni shilingi milioni tatu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ufafanuzi, kuna sifuri pale kwenye 260800 chini ya *sub-vote* 101.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya mafunzo Idara ambayo inashughulika na mafunzo katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni ile ya *Human Resource Management*. Kwa hiyo, hapa hili ni fungu la utawala, lakini hata hivyo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili fungu analoliona hapa la kwanza ni kwa ajili ya Ofisi ya Utumishi peke yake na siyo kwa ajili ya watumishi walioko nje.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilielewa hivyo hivyo kwamba ni kwa ajili ya watumishi walioko pale na ndio sababu nikasema mwaka jana nimeona walikuwa wamepata fedha hiyo shilingi milioni 66 lakini mwaka huu hakuna. Kwa hiyo, ndio nilikuwa nahoji: Je, Wizara hiyo ambayo ndio kioo cha watumishi haioni ni muhimu kuwaendeleza watumishi wake pale Makao Makuu? Ndio lilikuwa swali langu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni ukata au inakuwaje sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za mafunzo zimetengwa, lakini mafunzo kama unavyofahamu ni maendeleo kwa hiyo, zitakuwa kwenye miradi ya maendeleo kwenye kitabu tutakachokifuata.

MWENYEKITI: Sasa umekaribisha tena kwenye kitabu cha nne, tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nipo kwenye *vote* hiyo hiyo, wakati nachangia hotuba hii niliomba Serikali itufahamisha kwamba imechukua hatua gani au imefanya nini kuhusiana na watumishi wa Hospitali ya Mwananyamala waliosababisha kifo cha mama mjamzito, Marehemu Teddy Biloso siku ya tarehe 01 Juni, 2008 na hasa baada ya watumishi wengine wa hospitali hiyo hiyo kusema kwamba kuna uzembe mkubwa pale na wako tayari kutoa ukweli na uwazi na waliomba Serikali iunde Tume ili waweze kupatiwa nafasi ya kuweza kusema yale ambayo wanaweza kutoa kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind-up* sijaona lolote amegusia kuhusiana na suala hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, sijui unalo au lisubiri Wizara ya Afya!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili mahali pake haswa ilikuwa ni Serikali za Mitaa, wakati wa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini hata hivyo, linafanyiwa kazi na kwa sisi ambao tunamsikia yeye kwa sababu vyombo vya habari vilishakiri kwamba yule mama hakufia mapokezi, alifia wadini na alikuwa na uchungu mgumu sijui, kwa hiyo, taarifa na hatua nadhani zinafanyiwa kazi na wenzetu wa TAMISEMI.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia niliomba Waziri atueleze hatua ya wazee wastaafu na hasa wastaafu wa iliyokuwa Afrika Mashariki wakati ule ambao kwa siku nyingi wameelekea kuteseka na siku za karibuni wameelekea kwenda kupiga kambi hata Ikulu na siku za karibuni zaidi wametangaza na kuomba hata Watanzania wenye mapenzi mema kuwapatia chakula wakapopiga kambi Ikulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafahamu na nilieleza kwamba huko nyuma kulikuwa na kauli ya Rais mstaafu wa awamu ya tatu na baadaye kukawa na kauli vilevile ya Waziri wa Fedha wa wakati ule alipotangaza kwamba watalipwa kiwango, lakini baadaye kiwango kile kilibadilika. Sasa ninajua kwamba majibu haya kwenye kipindi hiki inawezekana yasiwe rahisi kupatikana, niliomba Waziri akubali kwanza kama ni kweli tatizo hili lipo, lakini kama lipo: Je, yuko tayari kutoa tamko sasa kwa Bunge hili katika nafasi maalum ili Bunge lifahamu ni tatizo gani limewakumba hawa wazee wetu? Hawa ni wazee wetu wengi, wao wako kwenye hali mbaya kiafya, wengi wamezeeka na wengine wanakufa, lakini wanapokwenda kupiga kambi Ikulu sio aibu tu

kwa Ikulu ni aibu kwa Bunge, aibu wa Taifa, ni sisi sote katika umoja wetu tunaibika kwamba hatuwajali wazee wetu. Nilitaka kujua kwanza kama tatizo hilo lipo, lakini la pili ni lini Waziri basi alipatie taarifa ya kina Bunge hili tujue tatizo hasa ni nini na Bunge liweze kushauri?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri una taarifa yoyote ya kulipatia Bunge?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni ile ile ambayo alitoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hili ni la Wizara ya Fedha. Mimi sina taarifa zaidi ya ile ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu liko kwake, kwa hili la Afrika Mashariki.

MWENYEKITI: Nadhani Serikali imsaidie hapa kwa sababu kama anavyosema, sasa kama wanapiga kambi Ikulu lazima Serikali iwe na maelezo fulani, haiwezi kuwa hakuna maelezo. Mimi naona kwa haki kabisa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba wastaafu wote wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikuwa ni 41,000, mpaka mwaka 2007 wastaafu 30,700 wameshalipwa na wastaafu 6,336 kama nilivyoeleza *cheque* zao zilikuwa zipo na hazijachukuliwa. Kwa hapo, utaona kwamba waliobakia ni kama elfu tatu na kidogo, ni wachache tu. Lakini lazima tufahamu kwamba nani ambaye anapaswa kulipwa kama ni mstaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kwanza, wale waliomaliza wakati Jumuiya inavunjwa tarehe 30 Juni, 1977, waliomaliza kabla ya tarehe hiyo hawapaswi kulipwa kwa kuwa walishalipwa wakati walipostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, vibarua hawapaswi kulipwa. Wako vibarua wengi walikuwa wanafanya kazi katika Jumuiya hizi, lakini kwa sababu hawakuwa na mikataba, wale hawapaswi kulipwa. Serikali inakubali kwamba wapo wastaafu karibu 3,000 ambao hao ndio tuliosema bado pesa zipo, waje ili tuweze kuona *documents* zao. Tatizo lililokuwepo, *documents* hizi baadhi ya mashirika hawakuziweka vizuri na baadhi ya *documents* hazikuwa na picha. *Documents* zote hazikuwa na picha, kwa hiyo, kumtambua inataka subira, uweze kwenda awamu kwa awamu mpaka uhakikishe kwamba huyu ndiye ambaye napaswa kulipwa. Baadhi ya wastaafu wengine wamefariki, warithi wanakuja, kambi mbili lazima ufanye suluhu kambi gani ichukue ile mirathi, lakini tunakubali kwamba wapo wastaafu karibu 3,000 tunawaita waje tualipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema, sio lazima wanifuata mimi Wizarani, tuna *treasury* ziko katika kila Mikoa waende huko watakapokuwa na tatizo kama wao ni wananchi kwa kukimbilia ni kwa Waziri. Waziri ni mwanasiasa, lazima awasikilize, kwa hiyo, sisi tuko tayari kuwasikiliza na fedha zipo na tutawalipa na hili jambo tunataka limalizike. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nadhani taarifa hii ni nzuri. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kuna zaidi ya hapo?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zaidi ya hapo. Taarifa aliyoeleza Mheshimiwa Waziri ni upande mmoja tu wa kile nilichokisema, kama nilifuatiliwa na Serikali vizuri nilieleza kwamba Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu alitamka kiwango na kama sikosei ni shilingi bilioni 400 wanalipwa wastaafu wale. Mheshimiwa Basil Mramba akasema watalipwa shilingi bilioni 40 na zilizobaki wataendelea kulipwa kidogo kidogo. Walizolipwa ni kidogo chini ya hapo, kwa hiyo, sasa tuna matatizo mawili.

Tuna tatizo la hawa 3,000 anaowasema Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kuna wale wote katika ujumla wao ambao hawakubaliani na kiwango kilicholipwa kwa sababu viwango hivi vilikuwa kimoja kwa Afrika ya Mashariki nzima, Kenya wamelipwa kiwango sahihi, Uganda wamelipwa kiwango sahihi, Watanzania hawakulipwa kiwango chao na wamelalamika kwamba kuna wengine wamelipwa hata *cheque* ya shilingi 133 kiwango ambacho hakistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndio nilikuwa ninaomba kwamba kwa wakati muafaka ni vyema Bunge hili sasa likaarifiwa, suala hili sio la kurushiana na Mheshimiwa Waziri, anasema ni la Wizara ya Fedha, lakini ninaomba nimwambie suala limefika kwa Rais, Ofisi ya Rais Katibu Mkuu Kiongozi ndiye anayeandika, sasa barua anaandikiana na hawa. Kwa hiyo, suala sio tena la Wizara ya Fedha peke yake kwa sababu Rais Mstaafu alishatolea kauli. Kwa hiyo, mimi nadhani Serikali ikubali kwamba italetta taarifa ya kina ya mgogoro mzima huu ili tuletewe mchakato wote tangu wakati hawa wastaafu walipostaafu, taratibu zote za malipo walivyolinganishwa na wenzao wa Afrika Mashariki fedha hizi zililipwa na Uingereza kama sikosei au na nchi fulani zikawekwa mahali. Kwa hiyo, kiwango walicholipwa ni tofauti na kile wanachotakiwa kulipa leo kwa sababu wamecheleweshewa zaidi ya miaka 20. Sasa haya ni madai makubwa, kwa hiyo, ni vyema Bunge likaarifiwa kikamilifu ili Bunge liweze kusimamia na kushauri Serikali inavyotakikana.

MWENYEKITI: Nitatoa wakati muafaka ili jambo hili liweze kutolewa taarifa. (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri katika mambo ambayo tuliyahoji katika hotuba yetu ya kambi ambayo hayajatamka wala hayajaelezwa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kuhusu...

MWENYEKITI: Kwa hatua hii hayazidi mawili, ndiyo Kanuni inavyosema. Usitaje mlolongo wa mambo.

MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sio haba, hata hayo mawili yanatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu watumishi waliorejesha fomu za mali na madeni ambao ilikuwa ni asilimia 53 tu katika watumishi 4,261 halafu kundi la pili katika viongozi wa kisiasa 2,130 ambao ni asilimia 53.5 waliorejesha kati ya 3,983. Halafu kuna hili kundi la utumishi wa umma 2,734 kati ya 3,400 ambao angalau hao ni asilimia 80. Sasa viongozi gani hawa wa siasa ambao hawakurejesha fomu kama ni Mawaziri, Wabunge au Madiwani? Tultaka utafafanuzi. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hii pensheni, kwa kawaida mtindo wa Serikali huwa inarithi madeni, aidha, kama Serikali hii, Serikali gani, sasa ikiwa kuna Idara imevunjwa na Serikali Kuu au *United Republic* ikachukua jukumu, leo aliyetoka upande mmoja wa Jamhuri unamlipa kiasi kikubwa upande mwingine unamlipa kiasi kidogo kwa madai kwamba alipoingia katika hii Jamhuri utumishi wake ni miaka michache. Hiyo itakuwa siyo haki. Kesho na kesho kutwa tunaweza kuwa tuna Idara hapa, tuna mambo ya gesi na mafuta, *TPDC*, ukaambiwa imeshakuwa na sura ya Muungano. Watumishi waliotoka upande wa Zanzibar wakaja wakati imeanza kuwa ndio chombo cha Muungano, leo wakaja wakahesabiwa wakati wa kustaafu awe analipwa kidogo kuliko mwenzake wa Bara. Hiyo siyo kutenda haki. Naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Menyekiti, naomba nifafanue hili la pili. Lile la kwanza la fomu nadhani fungu ambalo lilikuwa linahusika lilishapita, ni fungu 30, hili ni fungu 94.

MWENYEKITI: Ni kweli, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa alighafilika, kwa hiyo, hilo limepita. Huyu Waziri makini sana, anaangalia mambo haya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pensheni kwamba mtu ambaye amefanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, baadaye ikaja ikaunganishwa ikawa katika Muungano na kwamba pensheni analipwa nusu na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na nusu analipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ndivyo sheria ilivyo. Hata huku Bara wako watumishi ambao wanafanya kazi Serikali za Mitaa, baadaye wanahamishwa wanakwenda kufanyakazi Serikali Kuu, kwa hiyo, kila mfuko unamlipa.

Kwa hiyo, kipindi ambacho ametumikia akiwa Serikali za Mitaa atalipwa na mfuko wa Serikali za Mitaa na kipindi kile ambacho amefanya kazi Serikali Kuu, atalipwa na mfuko wa Serikali Kuu. Kule atalipwa na *LPF* na huku atalipwa na *PSPF*. Kwa hiyo, sio suala la nchi, ni suala la mifuko kwa sababu hatuna sheria ambayo inaturuhusu kuhamisha mafao kutoka mfuko mmoja kuja mfuko mwingine.

MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba hakuna hiyo *section* ya kulipwa huko, hawana mfuko mwingine, yaani hicho chombo kilivunjwa upande mwingine. Chombo ni kimoja tu, sasa hakuna suala la kwamba labda nusu walipwe huku na nusu walipwe huku, hakuna kitu kama hicho.

MWENYEKITI: Nadhani Serikali ya Muungano italiangalia na nadhani Mheshimiwa Mohammed Mnyaa mlifuatilie takwimu zipatikane. Nina hakika Serikali ni sikivu na tunaweza kupata ufumbuzi bila shaka.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliafikiwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko Yake)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i> Shs. 169,886,600/=
Kifungu 1003 – <i>Information, Education and Communication...</i> Shs. 36,744,600/=
Kifungu 1004 – <i>Procurement Management Unit</i> Shs. 37,481,100/=
Kifungu 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> Shs. 27,920,700/=
Kifungu 2001 – <i>Policy Development</i> Shs. 452,660,000/=
Kifungu 2002 – <i>Management Service</i> Shs. 210,128,900/=
Kifungu 2003 – <i>Establishment</i> Shs. 577,218,300/=
Kifungu 2004 – <i>Ethics Division</i> Shs. 122,012,600/=
Kifungu 3001 – <i>Human Resources Development</i> Shs. 642,247,700/=
Kifungu 3002 – <i>Civil Service Training Centre</i> ... Shs. 1,181,270,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu 3003 – *Tabora Secretarial College*... .. Shs. -

Kifungu 3004 - *Gender* Sh. 51,410,300/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub-Vote 3004*. Ninaomba ufafanuzi mdogo tu. Nimejaribu kuangalia kwenye kitabu tena kwa Wizara zote, sijaona mahali popote kwenye fungu linalosema *gender* peke yake ila nimeangalia kwenye maendeleo ya jamii na jinsi imeandikwa *Gender Development*. Sasa hii *Gender* kwa Wizara hii ni *Gender* kwa kufanyia nini?

Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwamba katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma tuna kitengo cha *Gender* na Anuai za Jamii.

Kwa hiyo, sisi shughuli yetu hasa hapa ni kuhakikisha kwamba masuala ya wanawake, watu wenye ulemavu na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanasaidiwa ikiwa ni pamoja na kwamba tunatoa mafunzo ya Uzamili kwa Watumishi wanawake ili kuwajengea uwezo wa kuweza kushika nafasi za juu za maamuzi na kuweza kuhimili ushindani na pia tunatoa miongozo kwa Wizara nyingine jinsi ya kuweza kuendeleza watumishi wanawake na pia wenye ulemavu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 4002 – *Management Information*

System... .. Sh. 115,673,100/=

Kifungu 4003 – *National Achieves... .. Sh. 388,809,200/=*

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kifungu 1001 – *Administration and General... .. Sh. 1,746,831,000/=*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, kwenye kitu gani sasa?

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa mwenyekiti, *Vote 33 Program 10 Sub-vote 1001* na pia hoja ambayo Mheshimiwa Mnyaa aliizungumza haikuwa imepita, ndiyo imefika wakati wake sasa. Kwa hiyo, nalichukua lile swali la Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa naliuliza. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto siyo mahali pake kwa sababu hii ni mishahara ya Watendaji na Mwenyekiti wa Tume na hatuwezi kutumia mishahara kuhoji kitu kama hicho. Mheshimiwa Grace Kiwelu!

MHE. GRACE S. KIWELU : Mheshimiwa Mwenyekiti lilikuwa ni swali hilo hilo.

MWENYEKITI: Mrejee kwenye Kanuni. Mshahara ni wa Waziri tu, hao ndiyo wanawajibika hapa. Hatuwezi kuchukua mishahara ya Mkurugenzi wa Tume, Sekretarieti na Kadhalika. Tunaendelea !

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 66 - Ofisi ya Rais Tume ya Mipango

Kifungu 1001 – <i>Administration and General</i> ...	Sh. 1,674,455,100/=
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 381,432,900/=
Kifungu 1003 – <i>Policy Information Development</i>	Sh. 498,149,900/=
Kifungu 1004 – <i>Information, Communication and Education</i>	Sh. 475,209,300/=
Kifungu 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 134,555,900/=
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 328,515,700/=
Kifungu 2001 – <i>Macro – Economy</i>	Sh. 1,395,287,900/=
Kifungu 2002 – <i>External Sector</i>	Sh. 1,408,229,300/=
Kifungu 2003 – <i>Infrastructure Services Cluster</i>	Sh. 1,349,731,700/=
Kifungu 2004 – <i>Social Services and Demographics Cluster</i>	Sh. 1,470,246,600/=
Kifungu 2005 – <i>Internal Trade and Economic Relations CL</i>	Sh. 1,023,070,100/=
<i>(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)</i>	

Fungu 94 - Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma

Kifungu 1001 – <i>Administration and General</i>	Sh.1,951,684,600/=
Kifungu 2002 – <i>Local Government Services</i>	Sh. 355,896,800/=
Kifungu 2002 – <i>Local Government Servive</i>	Sh. 496,541,700/=
Kifungu 2003 – <i>Teachers Services</i>	Sh. 3,700,000,900/=
Kifungu 2004 – <i>Fire and Immigration Services</i>	Sh. 56,570,000/=
Kifungu 2005 – <i>Health Services</i>	Sh. 335,055,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 30 - Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) sasa tutapitisha bila kuhoji chochote sasa, kwa sababu zimebaki dakika 10 katika zile 10 tena za nyongeza.

Kifungu 1003 – *Policy and Development*

Division... Sh. 59, 744,657,600/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 32 - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Kifungu 1001 – *Administration and General...* ... Sh. 3,437,791,100/=

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* Sh. 45,400,000/=

Kifungu 1003 – *Information, Education*

and Communication... Sh. 149,400,000/=

Kifungu 1004 – *Procurement Management* ... Sh. 149,400,000/=

Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* Sh. 7,600,000/=

Kifungu 2001 – *Policy Development* Sh. 1,546,630,000/=

Kifungu 2002 – *Management Services...* Sh. 1,021,783,000/=

Kifungu 2003 – *Establishment* Sh. 714,724,900/=

Kifungu 2004 – *Ethics Division* Sh. 247,105,000/=

Kifungu 3001 – *Human Resources*

Development Sh. 1,120,950,000/=

Kifungu 3002 – *Civil Service Training Centre* ... Sh. 421,000,000/=

Kifungu 3004 – *Gender...* Sh. 259,000,000/=

Kifungu 4002 – *Management Information System*. Sh. 2,247,882,000/=

Kifungu 4003 – *National Archives* Sh. 2,887,205,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kifungu 1001 – *Administration and General* Sh. 210,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila mabadiliko yoyote)

Fungu 66 - Ofisi ya Rais Tume ya Mipango

Kifungu 1001 – *Administration and General* Sh. 300,000,000/=

Kifungu 1003 – *Policy Information Development* Sh. 418,163,000/=

Kifungu 1004 – *Information, Communication and Education*. Sh. 200,000,000/=

Kifungu 2001 – *Macro Economy* Sh. -

Kifungu 2002 – *External Sector*... .. Sh. 200,000,000/=

Kifungu 2004 – *Social Service and Demographics Cluster* Sh. 100,000,000/=

Kifungu 3001 – *Social Services and Human Resources Dev* Sh. -

Kifungu 3002 – *Poverty Eradication* Sh. -

Kifungu 3003 – *Economic Empowerment* Sh. -

Kifungu 5001 – *Public Investment Planning* Sh. -

Kifungu 5002 – *Growth Strategies* Sh. -

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
Fungu 94 - Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma

Kifungu 1001 – *Administration and General...* ... Sh. 104,000,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, nakuomba utoe taarifa ya Kazi ya Kamati.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa ya kazi ya Kamati, wakati nawatambua waliochangia kwa maandishi nilimsahau Mheshimiwa Godfrey W. Zambi.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu lililokaa kama Kamati ya Matumzi limekamilisha jukumu lake kwa kuyapitia makadirio na matumizi ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja!

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kesho wanatakiwa Wabunge wafuatao kwenda katika uwanja wa Jamhuri. Hii itakuwa ni alfajiri nadhani. Nao ni *Captain* wa Timu Mheshimiwa Said Nkumba, sijui ni timu ya kitu gani hii.

Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, kha! Huu mchezo gani huu? Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatale, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy. Kesho katika uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi. (*Kicheko/ Makofi*)

Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba kwamba hapo nje kutakuwa na basi la kuwachukua Wajumbe wa Kamati kuwapeleka *Dodoma Hotel* kwa hafla iliyoandaliwa na Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Kutakuwa na basi la kuwachukua kwa sababu wao ndiyo Kamati yao.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi mliyoifanya, tutaendelea na mshikamano huo. Kwa hiyo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.45 jioni *Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 2 Julai, 2008 Saa 3.00 Asubuhi*)